# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 26 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 692

**Upungufu wa Walimu Wilaya ya Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:

Je, kuna upungufu kiasi gani wa walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na upi mpango wa kuondoa upungufu huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na halmashauri nyingine nchini na imekuwa ikiajiri walimu wa shule za msingi na sekondari ambapo katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 jumla ya walimu 29,879 waliajiriwa wakiwemo walimu 16,598 wa shule za msingi na walimu 13,281 wa shule za sekondari. Katika kipindi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilipangiwa walimu 213 kati yao walimu 145 wa msingi na walimu 68 wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu ili kupunguza upungufu uliopo zikiwemo shule za Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba katika hao walimu 12,000 watakaoajiriwa watapewa kipaumbele maeneo ya pembezoni kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ambako walimu wengi wanahama sana kuliko kuhamia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali inaendelea kuajiri walimu kila mwaka, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza motisha na kuboresha mazingira ya maeneo ya pembezoni ili kuvutia walimu na kubaki katika maeneo ya pembezoni na kupunguza walimu kuhama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake la msingi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira hizi za walimu 12,000, walimu hawa wanatarajiwa kuajiriwa kwa kuzingatia idadi yao, lakini pia kuzingatia uwiano na uhaitaji. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwa sababu Serikali mpango wake ni kuhakikisha kila eneo, mkoa, jimbo na kila shule yenye uhitaji inapata mgao, basi nikuhakikishie na wewe Mheshimiwa Mbunge katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru shule zako zenye uhitaji na zenyewe zitapata walimu hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufundishia katika maeneo ya vijijini. Kupitia miradi ya *BOOST, SEQUIP, GPE, TSP* na *EP4R,* Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana ya kujenga nyumba za walimu ili kuboresha mazingira hayo ya kufanyia kazi, lakini pia imekuwa ikihakikisha huduma zinapatikana kwa mfano umeme unapatikana kupitia *REA* (Umeme wa Vijijini); huduma za maji kupitia *RUWASA* na imekuwa ikihakikisha barabara za *TARURA* na zenyewe zinajengwa, lakini huduma za msingi kama afya zinapatikana kwenye maeneo ya vijijini. Yote hiyo ni kutengeneza mazingira mazuri ili walimu wanaopangwa kufundisha katika maeneo ya vijijini waweze kufanya kazi katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuendelea kuzisisitiza halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinafanya msawazo wa walimu ili wale walimu wanaokuwa wamejazana katika shule za mijini waweze kusawazishwa na kuweza kuhamishwa kwenye maeneo ya shule zilizopo vijijini ambazo mara nyingi zinakuwa na upungufu mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelewa, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru.

**SPIKA:** Hili swali lingine ni la kwako au ni Mheshimiwa...? Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, sasa aulize swali lake.

Na. 693

**Uwiano Sawa Katika Bajeti za Halmashauri**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha ili kuweka uwiano sawa katika bajeti za halmashauri ambazo zinasaidia katika ujenzi wa vituo vya afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mhehshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tofauti ya uwezo wa halmashauri kujiendesha kutokana na uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri. Hivyo, imezigawa halmashauri kwenye madaraja kwa kuzingatia uwezo wake wa kukusanya mapato na utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitenga halmashauri kwenye madaraja kulingana na kiwango cha makusanyo ya fedha za mapato ya ndani kwa asilimia za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, halmashauri zilizopo Daraja D huchangia 20%;

Daraja C huchangia 40%; Daraja B huchangia 60% na halmashauri za Daraja A zinachangia 70%.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuziwezesha halmashauri zenye uwezo mdogo wa kukusanya mapato ili ziweze kujiendesha na kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa nini Serikali inatoa kiwango cha bajeti za ujenzi wa vituo vya afya sawa wakati mazingira yanatofautiana? Kwa mfano, ukiangalia Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kama ujenzi unafanyika mchanga unapatikana Iringa Mjini ambako ni mbali sana. Ni kwa nini mnatoa *flat rate* katika utoaji wa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, halmashauri zile ambazo mnasema zipo Daraja D mtazisaidiaje ili ziweze kupata vituo vya afya na wenyewe waweze kuhudumiwa na Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza, ni kweli kwamba halmashauri zinatofautiana uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na shughuli za kiuchumi katika halmashauri hizo, lakini pia *potential* ya vyanzo vya mapato katika kila halmashauri zinatofautiana na ndiyo maana Serikali; kwanza kwa kutambua tofauti hiyo, kuna baadhi ya halmashauri zinazotoa ruzuku zaidi kuliko halmashauri ambazo zina uwezo mzuri zaidi wa kukusanya mapato, yaani kuna baadhi ya halmashauri zinapewa fedha za miradi zaidi, kwa mfano zipo ambazo hazina uwezo wa kujenga vituo vya afya kwa mapato ya ndani. Kwa hiyo, halmashauri

kama hizo fedha zote za ujenzi wa vituo vya afya, hospitali za halmashauri na zahanati zinatoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, yapo majiji ambayo yana uwezo wa kujenga kituo cha afya na hospitali za halmashauri kwa mapato ya ndani. Kwa hiyo, Serikali inapeleka fedha kidogo kutoka Serikali Kuu na kiasi kikubwa cha fedha zinapatikana katika mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spima, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua halmashauri zinatofautiana uwezo na katika bajeti za Serikali za kila mwaka kiwango cha fedha zinazopelekwa kwenye halmashauri zenye uwezo mdogo ni kikubwa zaidi kuliko fedha zile ambazo zinapelekwa kwenye halmashauri kubwa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kulingana na *population* ya eneo husika, lakini pia na uhitaji wa vituo vya huduma za afya na miradi mingine ya maendeleo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na fedha kupelekwa kwa usawa, kimsingi tumekuwa na uzoefu kwamba kwa zaidi ya 95% kwa mfano madarasa 15,000 ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zaidi ya 99% tulipeleka shilingi milioni 20 na madarasa nchi nzima yalikamilika. Kwa hiyo, bado tunajua kuna *discrapance* (utofauti), tumeendelea kuboresha kwamba kuna maeneo ya usafiri ni changamoto zaidi na kuna maeneo mengine *material* ni changamoto, tutaendelea kuboresha kwa utaratibu huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Saashisha Elinkyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 694

**Utaratibu wa Nchi Kuwa na Mipango ya Muda Mrefu**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kunakuwa na mpango wa maendeleo walau wa miaka 50 pamoja na kuwa na vipaumbele vya Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Stanslaus Haroun Nyongo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutoa majibu kwa upande wa Serikali, naomba uniruhusu kwa dakika moja nitoe maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na mpaka leo tuko hapa, lakini nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua katika nafasi hii kumsaidia katika ofisi yake na hasa katika kusimamia masuala ya mipango na uwekezaji, lingine nikushukuru sana, maana malezi yako yamenifanya niwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niendelee kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Maswa Mashariki kwa sababu nao ndiyo wamenifanya niweze kufika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, basi sasa kwa niaba ya Waziri wangu wa Mipango na Uwekezaji naomba nijibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajenda ya maendeleo ya Taifa letu inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambapo utekelezaji wake umegawanyika katika mipango ya

maendeleo ya muda wa kati na muda mfupi, vilevile inaainisha vipaumbele vyake. Utekelezaji wa Dira ya mwaka 2020/2025 unatarajiwa kufikia ukomo wake mwezi Juni, 2026.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kuwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kipindi cha miaka 25 unajengwa katika sababu kuu mbili; kwanza, ni wastani wa idadi ya miaka ya kizazi kimoja *(single generation)* kipindi cha Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kiasi kikubwa kinawiana na wastani wa umri wa kizazi kimoja *(single generation)* ambapo ni kati ya miaka 20 hadi 30 na sababu ya pili, ni uzoefu wa vipindi vya dira ya maendeleo katika nchi mbalimbali ambapo tathmini ya dira za nchi 18 za Afrika na Asia zinazoonesha kuwa wastani wa kipindi cha Dira ya Taifa ya Maendeleo ni miaka 21.

Mheshimiwa Spika, kipindi husika kinaonekana kinatoa fursa ya kuainisha utekelezaji wa mikakati mahususi ya kufikia malengo ya dira pasipo kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko au sababu zilizo nje ya uwezo na wa udhibiti wa nchi husika kwa mfano teknolojia, siasa za kijografia *(geo-politics)* na kadhalika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya kipaumbele cha Serikali ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa viwanda na utoaji wa huduma; je, Serikali haioni ni wakati sahihi sasa kuweka kwenye mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* kinajengewa uwezo ili kiweze kutumia chuma na makaa ya Liganga na Mchuchuma kuzalisha chuma pale *Kilimanjaro Machine Tools?*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa pia ni moja ya kipaumbele cha Serikali kuendeleza rasilimaliwatu, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuweka mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa kutafutia Watanzania ajira nje ya nchi ambazo zinapatikana kwa kiwango kikubwa ili Watanzania waweze

kupata ajira na Serikali iweke *remittance* kutokana na kazi hizo za Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, suala la kuandaa mpango au dira ya nchi ni jambo jumuishi, sasa hivi tunaandaa mpango mwingine wa mwaka 2050. Mpango huu unajumuisha sekta, wadau na wananchi wote na sasa hivi Tume ya Mipango ambayo inatekeleza jukumu hilo inakaribisha wadau na wananchi wote kuweza kutoa maoni. Naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hili tunaliingiza katika mpango huo na litakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuandaa Watanzania kwa maana ya rasilimaliwatu, ni jambo ambalo ni endelevu na sisi katika Mpango wa Taifa tumeliweka katika moja ya mambo ambayo yanashauriwa na tunamuomba sana Mheshimiwa Mbunge atupe ushirikiano katika kutoa ushauri katika jambo hili ili tuweze kuwaandaa Watanzania katika taaluma na ujuzi mbalimbali ambao utaweza kufanya kazi ndani ya nchi, lakini waweze kukubalika hata kufanya kazi nje ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa vipaumbele vya Kitaifa ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, je, upi mkakati wa Serikali wa kuwa na mdahalo mkubwa wa Kitaifa ambao utajadili vipaumbele vitakavyotumika kwa muda wa miaka 50 ijayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hasunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kweli kabisa tuna vipaumbele kama Taifa na lazima tushirikishe wananchi au wadau wote katika kuandaa mkakati huo kwa maana ya kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa letu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumekwishaanza, kupitia ile Tume ya Mipango ambayo iko chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais wetu tumekwishaanza kufanya hizo taratibu na tayari midahalo imekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumetoa njia mbalimbali za kuingiza maoni kwa Watanzania kuleta kwenye Tume ya Mipango. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunamkaribisha katika midahalo hiyo aweze kushiriki pamoja na Wabunge wote ili kutoa mawazo na maoni yao kuelekea Dira ya Taifa ya mwaka 2050.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 695

**Tatizo la Umeme Wilayani Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini changamoto za bei na mgao wa umeme Kata za Mawengi, Lubonde, Lugarawa, Lupanga, Mlangali, Madilu, Milo na Mawengi zitamalizika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mawengi, Lubonde, Lugarawa, Lupanga, Mlangali, Madilu, Milo na Mawengi Wilayani Ludewa zimekuwa zikipata umeme kutoka kwa wawekezaji binafsi *(JUWUMA* na *MADOPE HCL)*. Hata hivyo, Serikali na wawekezaji hao wamefika makubaliano ya kisheria ili miundombinu ya usambazaji umeme katika kata hizo ikabidhiwe *TANESCO* ambapo kwa sasa wapo kwenye hatua ya uwekaji saini makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, hatua hii, pamoja na hatua zote za makabidhiano zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2024. Baada ya hatua hii kukamilika, *TANESCO* watabadilisha mita za umeme ili ziendane na mifumo ya *TANESCO* ili kuanza kutumia umeme wa gridi. Aidha, kuhusu ujenzi wa *line* ya kuleta umeme kwa ajili ya kuziunganisha kata hizi na umeme wa gridi, mkandarasi aitwae *Ok Electrical* ameshafanya upimaji na usanifu wa kina na sasa yupo kwenye hatua ya kuagiza vifaa. Aidha, mkandarasi huyu ataanza kusimika nguzo za kujenga *line* ya umeme mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na hatua hiyo waliyofikia ni muhimu sana. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Swali la kwanza. Sasa hivi Ludewa inakwenda kuwa na viwanda vikubwa sana, lakini bado inategemea *power station* kutoka Wilaya ya jirani ya Madaba. Je, Serikali haioni haja ya kujenga kituo cha kupooza umeme pale Ludewa, ili kupunguza adha kwa wananchi ya kukatika kwa umeme mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ninapenda kufahamu iwapo Serikali ipo tayari kunipa wataalam kutoka *TANESCO* na *REA* niweze kwenda nao Kata za Lumbila na Kilondo ambako bado vijiji vingi havijapata umeme hadi sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninapongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Kuhusu kujenga kituo cha kupooza umeme Ludewa; tutaenda kulifanyia kazi kuona kama uwezekano upo na kama upo basi tutaweka. Kama haupo, kwenye ule mradi wa *grid* imara basi tutaona ni namna gani tutaweza kujenga kituo cha kupooza umeme pale Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafahamu Wananchi wa Ludewa ni wachapakazi sana kwa hiyo, wanahitaji umeme wa uhakika, kwa ajili ya viwanda vidogo na vikubwa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupewa *TANESCO* na *REA,* ili kuhakikisha kwamba, vijiji vya Nsele, Kilondo, Mkanda, Lumbila na Changali wanapata umeme kwa sababu, nafahamu vijiji hivi havina umeme; tulipata changamoto ya mkandarasi, kwa sababu vijiji hivi vipo Mwambao wa Ziwa Nyasa akaona ni vigumu katika utekelezaji, hivyo akaamua kuvirudisha *REA*. Hata hivyo, kwa sababu tulisaini naye mkataba na alifanya *survey* na akakubali mwenyewe kuvifanya, tumekataa yeye kuvirudisha vijiji hivi *REA* na tayari tumeshampa *schedule,* ili atuambie ni lini atapeleka umeme kule, *otherwise* tutamchukulia hatua kali za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuambia mkandarasi huyu ahakikishe anatekeleza mradi kwa wakati. *Otherwise* tutachukua taratibu za Kisheria kuhakikisha ya kwamba na sisi tunapata haki yetu kwa sababu, alisaini mkataba baada ya kufanya *survey* na akahakikisha kwamba, anaweza kupeleka umeme kwenye vijiji hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mwishoni kabisa tutajiridhisha hawezi kupeleka umeme katika vijiji hivi kwa wakati, sisi kupitia *TANESCO* na *REA,* tuna uwezo wa kupeleka umeme kwenye vijiji hivi. Kwa hiyo, tutachukua hatua zote za kisheria kuhakikisha umeme unaenda, lakini kama hataweza kupeleka kwa wakati

tutafanya wenyewe. Vilevile, tutamchukulia hatua kali za kisheria. Hatuwezi kukubaliana na wakandarasi wababaishaji. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi kwa hakika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 696

**Kukamilisha Usambazaji wa Umeme wa REA – Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa Umeme wa *REA* katika Kata na Vijiji 23 vya Jimbo la Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbulu Vijijini lina jumla vijiji 76 ambapo kati ya hivyo, vijiji 70 vimekwishapatiwa umeme kupitia miradi iliyotekelezwa na *REA*. Kazi ya ujenzi wa njia za kusambaza umeme katika vijiji sita vya Maheri, Gembakw, Endanyawish, Domanga, Umbul na Gidaludagau, vilivyosalia zinaendelea kwa sasa, ambapo mkandarasi anaendelea kuvuta waya na kuweka transfoma, ili aweze kuwasha umeme. Tunatarajia vijiji hivi kuwashwa umeme hivi karibuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya Mbulu Vijijini. Swali la kwanza; je, ni lini sasa mtatupatia umeme kwenye vitongoji vilivyobaki kwa sababu, kule ni sawasawa na vijiji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tulikubaliana kwenda kufanya uzinduzi wa kuwasha vijiji hivyo sita, je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa tunakwenda kuwasha hivi vijiji, ili Jimbo la Mbulu Vijijini lipate umeme wa kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Jimbo la Mbulu lina jumla ya vitongoji 361 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 80 ndivyo ambavyo vina umeme. Tutaongeza upatikanaji wa umeme kwenye vitongoji kupitia mradi wa vitongoji 15 vilevile tuna mradi wa ujazilizi pale kwa vitongoji 16. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutapunguza idadi ya vitongoji zaidi kupitia mradi wa *REA* ambao unatarajiwa kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000 kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Samahani, kuna hili swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kuhusu kwenda kuwasha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, nilimuahidi Mheshimiwa Mbunge, tutaenda kuwasha vijiji hivi sita. Kwa kuwa, natambua vijiji vitatu vitakuwa vimekamilika Tarehe 27, vijiji viwili vitakuwa vimekamilika Tarehe 28 na kimoja kitakuwa kimekamilika Tarehe 30 mwezi huu, basi tutapanga, ili kuona namna gani baada ya kukamilika Bunge hili tutaenda kuwasha vijijini kwako, Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa kifupi, moja kwa moja kwenye swali na Mheshimiwa Naibu Waziri majibu pia, kwa kifupi. Muda wetu unakimbia.

Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, mkandarasi anayeitwa Silo anasuasua kupeleka umeme Kijiji cha Kigulu. Yapi ni maelekezo ya Serikali kwa mkandarasi huyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Kuhusu kijiji hiki, tutamsimamia mkandarasi kwa weledi sana kuhakikisha anamaliza kufikia mwezi huu kwa sababu, ndiyo makubaliano ya kumaliza mradi huu ikifika Tarehe 30 ya mwezi huu. Kwa hiyo, namuelekeza Mkurugenzi wa Mradi huu wa *REA* ahakikishe anamfuatilia mkandarasi na kuhakikisha anatimiza kazi yake kwa kadiri ya muda wa mkataba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Kwanza naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo imeifanya kule Arumeru Mashariki, kwa ajili ya kusambaza umeme wa *REA*. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo, ukanda wa mashariki, hususan Tarafa ya King'ori, bado vitongoji vingi viko gizani. Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme wa *REA* kwenye ukanda huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusu hii ya kupeleka umeme huku King'ori; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutapeleka umeme katika vitongoji hivi, kwanza kupitia mradi wa vitongoji 15 na pia, tutaendelea kupeleka kupitia miradi ya *REA* ambayo tunayo kwa Mwaka huu 2025 na kuendelea. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 697

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne Igawa – Tunduma**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka Igawa hadi Tunduma utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Igawa – Tunduma kwa njia nne inajengwa kwa awamu, ambapo sehemu ya kuanzia Uyole eneo la Nsalaga – Ifisi, kilometa 29, ujenzi wake unaendelea na hadi sasa umefikia 15.5%. Kazi za ujenzi zimepangwa kukamilika tarehe 13 Aprili, 2025. Kwa sehemu iliyobaki ya Igawa – Uyole, eneo la Nsalaga na Ifisi – Tunduma zitajengwa kwa utaratibu wa *EPC+ F*. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Isangati ambayo inapita Igogwe, inatokea Mbalizi, kwa maana barabara hiyo ni muhimu sana, mazao mengi sana yapo kule na wananchi wanasumbuka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Bahati nzuri barabara hii naifahamu. Hii barabara bado haijafanyiwa usanifu kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili tuweze kupata gharama na kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Itoni – Lusitu, kilomita 50, imesimama ujenzi na hiki ndiyo kipindi cha kiangazi. Ni lini Serikali itatoa fedha, ili barabara hii iendelee kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli, barabara hii kilometa 50 ilishaanza, mkandarasi yupo *site* na ameshaleta maombi ya malipo, kwa maana ya hati za malipo. Tumeshaziwakilisha Wizara ya Fedha na muda wowote tutapeleka fedha, ili kazi iweze kuanza na aweze kuikamilisha kazi yake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, ni busara zipi za kitaalam au weledi upi wa kitaaluma ambao unaisababisha Serikali kuanzisha na kuibua miradi mipya ya barabara na kuacha viporo, kama ile barabara kutoka Kilosa – Mikumi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hakuna busara wala hekima ambayo imetumika, sana sana ni utaalam tu. Mipango yetu sisi ni kuhakikisha kwamba, tunajenga barabara zote ambazo tumezianzisha na wakati huo huo tukianzisha miradi mipya. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara yake ambayo anadhani ni kiporo, hapana, Serikali inaendeleanayo na tutahakikisha tunaijenga na kuikamilisha barabara hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati tunasubiri Mpango wa *EPC+F* ukamilike, je Serikali iko tayari kurekebisha maeneo korofi ya Barabara ya Mafinga – Mgololo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tumeshatoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Iringa kwa sababu, tunajua barabara hiyo ndiyo inasafirisha mbao na

magogo mengi kwamba wakati tunasubiri mradi huo kuanza ahakikishe hayo maeneo yote ambayo magari yanaweza kukwama anayatengeneza, ili magari yaendelee kupita. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri aliahidi kuunganisha barabara inayotoka Bulige – Ngaya, kipande kile kidogo pale katikati. Sasa, ni lini mpango huo utaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunategemea kuendelea na katika mwaka wa fedha unaokuja utaratibu huu utaendelea, ili kuweza kukamilisha ile ahadi ambayo tuliitoa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Serikali ilitangaza Barabara ya kutoka Kibena – Lupembe itajengwa kwa lami, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Barabara ya Kibena – Lupembe – Kidegembye, kilometa 42, tayari tuko kwenye hatua za mwisho kabisa za kukamilisha taratibu, ili barabara hiyo iweze kutangazwa na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwenye hili swali la msingi, sehemu ya mwisho umesema vipande vinavyobaki kutoka Igawa mpaka Tunduma vitajengwa kwa utaratibu wa *EPC+F,* lakini kilomita tatu kutoka Ifisi mpaka *Airport* zilishaahidiwa kwa hiyo, ni sehemu ya huu mkataba. Kilomita tano kutoka Nsalaga mpaka

Mlima Nyoka nazo zilishaahidiwa hapa. Kwa hiyo, nadhani hii *EPC+F* inahusu vipande vingine ukiacha hizo kilometa zinazokaa hapo katikati kwa maana ya 29 za kutoka Uyole – Ifisi, kilomita tatu kutoka *Airport* na kilometa tano kutoka Nsalaga – Mlimanyoka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, tukiwa hapa Bungeni, Bunge lako Tukufu, inatakiwa pia, kuwepo na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Hata hivyo, tangu tumeanza hapa kuanzia asubuhi, hakuna Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Inaweza ikajitokeza hoja yoyote pale wakashindwa kujibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Esther Matiko hapa ameomba Mwongozo kwamba, Serikali haina uongozi Bungeni. Sasa naona kuna aliyejitolea na amekimbia kwa mbio ambazo kwa kweli, angeweza kushinda riadha. *(Makofi, Kicheko)*

Kwa hiyo sawa, ameenda hapo kumuwakilisha Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Nafikiri hoja ya msingi itakuwa imewafikia, kipindi hiki ni cha Bajeti ya Serikali, mkiwa mnaliomba Bunge liidhinishe fedha za matumizi, mkiwa hampo humu Bungeni inakuwa mtihani kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Esther Matiko, Serikali ipo Bungeni, kwa maana ya Mawaziri wapo, siyo wote, lakini wapo. Wengine sina hakika sana kwa siku kama ya leo kama hawapo Dodoma, lakini nadhani ni utaratibu ambao mmejiwekea wenyewe, kila Waziri anaingia muda anaotaka siyo lazima awepo Bungeni. Sasa hayo mimi siwezi kuingia huko, lakini ni utaratibu mbovu kwa sababu, leo ni siku mnayohitimisha Bajeti ya Serikali kwa hiyo, ni muhimu kuwepo Bungeni. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 698

**Uhaba wa Vitendea Kazi Kituo cha Polisi – Mlandizi**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipatia vitendea kazi kama magari, majengo na shajara Wilaya ya Kipolisi ya Mlandizi, Jimbo la Kibaha Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa spika, Serikali inatambua uhaba wa majengo ya ofisi, vitendea kazi na nyumba za makazi ya askari katika Kituo cha Polisi cha Mlandizi. Tathmini kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za uchunguzi wa kisayansi, intelijensia na upelelezi imeshakamilika na fedha kiasi cha shilingi 82,000,000 zinahitajika. Pia, kiasi cha fedha shilingi 232,590,000 zinahitajika, kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa nyumba mbili za makazi ya askari za familia sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zote hizo kiasi cha jumla ya shilingi 314,590,000 zimetengwa kwenye Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha wa 2024/2025. Kwa sasa kituo cha Polisi Mlandizi kina gari

moja na pikipiki mbili, pindi magari 122 yaliyoagizwa na Serikali, kwa ajili ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya yatakapowasili, Kituo cha Polisi Mlandizi pia, kitapatiwa gari. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa masikitiko makubwa hili swali ninalirudia leo karibu mara ya pili au ya tatu sasa na majibu ya Serikali ni haya. Sasa, naomba nijue kutoka kwa Serikali kwamba, nini tamko la uhakika kabisa kwamba, pesa hizi zitafika na kuweza kutekeleza au kuondoa changamoto hizo ambazo nimezieleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Pale, hili gari ambalo wanalitaja ni moja, kwa ufupi jamani, lile ni lori la mizigo kwa hiyo, ni kazi sana askari kufanya doria kwenye maeneo ambayo yanaendelea na ujenzi kule Kwala, kwenye kongani ya viwanda ya *Morden Park Industries* na maeneo mengine ya Jimbo la Kihaba Vijijini. Sasa nataka nijue, haya magari ambayo yameahidiwa ni lini yanafika na ni wapi wanayakabidhi, ili niweze kushuhudia yakitolewa na wananchi wakipata huduma katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tamko la uhakika ni, ili kudhihirisha kwamba, tumechukua hatua kwanza tulifanya tathmini ya mahitaji ya majengo hayo ambapo, kama nilivyosema, hatua ya pili ni kutenga fedha kwenye bajeti hii ya Mwaka wa Fedha unaokuja wa 2024/2025. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa, tumeshachukua hatua kufanya tathmini, tumetenga bajeti,

naomba nimtoe wasiwasi kwamba, sasa tunaenda kutekeleza miradi hii, kama ambavyo tumeainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu magari; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tayari tumeshaagiza magari 122, kwa ajili ya ma-*OCD* wote nchi nzima. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha gari mtalipata, kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Mlandizi, kama ambavyo umeomba. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona narejea tena, maswali moja kwa moja kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wilaya ya Tanganyika haina Gari la Polisi. Ni lini mtapeleka gari kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari Serikali imeshaagiza magari 122. Kwanza tulishatoa magari 71 kwa ma-*OCD* hapa nchini na sasa hivi wakati wowote magari 122 yanaingia, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kila *OCD* katika nchi hii anapata gari, kwa ajili ya kulinda usalama wa wananchi na mali zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwenye haya magari ambayo unasema umeyaagiza au yameagizwa, kwa Wilaya ya Nyang'hwale tumekuwa na uhitaji mkubwa kwa muda mrefu. Naomba kauli ya Serikali kwenye haya magari na Nyang'hwale itapata? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Nyang'hwale pia, ni Wilaya. Kwa hiyo, watapata gari, kwa ajili ya kulinda mali zao na raia wetu wawe salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa Wilaya hizi zitakazopata Magari ya Polisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nchi hii ina Wilaya 139, tumeshagawa magari 71 na tumeagiza mengine 122. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi kwamba, Wilaya ya Kilindi ni moja kati ya Wilaya zitakazopata gari, kwa ajili ya wananchi wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshasema wilaya zote zitapata, natumaini na Muleba itapata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, lini Serikali itarekebisha majengo na kuweka vitendea kazi katika Kituo cha Polisi cha Wilaya Mbagala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua Mbagala ni eneo ambalo lina wakazi wengi, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Kituo cha Polisi cha Mbagala pia kinapata fedha kwa ajili ya kukarabatiwa ili waweze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itatatua changamoto za magari, pikipiki na vifaa vingine kwenye Kituo cha Polisi cha Ng'ambo – Unguja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tayari tumeshagawa pikipiki 105 mpaka sasa na tunazigawa kwa awamu. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge pia kituo chako ulichokisema tutaweka kwenye mpango ili tuweze kupata polisi kwa ajili ya kutoa huduma katika eneo lako ulilotaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 699

**Kudhibiti Wahalifu Wanaovamia Wavuvi**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti wahalifu wanaovamia wavuvi wakiwa ziwani na kuwanyang'anya mali zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa spika, wajibu wa Serikali ni kulinda maisha ya watu na mali zao. Katika kudhibiti uhalifu wanaofanyiwa wavuvi

wakiwa ziwani, Serikali kupitia Jeshi la Polisi kikosi cha wanamaji hufanya doria kwa kutumia boti na kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limewashirikisha wavuvi na vikundi vya Ulinzi na utunzaji wa mazingira ya fukwe kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili kudhibiti na kupata…

**SPIKA**: Mheshimiwa sogea huku ili mnapozungumza mtumie sauti kidogo. Simama, sogea pale alipo ama Mheshimiwa Waziri aje aketi nawe hapo, itarahisisha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze upya.

Mheshimiwa spika, wajibu wa Serikali ni kulinda maisha ya watu na mali zao. Katika kudhibiti uhalifu wanaofanyiwa wavuvi wakiwa ziwani, Serikali kupitia Jeshi la Polisi kikosi cha wanamaji hufanya doria kwa kutumia boti na kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limewashirikisha wavuvi na vikundi vya Ulinzi na utunzaji wa mazingira ya fukwe kuanzisha vikundi vya Ulinzi shirikishi ili kudhibiti na kupata taarifa za wahalifu wa ziwani. Serikali katika kuhakikisha matukio ya uhalifu unaovuka mipaka ziwani haufanyiki, imeweka utaratibu wa kufanya mikutano ya ujirani mwema kwa mikoa jirani ya nchi zinazotumia ziwa ili kudhibiti uhalifu huo na kupambana na vikundi vya uhalifu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. kumekuwa kuna uhalifu wa wizi wa mifugo kwa maana ya ng'ombe na jambo hili limekuwa likiendeleza na likitia umaskini wananchi ambao ni wafugaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa lengo na dhumuni la

kuanzisha Kanda Maalum Rorya ilikuwa ni kudhibiti wizi wa mifugo kwenye eneo hili na jambo hili limekuwa likiendelea.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kupitia upya Kanda Maalum ya Tarime – Rorya kuifumua na kuunda upya ili kuongeza ufanisi wa kudhibiti uhalifu unaoendelea kwenye eneo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa matukio haya mawili wizi wa mifugo na uvamizi wa wavuvi ndani ya ziwa imekuwa ikiendelea na majibu yamekuwa haya haya kwenye majibu ya msingi. Je, Mheshimiwa Waziri hauoni baada ya Bunge hili kuna umuhimu wa mimi na wewe kuongozana ikibidi na *IGP*, kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, kukaa na wadau na wananchi wanaoathirika na matukio haya mawili ili kuona namna ya kudhibiti na kuongeza ufanisi kwenye maeneo haya kwa ajili ya kulinda usalama wa raia na mali zao ndani ya Wilaya ya Rorya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu wizi wa mfugo, katika Wilaya ya Rorya tayari tushaanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi, lakini nimhakikishie kwamba sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani tumeongeza pia Askari wa Polisi wanaohusika na kuzuia wizi wa mifugo katika Mkoa wa Polisi Kanda Maalum ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu suala la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza tumeongeza boti za doria na tumeshaagiza boti 10. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge baadhi ya boti zitaenda katika eneo lake la Rorya kwa ajili ya kufanya doria katika Ziwa Victoria, lakini pia niko tayari kuongozana naye baada ya Bunge hili kuhakikisha kwamba tunawasikiliza wananchi na kutatua changamoto hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 700

**Mgogoro wa Ardhi Kati ya Gereza la Rusumo na Wananchi**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Gereza la Rusumo na Wananchi wa Kijiji cha Rusumo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa spika, Gereza kilimo Rusumo lipo Wilaya ya Ngara Mkoani Kagera lenye ukubwa wa ekari 9,442.9. Gereza hilo limepimwa na kupata Hati Na.5548 katika mwaka 2023.

Mheshiwa spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inatambua changamoto ya uhitaji wa ardhi kwa wananchi wa Kijiji cha Rusumo na kilichopo ni wananchi kudai majira ya nukta za upimaji ya Gereza Rusumo uliofanywa na Halmashauri ya Wilaya Ngara uliopitiliza hadi kwenye barabara na maeneo ya Hifadhi ya Mto Kagera. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Magereza imeendelea kuchukua hatua mbalimbali vikiwemo vikao vya ujirani mwema na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa ajili ya kushughulikia changamoto hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge mliokaa kwenye viti vya Waheshimiwa Mawaziri, rudini nyuma mpaka tumalize kipindi cha maswali. Waheshimiwa Wabunge mlio upande wa Waheshimiwa Mawaziri, rudini nyuma, Waheshimiwa Mawaziri wasikilize maswali, mtarejea baadaye kidogo tukimaliza kipindi cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *Briefly* tu nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pia kwa kutuma *vehicle* yeye na Ndugu Suzan Kaganda kwenda kutatua changamoto ya leseni Ngara. Nina swali moja la nyongeza

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya majira ya nukta yanayosemwa na Mheshimiwa Naibu Waziri yalitokana na magereza kufanya upimaji bila kuhusisha kijiji wala wananchi wanaohusika maeneo yale na hivyo kuleta matatizo makubwa mpaka kuingilia hifadhi na ardhi nyingine ambayo ipo nje ya nchi *(no man's land)*.

Ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri ataambatana na mimi twende Rusumo, tukae na wananchi tukatatue matatizo ya ardhi kwenye Kijiji cha Rusumo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge la Bajeti tutapanga utaratibu mzuri, twende kwa wananchi tukaisikilize changamoto hii, lakini pia naagiza Jeshi la Magereza kwamba wataalamu wetu watangulie waanze kupima kabisa ili tukifika tumalize mgogoro huu ambao umedumu kwa muda mrefu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 701

**Ukarabati wa Miundombinu ya Maji – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa miundombinu ya maji iliyochakaa na kusababisha upungufu wa maji – Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya majisafi na salama wilayani Chemba, Serikali imekamilisha ukarabati wa Skimu mbili za Maji ya Songolo na Chemba Mjini katika mwaka wa fedha 2023/2024. Uboreshaji huo umerejesha huduma ya maji kwa wananchi 16,084 wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na ukarabati wa Skimu za maji za Humekwa, Mlongia, Soya, Daki, Dalai, Gumbu, Kwamtoro, Kubi, Moto, Chinyika, Kelema Maziwani, Ovada na Churuku. Ukarabati wa skimu hizo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi 13,770 wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kukarabati Skimu za maji za Kelema Balai na Khubunko utakaoboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi 7,906 waishio kwenye vijiji vitatu vya Kelema Balai, Kelema Mashariki na Khubunko katika Wilaya ya Chemba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nina swali moja muhimu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Igunga tumechimba maji mara tatu lakini hatujapata maji ardhini. Tumeomba shilingi 300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuyatoa Ntomoko kuyaleta kwenye Kijiji cha Igunga. Nini kauli ya Serikali juu ya kuleta fedha hizo ili Watu wa Igunga waweze kupata maji? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kijiji cha Igunga baada ya kufanya utafiti na kuchimba maeneo kadhaa tukajiridhisha kwamba hakuna maji. Sasa, Serikali ikaangalia chanzo kilichopo Ntomoko na tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekubali kutoa kiasi cha shilingi 350,000,000 kwa ajili ya kuyaleta maji kutoka Ntomoko kuja katika Kijiji cha Igunga. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wananchi wa Kijiji cha Boma la Ng'ombe ambapo mwenge umepita juzi, walitoa malalamiko makubwa kuhusu upungufu wa maji kwenye Kijiji cha Boma la Ng'ombe. Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji kwenye Kijiji cha Boma la Ng'ombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa kazi kubwa anayoifanya Kilolo.

Mheshimiwa Spika, nimeshafika Kilolo na kujionea changamoto hiyo lakini tunafahamu kwamba Serikali iko katika juhudi mbalimbali za kuboresha na kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji unaendelea kuboreshwa. Tayari tumeshasaini mkataba katika baadhi ya kata, tunaamini kwamba baada ya kukamilika mikataba hiyo na kutekelezwa, basi tutaangalia uhitaji katika maeneo mengine na tutahakikisha kwamba tunapeleka huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni lini Mradi wa Maji wa Lema katika Kata ya Busale wilayani Kyela utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, eneo la Busale – Lema, Serikali imetoa kiasi cha shilingi 223,000,000 na mradi umefika 67%. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika na kutoa huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Namtumbo kwenye Kata ya Mgombasi, Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kujenga mradi wa maji wa shilingi 2,700,000,000. Imejenga vizimba, chanzo cha maji na tanki la maji lakini kuna bomba la nchi nane ambalo halijapatikana…

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa…

**MHE. VITA R. KAWAWA:** …mpaka sasa karibu miezi 10.

Je, Serikali itanunua lini bomba hili la nchi nane ili sasa watu waweze kupata hayo maji? Zaidi ya miezi 10 sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge alichokiongea na amekuwa akifuatilia na sisi (Serikali) tumeshachukua hatua. Tayari tumeshaelekeza ununuzi wa bomba la nchi nane ufanyike haraka ili liweze kwenda kulazwa kwa ajili ya kutoa huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kijiji cha Mtonya Kata ya Likuyuseka Halmashauri ya Namtumbo bado inatumia visima vya pampu ya mkono. Kati ya visima hivyo, 13 viko sawa lakini vitatu ni vibovu. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati kwenye visima hivyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia Bunge lako Tukufu, katika visima hivi 13 na vitatu ambavyo havitoi huduma kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu. Nawaelekeza *RUWASA*-Namtumbo kuhakikisha kwamba ukarabati huu unaanza mara moja na kwa sababu hatuna changamoto sana ya pampu, ili waweze kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo hili la Mtonya waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini mradi wa Mwakaleli *1* na Mwakaleli 2 unaohudumia vijiji nane utaanza kutoa maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nipokee swali la Mheshimiwa Mwakibete ili nikatafute kuona *status* yake imefikia wapi na baada ya hapo tutakutana kwa ajili ya kupeana taarifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 702

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria Kutoka Butiama hadi Nyamuswa – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Butiama kwenda Nyamuswa - Bunda utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambao utatoa maji kwenye tanki la lita 2,000,000 la Mradi wa Mugango - Kiabakari lililoko Wilaya ya Butiama kwenda Bisarye mpaka Nyamuswa wilayani Bunda Mkoani Mara. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 500,000, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 23.1, ukarabati wa vituo 18 vya kuchotea maji pamoja na kuunganisha zaidi ya wateja 2,000 wa majumbani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza naipongeza Wizara ya Maji kwa kunikumbuka kwenye hoja hii ya kutoa maji Butiama kwenda Nyamuswa.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, kwa kuwa usanifu umekamilika na kwa kuwa Bajeti 2024/2025 imetaja kwamba itatekeleza mradi huo. Je, ni bajeti kiasi gani imetengwa ya kutekeleza mradi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna mradi wa vijiji 33 ambapo Serikali imetumia shilingi 800,000,000 kufanya usanifu. Ni hatua gani imefikiwa katika mradi huo wa kupeleka maji katika vijiji 33 kwenye Jimbo la Bunda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Getere amekuwa kinara wa kupambana kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kwa ajili ya wananchi wake. Katika bajeti yetu, usanifu umeshakamilika na utekelezaji utaanza katika bajeti yetu ya 2024/2025. Tayari Serikali imetenga kiasi cha shilingi 2,000,000,000 kwa kuanzia ili kuhakikisha kwamba shughuli ziendelee.

Mheshimiwa Spika, katika suala la pili katika vijiji 33, Mtaalamu Mshauri ameshawasilisha rasimu ya usanifu. Sasa Wizara ipo katika mchakato wa kuipitia rasimu hiyo ili tujiridhishe na hali halisi na baada ya hapo, tutatangaza zabuni za kumpata mkandarasi ili aweze kwenda kutekeleza mradi huo. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kushirikiana naye, kama yeye anavyoendelea kushirikiana na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kutupa visima vidogo vidogo vya maji. Swali langu la msingi, je, Serikali lini itapeleka mradi mkubwa wa maji Wilaya ya Mbogwe ili tukomeshe kabisa suala la uhaba wa maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, wakati tukisoma Bajeti ya Serikali na upande wa *RUWASA*, Mheshimiwa Waziri alielekeza tuchimbe visima 900 nchi nzima tukizingatia kwamba kila Mheshimiwa Mbunge atapata visima vitano. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwaelekeza, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri yapo *clear*, waanze kuhakikisha kwamba mitambo ambayo ilinunuliwa na Serikal, ianze kufanya kazi mara moja ili visima hivi vitano vitano, kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa viwe vimekamilika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shukurani zenu nimeshazipokea. Ili tuukomboe wakati, hamna haja ya kunishukuru nikikupa nafasi ya swali.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba mradi wa zaidi ya shilingi 500,000,000,000 wa maji Arusha, ulilenga kupeleka maji katika Kata ya Mererani, Endiamutu, Shambarai na Naisinyai. Je, ni lini sasa maji yatapelekwa katika Kata ya Shambarai na Naisinyai baada ya kwamba yamepelekwa katika Mji wa Mererani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa maji katika kata ambazo Mheshimiwa Ole-Sendeka amezitaja. Nakuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka baada yakutoka hapa tuonane ili niweze kupata majibu sahihi ya Serikali kwako Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ni upi mpango wa Serikali kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 ili Kata za Mswaha na Mji wa Korogwe na maeneo mengine, yatatue changamoto kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Miji 28 kwa upande wa Mkoa wa Tanga, unaojumlisha Handeni, Muheza, Korogwe pamoja na Pangani wenye jumla ya shilingi 170,000,000,000 umefikia wastani wa 32%. Juzi nilikuwepo kule nimetoa maelekezo kwa wakandarasi kuharakisha mradi huu kwa sababu hakuna changamoto ya kifedha. Kwa hiyo sisi kama Serikali tumeelekeza mradi huu usiwe nyuma ya wakati ili wananchi wa maeneo hayo wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Wilaya ya Meatu ni miongoni mwa wilaya ambazo ni kame sana, kule maji ni tatizo kubwa. Je, ni lini visima hivi vitano vitachimbwa katika Wilaya ya Meatu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Meatu ipo kati ya wilaya tano ambazo zitafikiwa na maji ya kutoka Ziwa Victoria na tayari mradi umeshaanza kwa awamu ya kwanza kwa kujumuisha Wilaya ya Busega, Bariadi pamoja na Maswa lakini katika awamu ya pili, tutaenda katika Wilaya ya Meatu pamoja na Itilima. Tunafahamu kwamba huo ni mradi wa muda mrefu lakini tuna miradi ya muda mfupi ambapo tumeelekeza wataalamu wetu kufanya usanifu wa kupata vyanzo vya maji ili tuchimbe visima na kuhakikisha kwamba wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini mtarekebisha mabomba chakavu katika Kata ya Kilakala – Kigunga ili uhaba wa maji uweze kupotea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, uchakavu wa miundombinu unatusababishia hasara hata sisi Serikali tunapozalisha maji lakini yanafika machache na mengine yanapotea, hivyo kututia hasara kubwa sana. Nilikuwepo Dar es salaam katika Majimbo ya Kibamba lakini nafahamu, natambua kwamba uwepo wa Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Temeke pia tatizo bado lipo lile lile. Nimeishatoa maelekezo lazima sasa tufanye ukarabati wa miundombinu yetu yote ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kupata maji safi na salama lakini pia tunajiepusha na upotevu wa maji ambayo yanasababisha hasara sana katika mamlaka zetu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 703

**Kukamilisha Mradi wa Majitaka Kata ya Olmot – Arusha Mjini**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, lini mradi wa majitaka uliopo Kata ya Olmot ambao utaunganishwa na Kiwanda cha A to Z utakamilika

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Arusha *(AUWSA)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji majitaka wa Olmot utakaonufaisha Kiwanda cha A to Z pamoja na wakazi

1,200 wa maeneo hayo. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 11.8, ujenzi wa nguzo 30 za kushikilia bomba kwenye vivuko na ujenzi wa Chemba 125 za ukaguzi wa mfumo wa majitaka.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba kwa miaka mitatu toka 2021 mpaka 2024 wameweza kukamilisha kiwango cha 40%, lakini anatuambia kwamba kufikia Desemba mwaka huu ambayo imebaki miezi sita tu na kiwango kilichobaki cha kazi ni 60%, je, Serikali ina mpango gani wa ziada kuhakikisha kwamba wanakamilisha 60%?

Swali langu la pili la nyongeza je, kiasi gani cha fedha kimebaki cha kukamilisha mradi huo na Serikali mmejipangaje kupeleka fedha hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua wasiwasi wa Mheshimiwa Mrisho Gambo na natambua wasiwasi huo kwa wananchi wake. Nimtoe hofu Serikali kama ambavyo nimejibu katika majibu ya msingi kufikia 2024 Desemba, mradi huo utakuwa umekamilika na fedha ambazo zitakuwa zimebaki kwa ajili ya kukamilisha mradi huo zitapelekwa kwa wakati sahihi ili kuhakikisha kwamba mradi unakamilika kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Habari,

Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 704

**Usimamizi wa Biashara ya Mitandaoni Nchini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia ipasavyo biashara za mitandaoni nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa biashara za mtandaoni zinasimamiwa ipasavyo, Serikali imetunga sheria za usalama wa mtandao ambazo ni Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015, Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya Mwaka 2015 na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022, ili kuwa na anga salama ya mtandao na mazingira mazuri ya kuwalinda watumiaji wa mitandao. Aidha, tumefanya marekebisho ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya mwaka 2015 pamoja na kuandaa za kanuni za watoa huduma za uidhinishaji ili kuwezesha matumizi ya saini za kielektroniki kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa watumiaji wa mtandao ambayo itawezesha usimamizi mahiri wa biashara mtandaoni.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau tumeandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (2024 – 2034) ambao pamoja na mambo mengine unaweka mazingira mazuri ya biashara mtandaoni ambayo yatazingatia ulinzi, usalama na faragha za watumiaji wote wa bidhaa na huduma ya TEHAMA nchini.

Aidha, tuko katika hatua za kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 ili kuimarisha mazingira ya matumizi ya teknolojia zinazoibukia katika utoaji wa huduma mbalimbali kidijitali ikiwemo biashara mtandaoni. Vilevile, Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara katika ukamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Biashara Mtandao ambao pia utaimarisha biashara ya mtandaoni nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria nzuri zilizopo bado wananchi wanatapeliwa sana kwa biashara za mitandaoni. Je, Serikali haioni haja ya kuandaa elimu mahsusi kwa wananchi kwa ajili ya eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa biashara yeyote nchini ni lazima isajiliwe na ilipiwe kodi. Je, Serikali imejipanga vipi kukusanya mapato kupitia biashara za mitandaoni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatapeliwa sana kuhusu kutoa elimu, sisi kama Wizara tayari tunaendelea kutoa elimu kupitia vyombo vyetu vya habari. Vilevile katika *SMS* wananchi wengi wanaweza wakawa mashuhuda, hata ninyi Waheshimiwa Wabunge *SMS* mbalimbali tunazotumiwa kwamba labda usitoe namba yako ya siri, namba ya siri ile *pin number* ni ya kwako peke yako, hapaswi kuijua mkeo wala mumeo wala watoto ni ya kwako kwa sababu za kiusalama.

Mheshimiwa Spika, vilevile kupunguza kusikiliza maneno ya matapeli. Unapigiwa simu na mtu usiyemjua anakwambia maneno ya kukulaghai na wewe unaendelea kumsikiliza mwisho wa siku unampa ushirikiano. Kwa hiyo, haya yote tunaendelea kuwasihi wananchi kuepuka kusikiliza simu ambazo humjui nani

amekupigia, anakulaghai kwa sababu anafahamu sasa wananchi wako *busy* kutafuta fedha. Kwa hiyo, elimu tayari tunaitoa na tutaendelea kuitoa, nikushukuru sana Mheshimiwa Husna kwa kuendelea kuwa sehemu ya kusisitiza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara yoyote inatakiwa kusajiliwa na kulipa kodi, sisi kama Serikali hakika tunaendelea na mipango mbalimbali kuhakikisha kwamba tunaweza kuwa sehemu ya kuhakikisha kodi inakusanywa kupitia biashara ya mtandao. Pia mikakati yetu mbalimbali kama kuweka mkakati huu wa uchumi wa kidigitali, lengo ni kuona kwamba kwanza tunaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, wakati mimi naapishwa kwenye Wizara hii Mheshimiwa Rais alinipa agizo la kuhakikisha ninashughulikia *unique identification number.* Kwa hiyo, tukiweza kuhakikisha hizi namba zinaweza kutumika, makusanyo ya kodi yataweza kukusanywa vizuri na sisi kama Wizara tutakuwa tumeweza kuchangia katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 705

**Mgogoro wa Mpaka kati ya Hifadhi ya Mpanga na Vijiji Jirani – Wanging’ombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele na Vijiji vya Luduga, Mpanga, Malangali na Wangamiko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Mpanga Kipengele na Vijiji vya Luduga, Mpanga, Malangali na Wangamiko vilivyopo katika Wilaya ya Wanging'ombe umetatuliwa baada ya kutekeleza maelekezo ya Serikali yaliyotolewa kupitia Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta. Maelekezo ya Serikali ilikuwa ni kutoa sehemu ya ardhi ya hifadhi kwa vijiji, kufyeka na kuweka alama za mpaka.

Mheshimiwa Spika, kupitia maelekezo haya, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi, Mikoa ya Njombe na Mbeya ilifanya mapitio ya mpaka wa Hifadhi ya Mpanga Kipengere na kumega eneo lenye ukubwa wa ekari 18,221.43 na eneo hilo kutolewa kwa wananchi wa vijiji vya Luduga, Mpanga, Malangali na Wangamiko. Aidha, Hifadhi ya Mpanga Kipengere kwa ujumla imemega ardhi yenye ukubwa wa ekari 52,877.602 na kutolewa kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo na hivyo kumaliza migogoro iliyokewepo kati ya hifadhi na vijiji hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Hifadhi ya Kituro na Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Kituro ngazi ya Wilaya ya Makete, ngazi ya Mkoa wa Njombe ulishapeleka mapendekezo Wizarani. Kazi iliyobakia ni kwa Wizara tu kuthibitisha ili mapendekezo hayo yaweze kufanyiwa kazi.

Je, ni lini Wizara itafanyia kazi suala hilo ili tumalize ule mgogoro kule Makete? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inashughulikia migogoro hii kupata utatuzi wa migogoro ili kuondokana na changamoto hii. Katika kushughulikia migogoro hii umakini mkubwa unahitajika ili kuhakikisha kila mtu anapata haki stahiki, namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati tunalishughulikia jambo hili ili mwisho wa siku tukilimaliza lisiwe na changamoto nyingine yoyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza je, Serikali imejipangaje kumaliza mgogoro katika Mbuga ya Kikwachi iliyopo Wilayani Ulanga ili wale wananchi wasiendelee kupata usumbufu katika kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu swali hili ni *specific* kwa eneo tofauti na swali la msingi namuomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu tukutane ili tuweze kupata majibu ya uhakika kwa eneo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba, tangazo la wageni litakapokuja hapa tutawatangaza.

Katibu.

**26 JUNI, 2024**

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wachangiaji.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naleta mchango wangu kuhusu sekta ya milki katika ukuaji wa uchumi Tanzania na nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napongeza wawasilishaji wote wawili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa mawasilisho yao katika Bajeti Kuu ya Serikali na mpango wa Serikali uliowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya milki ni sekta muhimu katika uchumi, ni sekta mama kuchochea ukuaji wa uchumi katika sekta nyingine *(multiplier effect)* hasa ikisimamiwa vizuri na kuwekewa utaratibu nzuri unaolenga kuchochea ukuaji wake. Sekta inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kupunguza umaskini na kuleta ukuaji wa uchumi endelevu mijini na vijinini. Mchango wa sekta ya milki upo katika maeneo mengi kwa kuwa inagusa kila eneo la kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, utulivu wa kiuchumi *(economic stability);* soko la mali isiyohamishika linalofanya kazi vizuri na bei thabiti hutoa uhakikisho kwamba uchumi unafanya vizuri. Mali isiyohamishika hutumika kama dhamana ya ufadhili na ni nyenzo muhimu ya utulivu wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta zingine za kiuchumi *(other sector economic growth);* sekta zote za kiuchumi ambazo ni uzalishaji wa viwandani (manufacturing), kilimo cha kibiashara *(mechanized agriculture),* usafirishaji *(transportation), tourism* (utalii), *arts and sports* (sanaa na michezo), makoso ya rejareja *(retails)* na kadhalika zinahitaji sekta ya milki inayofanya kazi vizuri ili kuweza kupata mahali na ardhi kwa ajili ya uzalishaji wake.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa mitaji ya ndani na nje *(attraction of domestic and foreign capital);* soko la milki thabiti ni kivutio kikubwa cha mitaji hasa ya nje *(foreign capital)*. Pia linaleta fursa ya uwekezaji wa mitaji kutoka soko la ndani na hivyo kuchochea uchumi zaidi. Hii pia inasaidia kukuza na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuwa wawekezaji wengi kutoka nje watatakiwa kuja na mitaji yao kutoka katika masoko ya fedha ya nje na siyo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa teknolojia na ubobezi *(technology and expertise);* sekta ya milki thabiti na yenye kufanya kazi vizuri inavyovutia wawekezaji ndivyo wanavyoleta teknolojia katika ujenzi *(construction),* vifaa vya ujenzi vinavyotumika *(building materials),* ujuzi wa ujenzi *(construction knowledge)* na kusaidia ukuaji thabiti katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi *(wealth creation);* usimamizi mzuri wa soko la nyumba na ardhi *(real estate)* kutakuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji, wajenzi na wamiliki wa nyumba na ardhi *(investors, developers and property owners)*. Soko la nyumba na ardhi linakuwa na thamani inaongezeka kila wakati, faida ya mauzo inayopatikana inaweza kuwekezwa tena kuendeleza milki au kutumika kwenye maeneo mengine ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ajira *(job creation);* uwekezaj kwenye majengo na ardhi kunatoa fursa nyingi za ajira katika ujenzi *(construction),* ubunifu wa michoro *(architecture),* uhandisi *(engineering),* usimamizi wa ujenzi *(project management),* uuzaji wa majengo na ardhi *(real estate brokerage),* usimamizi wa majengo na nyenzo *(property management)* na ukarabati

*(maintenance)*. Pamoja na ajira ambazo siyo za moja kwa moja nyingi zinazozalishwa kutokana na ukuaji mzuri, thabiti na tulivu wa soko la nyumba na ardhi.

Mheshimiwa Spika, haya ni maeneo machache kati ya mengi ambayo usimamizi mzuri wa sekta ya milki (nyumba na ardhi) inaweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unaosema, "*when spider webs unite, they can tie up a lion.*" Hii ina maanisha usimamizi mzuri wa sekta ya milki ni mtambuka ni jambo la pamoja *(collective action)* kwenye taasisi na idara zote zinazosimamia ardhi na nyumba. Kuanzia upangaji, upimaji, utoaji wa ardhi, ujenzi na usimamizi (utumiaji).

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, wakati Wabunge tunachangia hoja ni nyingi hata hivyo mara nyingi hoja za msingi hazijibiwi. Waziri anasema hoja nyingine nitajibu kwa maandishi, lakini hakuna majibu tunayoletewa. Mfano hoja ya matrekta na mikopo vijijini Mheshimiwa Bashe alijibu vizuri na vijiji wanasubiri matrekta na mikopo. Sasa hoja yangu ya kuboresha mishahara na marupurupu ya Makamu Mkuu wa Vyuo Vikuu yatafanyika lini? Vyuo Vikuu Vishiriki vya Mkoa wa Ruvuma wasaidiwe vianze kuonesha maendeleo yake hasa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya TAMISEMI ije baada ya Maji, Elimu, Ardhi na Afya kwa sababu hizo Wizara hoja zake nyingi TAMISEMI inaweza kuzijumuisha na kuona namna ya kuzi-*contain*.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Mipango na Uwekeza, Profesa Kitila Mkumbo kwa hotuba nzuri ya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka wa 2023 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kuongoza Wizara mpya ya Mipango na Uwekezaji ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais. Kuanzishwa kwa Wizara hii kulikuwa ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni mwanazuoni mahiri na nina uhakika ataitendea haki nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipopata uhuru nchi yetu ilikuwa inakabiliwa na maadui wakuu watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Nchi imepiga hatua kupambana na maradhi na ujinga ila bado tuna njia ndefu ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, nchi yetu inahitaji mipango madhubuti ya kuondoa umaskini unaowakabili wananchi wa Tanzania, kwani Mungu ametujalia rasilimali nyingi za kimkakati ambazo kama zitatumika vizuri zitasaidia sana kuondoa umaskini unaowakabili Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inasifika kwa kuwa na rasilimali nyingi yakiwemo madini ya aina nyingi, ardhi nzuri ya kilimo, mifugo, mbuga za wanyama katika kila kanda, maziwa, mito, bahari, bandari na vitu vingine vingi. Pamoja na baraka hii kubwa nchi yetu imekosa mipango madhubuti ya kuzitumia rasilimali zilizopo kutuletea maendeleo. Bado watu wetu ni maskini sana.

Mheshimiwa Spika, toka tupate uhuru maendeleo tuliyofikia ni kidogo. Kuna nchi nyingi hapa duniani zilikuwa na uchumi sawa au kidogo kuliko sisi, lakini kutokana na mipango mizuri ya maendeleo na usimamizi wa utekelezaji mipango, nchi hizo zimefikia uchumi wa juu. Ni maoni yangu kwamba Tanzania hatustahili kuwa katika kiwango hiki cha maendeleo (cha uchumi wa kati kiwango cha chini) tukilinganisha na utajiri mkubwa wa rasilimali tulizonazo ambazo nimezitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaja na mpango bora wa kuboresha uchumi na kuwaletea Watanzania maendeleo

endelevu yatakayohakikisha upatikanaji wa mahitaji ya kizazi cha sasa pasipo kuathiri upatikanaji wa hayo mahitaji kwa kizazi cha baadaye. Nashauri mpango huo ulindwe kisheria ili pasiwepo mabadiliko katika utekelezaji na usiwe unatekelezwa kwa matakwa mengine yoyote nje ya utaifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara ya Mipango na Uwekezaji ije na mpango madhubuti utakaohakikisha miundombinu ya uchukuzi na mawasiliano inajitosheleza kwenye Taifa letu. Tuwe na uhakika kwamba reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari na mtawanyiko wa mikongo ya njia za mawasiliano ni imara, kwani hivi ni vitu vya msingi kwenye kutuletea maendeleo kwani vinahitajika sana kurahisisha biashara na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ili kutupatia maendeleo ya haraka, sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zinahitaji kipaumbele cha kipekee katika mpango wa Serikali, kwani sekta hizi zinaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Kwenye sekta ya viwanda ni muhimu sana mipango madhubuti itengenezwe ili tuwe na viwanda vya aina mbalimbali (vidogo, vya kati na vikubwa) ili vitumike kikamilifu kwenye kuchakata malighafi za kilimo na madini. Mipango ikifanikisha hili ni kwamba viwanda vitasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo, ninaishauri Serikali iwekeze kimkakati katika madini mapya ya kimkakati ya *lithium,* chuma, makaa ya mawe na *helium* ili viwanda vijengwe hapa nchini badala ya kuyapeleka madini haya nje ya nchi kama malighafi kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sana kuhakikisha mipango yetu inasimamiwa na kuhakikisha huduma za elimu nchini zinaimarishwa. Ni muhimu mpango uzingatie kuwa kuna vitendea kazi vya kutosha na miundombinu mingine yote pamoja na rasilimali watu ya kutosha ili kwa pamoja vitoe elimu bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mipango yetu ya maendeleo iweke vipaumbele na kuhakikisha kuwa huduma za umeme wa uhakika, maji safi na salama na zile za afya nchini zimeimarika.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha mchango wangu kwa kushauri kwamba ni vyema mpango na dira ya Taifa letu ijumuishe mambo muhimu yenye maslahi mapana kwa Taifa letu na utekelezaji wake ulindwe kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi katika Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2024/2025 iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa inayochukua katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wa Mipango na Uwekezaji kwa kuja na mpango wa maendeleo pamoja na Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bajeti ambayo ni nzuri na mkombozi wa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa bajeti hiyo haitakuwa na thamani yoyote iwapo utekelezaji wake hautapewa umuhimu kwa maana ya watendaji ambao ndio watekelezaji wafanye kazi kwa bidii kuhakikisha wanakamilisha kazi walizopangiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara ya Fedha ina wajibu wa kuzipatia fedha walioomba Wizara za Kisekta ili waweze kukamilisha shughuli walizozipanga, iwapo Wizara hazikupatiwa fedha zote na kwa wakati ni wazi kwamba malengo hayatoweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naendelea na mchango wangu kwenye eneo la kuchangia pato la Serikali na nazungumzia eneo la mazingira. Serikali ijenge viwanda vikubwa vya kuchakata taka na kuzalisha mbolea ambayo tutatumia nchini pia tutauza nje na kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunazalisha taka nyingi ambazo zimekuwa kero kwa kuchafua mazingira na kusababisha maradhi ya mllipuko, tukumbuke kuwa kila kiumbe nchini kinazalisha taka, hivyo changamoto hiyo tuigeuze kuwa fursa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; kwanza, kupitia halmashauri zetu uwekwe mkakati maalumu wa kukusanya taka kwenye masoko yote; pili, kuwa na mkakati maalumu wa kukusanya taka majumbani; tatu, kuwa na mkakati maalumu wa kusafisha mitaro ya maji machafu; nne, kuwa na utaratibu maalumu wa kusafisha fukwe; tano, kitengo cha kukusanya taka kwenye halmashauri zetu kiimarishwe kwa kupatiwa vifaa vya kisasa na sita, wawepo wakaguzi wa kila siku kukagua usafi wa masoko. Hii itasaidia maeneo yetu kuwa safi, pia kupata malighafi ya kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu Benki ya Wananchi wa Mufindi *(MUCOBA)* kuchukuliwa fedha zake shilingi milioni 681 na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango huu wa maandishi naomba Waheshimiwa Mawaziri warejee mchango wangu kuhusu Benki ya Wananchi Mufindi *(Mufindi Community Bank-MUCOBA)*.

Mheshimiwa Spika, benki hii ni benki ya kwanza ya wananchi hapa nchini, kama nilivyoeleza katika mchango wangu. Benki hii ilipitia kipindi kigumu sana kiasi kwamba *BOT* ilitishia kuifunga kama ilivyotokea katika baadhi ya Benki za Wananchi. Benki hii ni mkombozi wa wananchi wa Mufindi hasa katika mikopo ya masharti nafuu. Benki hii imesaidia kwa miaka

mingi kuchangia uchumi wa wananchi wa Mufindi kuanzia kutoa ajira na kutoa *support* kwa wafanyabiashara wadogo hususani wafanyabiashara wa sekta ya mazao ya misitu, vikundi vya wajasiriamali vya vijana na wanawake. Ni benki ambayo ni mkombozi wa wananchi wa Mufindi na Iringa kwa sababu benki ilijitanua mpaka kufungua Tawi Iringa Mjini, Ilula na kufungua Ofisi za Mawakala katika maeneo ya Igowole mpaka Madibira ambako ni Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya. *MUCOBA* ni nembo ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni matarajio yetu wana Mufindi kuona kuwa baada ya kupitia kipindi kigumu hata kufikia Benki ya Watu wa Zanzibar - *PBZ* kuongeza mtaji, Serikali ingekuwa mlezi mwema wa kuhakikisha kuwa benki inastawi na kushamiri kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi. Kiuwekezaji benki hii imesaidia wawekezaji wengi wa ndani ya Mkoa wa Iringa kwa kuwapa mikopo na huduma mbalimbali za kifedha. Katika nyakati ambazo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuunda Wizara ya Mipango na Uwekezaji, ni matarajio yetu Wana-Mufindi kuwa uwekezaji wa taasisi *local* za wananchi unapaswa kulindwa na kulelewa ipasavyo. Huu ni mfano halisi wa *local content* katika sekta ya kibenki. Benki hii ni mfano wa nguvu ya wananchi siyo tu kushiriki bali kumiliki uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, haikuwa kazi rahisi kwa benki hii kusimama tulifanya jitihada kubwa sana na vikao visivyokuwa na hesabu mpaka kufikia hatua ya wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukubali Benki ya Watu wa Zanzibar - *PBZ* kuingiza mtaji wake. Tulikaa vikao vya kutosha kati yetu na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa, sisi tukiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mufindi Mzee Yassin Daud ambaye sasa ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Mzee Mizengo Pinda - Waziri Mkuu Mstaafu akiwa wakati huo mlezi wa CCM wa Mkoa wa Iringa alishirikiana nasi katika kuhakikisha kuwa benki hii inajikwamua kutoka hatari ya kufungwa na *BOT*.

Mheshimiwa Spika, vikao hivyo na majadiliano ya mara kwa mara na Maafisa wa *BOT* ambao walifikia hatua ya kuweka afisa

mahususi kushirikiana na benki isifilisike, vilizaa matunda kwa Benki ya Watu wa Zanzibar kuona *potential* iliyopo ndani ya *MUCOBA* na kuamua kuongeza mtaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hatua za *TRA* kuchukua fedha kiasi cha shilingi milioni 681 kwa nguvu imeturudisha nyuma sana kama benki na kama wananchi wa Mufindi na kwa ufupi, pamoja na kuwa mimi siyo mchumi, inashangaza benki ambayo inasuasua kiuchumi, haitengenezi faida, inawezaje kuwa na malimbikizo ya kodi ya shilingi milioni 681?

Mheshimiwa Spika, shida ilianza pale ambapo *TRA* ilipokadiria kodi kama vile hii ni benki kubwa za kiwango cha *NMB* au *CRDB,* hii ni benki ndogo isiyozidi mtaji wa shilingi tano, matokeo yake *PBZ* wameondoa fedha zao na sasa benki inakaribia kushindwa kufikisha ile *minimum requirement* ya *BOT,* hili jambo limewashangaza hata wenzetu wa *PBZ* kwamba wao wameweka fedha kama mtaji, sisi *(TRA)* tunatoa fedha za mtaji shilingi milioni 681.

Mheshimiwa Spika, athari za hatua hii ni kuwarejesha wananchi kwenye mikopo tunayoita kausha damu, yawezekana siyo wote wanapata mikopo *MUCOBA,* lakini hata hao waliokuwa wanapata hivi sasa hawapati, hakuna gawio kwa wanahisa, lakini zaidi ya yote linafifisha jitihada za benki kuendelea kupanua wigo wa kukua, mwisho *PBZ* imeamua kuondoa mtaji wake na matokeo yake hata kisiasa hili suala litaathiri sana Chama Cha Mapinduzi kwa sababu hii ni benki ya wananchi ambayo sehemu ya mtaji wake ulitoka kwa wananchi kupitia michango yao ya kukatwa kiasi fulani cha fedha kupitia *IMUCU* na pia halmashauri zote mbili za Mufindi na Mafinga ni wanahisa na wananchi walinunua hisa.

Mheshimiwa Spika, je, hatuoni kuwa tunatengeneza chuki kwa Serikali? Sina maana kwamba sheria zisifuatwe, hapana, naomba tuangalie kiasi hiko cha shilingi milioni 681, ni kiwango sahihi, je, tunaenda nyuma au tunaenda mbele?

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi na kwa wananchi wa Mufindi na Iringa kwa ujumla tunawarudisha nyuma kijamii, kiuchumi hata kisiasa wanakuwa na hasira na Serikali. Haiwezekani wananchi hawapati gawio, hawapati mikopo, utarajie wawe na furaha. Tutafakari suala hili kwa umakini na hekima ya Mungu ituongoze.

Mheshimiwa Spika, ushauri/ombi, ninashauri Serikali kwa maana ya Wizara, *BOT* na *TRA* kuona uhalali wa jambo hili na kulitafakari upya sio tu kwa mustakabali wa *MUCOBA,* bali sekta nzima ya benki. Nasema hivi kwa sababu sisi Mufindi tumekuwa shule kwa benki nyingine zote za wananchi *(community banks)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili lilikuwa bado katika majadiliano, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mamlaka aliyonayo, aamuru *TRA* irejeshe fedha hizo ili benki iendelee kuzungusha mpaka hapo mwafaka utakapofikia, kwangu mimi ni ubabe kwa Serikali/*TRA* kuchukua fedha katika jambo ambalo liko kwenye majadiliano.

Mheshimiwa Spika, ninaamini Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake wa Wizara, *BOT* na *TRA* mtaona kilio hiki cha Wana-Mufindi na kama kuna mapungufu yoyote ninyi kama walezi mnaweza kuona namna njema ya kulifanyia kazi suala hili kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28, Mji wa Mafinga ni sehemu ya Mradi wa Maji wa Miji 28 ambapo ndani ya Serikali ilikubalika kuwa kwa kuwa fedha za mkopo nafuu kutoka India *USD* milioni 500 hazitaweza ku-*cover* miji yote 28 iliamriwa kuwa miji minne ikiwemo Mafinga itagharamiwa kwa fedha za ndani, lakini kwa nia njema ibaki ikitambulika kuwa ni mradi wa miji 28. Mradi huu sisi Wabunge na viongozi wa chama kutoka maeneo ambayo ni wanufaika wa mradi tulialikwa kwenye *signing ceremonies* pale Ikulu mbele ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, *Jandu Plumbers* ni kampuni inayotekeleza mradi huu, hata hivyo ikiwa imebaki miezi minne

muda wa miezi 20 ukamilike mradi umefikia *only 22%,* shida kubwa ni fedha, mpaka sasa mkandarasi ametoa *certificates* nne hajalipwa, matokeo yake amewaondoa wafanyakazi *site*. Ninawaomba sana kama sehemu ya kumheshimisha Mheshimiwa Rais tutoe fedha ili mradi huu ukamilike, shida kubwa ni fedha, isije ikaonekana sisi ambao mradi unatekelezwa kwa fedha za ndani ni kama tumefanya dhambi maana miji 28 mambo yanaenda vizuri, najua hali ya fedha ilivyo kutokana na miradi mikubwa, hata hivyo ninaomba mtuangalie Mafinga kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Mafinga - Mgololo kwa Mfumo wa *EPC+F,* suala hili limeleta mkanganyiko sana ndani ya Bunge na ndani ya nchi, siyo tu kwa sababu ya mfumo wenyewe, bali kutokana na shauku ya uhitaji wa kuwa na barabara kwa ajili ya kuchochea shughuli za uzalishaji na uchumi kwa ujumla. Barabara ya Mafinga - Mgololo ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa mazao ya misitu, mazao ya chai, mazao ya chakula na shughuli nyingine za kiuchumi. Ni *catalyst* kwa uchumi wa Mufindi, Iringa na Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, nawaomba Serikali kwa namna yoyote itakayofaa, ujenzi uanze katika Barabara ya Mafinga - Mgololo na nina hakika takwimu ziko wazi hasa katika suala zima la mchango wa Mufindi katika pato la Taifa. Takwimu za *TRA* za *larger taxpayers* mtaona, hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kujengwa kwa barabara hii kutasaidia na kupanua wigo wa mchango wa Mufindi katika pato la Taifa, nawaomba sana fursa hii isipotee ili Mufindi tuendelee kuwa na mchango madhubuti katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuchangia bajeti ya Serikali na Mpango wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia katika sekta ya kilimo, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza

bajeti ya Kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na 65% ya Watanzania ni wakulima ambao wengi wanatumia kilimo cha mkono.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa jitihada zake za kununua magari ya kuchimba maji katika maeneo yenye uhaba wa maji, kwani hii itasaidia wakulima kulima kilimo chenye uhakika ambacho ni kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iongeze magari haya ya kuchimba maji ili yasambazwe katika maeneo mengi yenye uhaba wa maji nchini kwa ajili ya kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuongelea pia kuhusu upimaji wa udongo (afya ya udongo), nchi yetu ina eneo kubwa na kila eneo kuna wakulima wa mazao mbalimbali, lakini wakulima wanalima mazao ambayo hawana uhakika wa mazao yao kustawi katika maeneo hayo na hivyo hupoteza nguvu nyingi na kuvuna mavuno machache kulingana na ustawi wa mazao hayo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iongeze jitihada za upimaji wa udongo katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini ni mazao gani yanastawi wapi ili wakulima walime kilimo chenye tija na kukuza uchumi wa Taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa wema wake kwa uhai huu, lakini pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana na nzuri kwa kuiweka nchi yetu katika maendeleo ya kitaifa, yapo mambo makubwa ya kiafya, elimu, miundombinu, maji na kadhalika kwani kila sekta amegusa kwa uwezo mkubwa sana, hakika ameziweka zile *4Rs* vizuri.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri wote, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwekezaji pamoja na Naibu

Mawaziri wao pamoja na jopo zima la wasaidizi wao kwa bajeti hii nzuri na hasa pale nilipoona wanavyopambana kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimesoma na kuona jinsi gani nguzo ya rasilimali watu na hasa kwa utekelezaji wao tuangalie watumishi wa umma kwa maendeleo hasa kwa kutowahamisha hamisha bali waangaliwe na kuwaweka pale ambapo mtumishi ana uwezo napo na kuweza kushauri kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda ninashauri tuwe tunafanya tathmini kwa sehemu ambazo viwanda vinaweza kujengwa kwa maoteo ya lengo husika mfano viwanda vya mzao vijengwe sehemu ya ulimaji wa zao husika au madini na kadhalika ili viwe na tija na faida kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa uamuzi wake ambao ni bora na lengo lake la kuwezesha upatikanaji wa sukari nchini na hii ni nzuri kwani itawaondolea wenye viwanda kuhodhi bila kuathirika kwa dhamira ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua ya kutoa idhini ya kuingiza sukari tani 410,000 kupitia *NFRA* na natambua dhamira nzuri ya Serikali na pia Serikali kufanya marekebisho ya kanuni ya *NFRA* na kuiweka sukari kuwa sehemu ya usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kusema kuwa dhamira ni nzuri, lakini *NFRA* inategemewa na wakulima kununua mazao yao hivyo wasisahaulike.

Mheshimiwa Spika, niishauri pia Wizara ya Viwanda na Biashara inaposema inachochea uchumi basi waweke mahusiano mazuri na walipakodi ili kuona wanatendewa sawa na sheria zinzosimamia taratibu za biashara. *TRA* wawatembelee wafanyabiashara na kusikiliza hoja zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kipekee nipongeze juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mipango na mikakati mizuri ya kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Mheshimiwa Rais halali usiku wala mchana kwa ajili ya Watanzania, hongera sana Mheshimiwa Rais, tunakupenda, tunakujali na tutaendelea kukujali na tunasema piga kazi mama, tupo nyuma yako mpaka kieleweke na katu haturudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha, Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa kazi wanazozifanya kwa kuandaa hotuba hizi na kuwasilishwa kwetu kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naanza na suala la kodi ambapo hotuba imeeleza mabadiliko ya sheria kwa wafanyabiashara wanaokwepa kutoa risiti. Nataka niseme ni kweli kwamba baadhi ya wafanyabiashara pamoja na kwamba Serikali imeweka msisitizo kuhusu matumizi ya *EFD* wanapouza na kudai risiti pale mtu anaponunua. Hii imechukuliwa tofauti na baadhi ya wafanyabiashara kwa kuleta visingizio vya kuharibika kwa mashine au biashara mpya hawajapata, hawajapata mashine na haya yote ni kuwepa kodi. Isitoshe wafanyabiashara wamekuwa na malalamiko makubwa kuhusu utarabu uliowekwa kisheria kwamba unamuumiza sana mfanyabiashara hasa mdogo na kusema kwamba hili la sasa linaweza likachangia rushwa kwa kiwango kikubwa kwa wafuatiliaji wa makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini kabla ya matumizi ya sheria hii Serikali iamue kukutana na wafanyabiashara wote kulingana na maeneo wanayofanyia biashara zao ili kuondoa mkanganyiko wa malalamiko kwa wafanyabiashara kwamba kumekuwa na utitiri wa kodi ambao unaendelea kukwamisha mwenendo wa ukuaji wa biashara zao.

Mheshimiwa Spika, moja, kodi ya jumla wakati mzigo unapoingia nchini na pili, mfanyabishara anapouza likitokea kosa kwa mnunuzi kwa kusahau *TIN* adhabu inarudi kwa muuzaji na

kutakiwa kulipa fidia na tatu, kodi inayotozwa inaangalia kwenye mtaji zaidi wa mfanyabiashara na siyo faida kama ilivyo taratibu.

Mheshimiwa Spika, ifanyike tathmini ya jumla ya kadirio la kodi kuanzia pale mzigo unapofika na pale unapokuwa dukani na kama mfanyabiashara hakutimiza kodi yake hapo ndio Serikali iweke msisitizo wa sheria aweze kulipa fidia kama hakukamilisha kodi yake na hii iweke ulingahisho kutokana na thamani ya biashara husika ili tusiumize wafanyabiashara wadogo. Hii itawafanya wafanyabiashara kuongeza wigo mpana kukamilisha kodi yake ambapo nusu ya kodi ameshalipia mapema.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na sheria kwa kufanya ufuatiliaji madhubuti kwa wale wote wanaopita kukusanya kodi kwa wafanyabiashara kwani wengi wao wamejilimbikizia mali na majumba ya kifahari. Ufuatiliaji uanzie mwanzo anapoanza kazi hii ya ufatiliaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linahusu Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu *TANAPA* na *NCAA* kuhusu sheria inayowataka makusanyo ya kodi yabaki na kuwawezesha kutumia katika miradi ya maendeleo. Katika hotuba ya Wizara haionekani wazi mabadiliko ya sheria hiyo ambapo wataweza kukusanya na kutumia fedha kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi niunge mkono hoja na kuwataka wananchi waone na kuzingatia umuhimu wa kulipa kodi. Lipa kodi kwa maendeleo ya Taifa. Niwaambie wananchi tu kwamba bila kulipa kodi mipango ya Serikali kuhusu huduma za wananchi haiwezi kufikiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo na Mheshimiwa Angellah Kairuki ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii na mimi nasimama hapa kuunga mkono hoja na napenda kukumbusha tu wakati Waziri wa Fedha anasoma hotuba yake alitumia maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, alizungumza kwamba *a politician looks at the next election but a state person looks at the next generation*. Alizungumza hivyo kwa kusisitiza kwamba Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuwekeza na kuweka kipaumbele sana kwenye elimu siyo tu katika suala la miundombinu, lakini katika kubadilisha mfumo, mitaala na sera ya elimu, jambo ambalo matunda yake hayataonekana mapema sana, anafanya hivyo kwa sababu amekusudia siyo kuangalia tu uchaguzi ujao, amefanya hivyo kwa sababu anataka kuangalia vizazi na vizazi vijavyo vya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo tunaweza tukayaona kwanza katika miundombinu halafu nitaelezea kidogo kuhusu mikopo ya wanafunzi suala ambalo limezungumzwa sana humu na utekelezaji wa mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika, katika miundombinu ni vizuri tu nikakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba chini ya uongozi wa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Elimu ya Juu kwa mara ya kwanza kabisa katika nchi yetu sasa hivi tunaenda kujenga kampasi za Vyuo Vikuu katika Mikoa yote ambayo ilikuwa haina kampasi ya Vyuo Vikuu ukiacha Chuo Kikuu Huria. Tutamaliza Mikoa yote isipokuwa tu Mkoa wa Pwani ambao mkakati wake tunaenda kuuweka. Kwa hiyo, Mkoa kama Kigoma sasa hivi, Tabora, Kagera, Lindi, Tanga, Ruvuma na kadhalika kazi ya ujenzi inaendelea kwa sababu ya maelekezo ya Rais wetu, Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango kwa kweli wanatusaidia kulisukuma jambo hilo mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni kubwa vilevile ni lile suala la ujenzi wa vyuo vyetu vya *VETA*. Niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge hasa wenyewe kwa mchango wao kwamba Serikali imeamua na ni utekelezaji wa maelezo ya Rais wetu kwamba sasa hivi katika kila Wilaya ambayo *VETA* imejengwa lakini Wilaya hiyo ni kubwa kiasi kwamba ina Majimbo zaidi ya moja la uchaguzi, kama *VETA* imeenda kwa Mbunge mmoja, huyu Mbunge mwingine anajengewa shule ya sekondari ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari ya ufundi siyo tu mafunzo ya amali, maana yake mafunzo ya amali kuna mambo ya utalii, kuna kilimo na kadhalika, hizi ni *technical secondary school* kama tulivyokuwa tunajua Tanga *Tech,* Ifunda *Tech,* Bwiru *Tech,* Moshi *Tech* na hizi zitajengwa na zitakuwa zinatumia teknolojia ambayo ni *modern* zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mchengerwa wakati anawasilisha bajeti yake zinajengwa shule 100 mpya, shule 26 tunakusudia zianze kuchukua wanafunzi ifikapo Januari kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya elimu yetu katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kila Mheshimiwa Mbunge sasa hivi atakuwa na cha kusema kama hana *VETA,* atakuwa na sekondari ya ufundi ili aweze kwenda kuisemea Serikali yetu kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nielezee kidogo kuhusu mikopo. Kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia kuhusu mikopo ya elimu ya juu, najua kuna masuala kwamba kuna watu wameomba mikopo wanaonekana hawajapata lakini ni vizuri kwanza tujue tulitoka wapi, tuko wapi, halafu tutapata matumaini tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, wakati Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anachukua uongozi wa nchi, mikopo ya elimu ya juu ilikuwa ni shilingi bilioni 464 na nyongeza ilikuwa ikienda taratibu sana tangu tuanze mikopo ya elimu ya juu. Alipoapa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya vitu vya kwanza alivyosisitiza ni kuuliza ajue mikopo ya elimu ya juu ikoje akaagiza iongezwe, iliongezwa kwa mkupuo kutoka shilingi bilioni 464 kwenda bilioni 570 kwa mwaka wake wa kwanza ofisini. Mwaka uliofuata tumefika bilioni 654, mwaka uliofuata bilioni 731. Sasa hivi tuna bilioni 787, tunakaribia shilingi trilioni moja kwenye mikopo ya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hayo? Nasema hayo kwa sababu hata pamoja na changamoto ambazo bado zinakuwepo katika mikopo ni vizuri tujue na wanafunzi wajue kwamba nyongeza iliyofanyika kwenye mikopo ya elimu ya juu ni

kubwa kuliko kipindi kingine chochote tangu tuanze kutoa mikopo ya elimu ya juu. Zaidi ya hapo mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yalikubaliwa na Rais wetu na hivyo Hazina ilitenga hela na tumeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma *Diploma.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mara ya kwanza sasa hivi katika fani kadhaa tunatoa mikopo kwa wanafunzi ambao wanasoma *Diploma.* Kazi yetu kubwa ni kuendelea kuboresha namna ya kugawa mikopo hii kwa haki, wapate wale ambao wana mahitaji makubwa zaidi wakati ambapo tunaendelea kupambana namna ya kuongeza fedha kwa ajili ya kutoa mikopo hiyo. Hili ni vizuri tuliseme ili wakati tunapoona changamoto tusije tukasahau kwamba kwa kweli tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hivyo napenda kuwaambia wanafunzi wote wanaosoma, wanaonisikia kwamba Serikali sasa hivi iliongeza, Rais wetu alikutana na uongozi wa wanafunzi iliongeza fedha za kujikimu kwa siku kwa wanafunzi wote kwa mkupuo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho najua kengele imepigwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda wako umeishaisha Mheshimiwa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa unachukua dakika za wenzio, sekunde thelathini malizia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kuhusu utekelezaji wa mitaala, bajeti ipo muda wangu hautoshi na mkumbuke mitaala inatekelezwa kwa awamu, Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza la Tatu na Sekondari Kidato cha Kwanza Mafunzo ya Amali. Fedha zimetengwa za vitabu na walimu wote wa viwango hivyo wameishapata

mafunzo namna ya kutekeleza mitaala mipya na tunazo fedha kwa ajili ya kuendelea darasa la pili, darasa la nne la tano la sita mpaka tutakapo kamilisha mwaka 2027 tutakapoanza sasa kwenda elimu ya miaka 10 ya lazima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii, narudia tena kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanste sana; Waheshimiwa Wabunge nilete kwenu tangazo la wageni ili kutoa fursa kwa wageni wengine kuweza kuingia baada ya hawa walioingia awali kutoka. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

Ngoja, ngoja, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Nimesimama wengine bado mnaongea, sasa sijui niwataje kwa majina? Kuna wengine bado wanaongea pale Mheshimiwa Naibu Waziri anamsikiliza Mbunge kwa bidii kabisa.

Haya, tusikilizane.

Tunao Wageni wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ambaye ni Spika Mstaafu. Hawa ni viongozi wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa, wakiongozwa na Baba Askofu Razineth Kingamkono. Ahsanteni sana. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Huyu ni Ndugu Lawrence Mafuru ambaye ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mjini. Huyu ni Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni sita wa Mheshimiwa Deus Sangu na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. Hawa ni Viongozi wa Shirikisho la Bima la Taifa *(NIC)* kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma. Hawa ni Ndugu Justine Mwandu ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi, ameongozana na Ndugu Furaha Mbwambo ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Fedha na Uwekezaji, Ndugu Harbert Polepole Mkurugenzi wa Bima za Maisha, Ndugu Goodluck Nyiti Meneja wa Uandikishaji Bima, Ndugu Alex Suzuguye Meneja wa Kanda ya Kati Dodoma na Ndugu Karim Meshaki Mkurugenzi wa Masoko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 122 wa Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew ambaye ni Naibu Waziri wa Maji. Hawa ni wenyeviti, makatibu na waenezi kutoka Jimbo la Bariadi Mkoa wa Simiyu. Viongozi hawa wa chama wameongozwa na Katibu wa Chama wa Wilaya. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia, wapo wazee maarufu 23 ambao kiongozi wao ni baba mzazi wa Mheshimiwa Kundo ambaye anaitwa Mathayo Mloza. Karibuni sana Bungeni. Mzazi wa Mheshimiwa Naibu Waziri ni yupi, baba yake? Sawa, karibu sana baba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni watatu wa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini. Huyu ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Ilkisongo Monduli pia ni Mwandishi wa Vitabu vya Hesabu na Mwanafunzi wa *Cyber Security* Chuo Kikuu cha Dodoma, kutoka Longido Mkoani Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ambaye ni Mwalimu kutoka Muleba Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mjasiriamali wa Zao la Mwani kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao ni wapigakura wake kutoka Arumeru Magharibi Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ambaye ni mdogo wake kutoka Masasi Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi ambao ni wapigakura wake kutoka Kibosho Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila ambao ni watoto wake na waandishi wa KEIFO *FM* na Busokelo *TV* kutoka Kyela Mkoa wa Mbeya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, watoto wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ni Charlotte na Precious. Ndio wako wapi watoto wake? Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao Wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, ambao ni Wapigakura wake kutoka Nyamagana Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mhandisi Isack Aloyce Kamwelwe ambao ni watumishi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* kutoka Mkoa wa Katavi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni wengine 13 wa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ambao ni wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Mtwara Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ambao ni wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kata ya Msigani Jimbo la Kibamba, Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa wa Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, ambao ni Masheikh kutoka Arumeru Mashariki Mkoa wa Arusha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ambao ni Viongozi wa Kanisa la *Kingdom of Heaven on Earth Mission* kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni 61 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wachungaji, wainjilisti na waimbaji wa Kwaya ya Uinjilisti Dongobesh Kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara. Ahsante. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Bujiku Kaswahili kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Ndugu Yohana Joseph Ihombwe ambaye ni Mhasibu wa Hospitali ya Bugando kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wanafunzi 48 na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Dar-ul-Muslimeen ya Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao; lakini nimepata ujumbe hapa, sina uhakika kama wageni wameshaingia hapa ndani ama bado. Yupo John Ndejembi, mtoto wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Deo Ndejembi, huyo ni mwanaye anaitwa John Ndejembi. Pia yupo mdogo wake anaitwa Bonita Ndejembi. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge ambaye anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, leo tarehe 26 Juni, 2024 kutakuwa na hafla fupi ya uzinduzi wa vitabu vya Bunge itakayofanyika katika

Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 07.00 Mchana. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria hafla hiyo. Baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Seleman Jafo atafuatiwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye kwa mara nyingine ametuwezesha kushiriki kwa pamoja katika Bunge hili, lakini sasa hivi tukiwa katika hatua za mwisho za kuhitimisha bajeti yetu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Naomba niwashukuru na niwapongeze Mawaziri wote wawili ndugu yangu Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Profesa Mkumbo na Manaibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mjadala hapa kubwa zaidi katika bajeti ya mwaka huu kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ni hasa biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, kwamba mwaka 2022 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais tulikuja na mwongozo na kanuni za biashara ya kaboni kwa sababu eneo hili lilikuwa halijatumika vizuri. Kipindi kile hali yetu haikuwa nzuri katika suala la usimamizi katika eneo hili. Leo hii naomba nikuhakikishie kwamba, Bunge lako hili na Serikali yako Tukufu, tumeshafikisha usajili wa miradi takribani 50 kwa mara ya kwanza ambapo hivi karibuni tumeshuhudia Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambao hivi karibuni walipata bilioni 14 kutokana na mapato yatokanayo na biashara ya kaboni. Hii inatuonesha namna usimamizi katika eneo hili utakavyoweza kuleta manufaa makubwa sana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imejipanga na tunakwenda vizuri. Mfano mzuri ni huu uliotokea hivi juzi kama

nilivyosema, Halmashauri ya Tanganyika ambao makusanyo yao yalikuwa ni wastani wa shilingi bilioni mbili hadi bilioni tatu, leo hii kwa mara ya kwanza wamepata bilioni 14 ndani ya vijiji vyake. Hii ni faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama nilivyosema, tayari tumesajili mradi takribani 50. Kati ya miradi hiyo 26 ni sekta ya misitu na 14 ni sekta ya *energy*. Kwa hiyo hata katika suala la mpango wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan la kwenda katika nishati safi ya kupikia kupitia biashara ya kaboni, eneo hilo nalo tumeweza kulifanyia kazi kubwa zaidi. Hivi sasa tunashukuru kwamba kuna baadhi ya kampuni zimeanza hatua kubwa sana hasa katika suala la kupata majiko banifu na majiko mengine ambayo yatakuwa na gharama nafuu kwa lengo la wananchi kuingia katika biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba ninawashukuru Mawaziri hawa wawili hasa kwa kuweka mipango mizuri ya jinsi nchi yetu inavyokwenda. Kupitia ofisi yetu kwa ushahidi wa kutosha kabisa katika hiki kipindi cha karibuni, tumeona; na nimshukuru sana Dkt. Nchemba na hasa katika mifumo hii tunayoweka na Waziri wetu wa Uwekezaji. Leo hii kupitia Taasisi yetu ya *NEMC* takribani miradi elfu tisa na sitini na moja imesajiliwa kupitia *NEMC*. Hiyo maana yake ni uwekezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kama nilivyosema awali, kwamba kwa sera nzuri za Dkt. Samia Suluhu Hassan leo hii tunaona kupitia ofisi zetu kwamba tumeweza kusajili baadhi ya miradi kupitia kituo chetu cha *NEMC*. Leo hii takribani miradi 9,061 imesajiliwa. Hii ni *trend* ya miaka mitatu, unaona jinsi gani sasa sera nzuri zinavyotusaidia hasa katika ujenzi wa uchumi wetu. Miradi hiyo ukiikokotoa kwa ujumla wake uwekezaji huo ni zaidi ya trilioni 37. Hii maana yake ni ile miradi iliyopita katikia ofisi yetu kupitia Taasisi yetu ya *NEMC* tu.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba Watanzania tusijidharau, tunafanya vizuri katika mchakato mzuri wa uwekezaji wetu wa uchumi katika nchi yetu. Katika hili lazima tumpe kongole Dkt. Samia Suluhu Hassan. Anayoyafanya leo hii ndiyo yameweka misingi mizuri. Kama nilivyosema, kwamba uwekezaji huu ni zaidi ya trilioni 37.55, ambapo hii ni kwa *trend* zilizopitia kwenye uwekezaji katika kituo chetu cha *NEMC* ambao ni kwa ajili ya kupata vyeti vya tathmini ya athari ya kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe ndugu zangu, kama nilivyosema, kwamba tusijidharau Watanzania leo hii tunafanya vizuri. Hata kama kuna changmoto za hapa na pale lakini tunafanya vizuri. Kubwa zaidi tushikamane na hasa katika kushughulikia masuala ya mazingira, kwa sababu nchi yetu inapoteza Dola za Kimarekani takriban milioni 500 kwa mwaka kwa ajili ya kushughulikia miradi ya *adaptation* na *mitigation* kutokana na kushughulikia athari za mabadiliko ya tabianchi. Hili jambo ni kubwa, kwa hiyo Watanzania wote lazima tuweke kipaumbele cha jinsi ya kushirikiana kwa pamoja katika kuweka ajenda ya utunzaji wa mazingira na hasa suala zima la kutekeleza miradi yote, kama Serikali ilivyoamua sasa hivi kutekeleza miradi yake ya kushughulikia masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, tuishukuru sana Serikali yetu leo hii tunaona katika sekta ya maji kazi kubwa imefanyika ambapo takriban miradi ya maji 222 imesajiliwa na katika sekta ya ujenzi takribani miradi 1,894. Yote hii inajenga uchumi katika upande wa nchi yetu. Kikubwa zaidi, hasa katika sekta ya nishati, leo hii kuna miradi 1,340 ambayo sisi upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais tunasema kwamba eneo hili tunaweka tija katika suala la upatikanaji wa nishati, ambapo kwa namna moja au nyingine ajenda ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaenda kufikiwa. Kwa hiyo, kubwa zaidi niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuunga mkono bajeti hii ya Mwaka wa Fedha ya 2024/2025 kwa sababu kwa kiwango kikubwa imeakisi uhalisia, na hasa katika upande wetu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kabla sijagongewa kengele, kwa sababu najua kwamba dakika zangu ni saba, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Innocent Bashungwa ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu chini ya uongozi wake tumeendelea kuona namna ambavyo mazingira ya biashara na uwekezaji katika Taifa letu yameendelea kuimarika chini ya uongozi wake mahiri.

Mheshimiwa Spika, pia nikupongeze nawe kwa namna ambavyo unaendelea kuliongoza Bunge letu na kwa namna ambavyo unaendelea kutuwakilisha kimataifa.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza pia viongozi wengine wakuu. Mheshimiwa Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wanaendelea kutusimamia na kutupatia miongozo mbalimbali na hatimaye tunaweza kupata tija na ufanisi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizo niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri Wawili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa namna ambavyo wanaendelea kusimamia na kuongoza katika masuala ya sera na utekelezaji katika sekta zao na kwa kuleta Mpango mzuri wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2024/2025 pamoja na bajeti yetu hii kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha ujao 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, utaweza kuona namna ambavyo bajeti hii imeendelea kuakisi umuhimu wa kuendelea kukuza uchumi wetu na pia umuhimu wa mchango wa bajeti hii kupitia mkazo mbalimbali wa kisera na mazingira kwa upande wa kukuza ajira.

Vile vile, unaona namna ambavyo imeweka mkazo pia katika suala la uwekezaji wa ndani na kuendelea kuongeza au kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi. Kubwa zaidi, nikiwa ninasimamia sekta ya utalii tushukuru kuona kwamba, katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa katika sekta chache zilizowekewa kipaumbele suala la sekta ya utalii nalo limeingizwa na tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia katika bajeti hii unaona namna ambavyo imelenga kuongeza zaidi ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za biashara na uwekezaji. Imeendelea pia kuweka mkazo wa matumizi ya Shilingi za Kitanzania katika malipo mbalimbali. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi Mipango kwamba, kama Wizara ya Maliasili na Utalii tayari tumeshaanza marekebisho ya kanuni zetu ili kuhakikisha kwamba tunaakisi tozo zote na gharama zinazotozwa katika sekta zetu basi zinatozwa kwa Shilingi za Kitanzania. Kubwa zaidi tupongeze pia kwa namna ambavyo bajeti ijayo imeelekeza katika kukamilisha miradi ya maendeleo ya kimkakati, na tunaamini itaweza kumalizika ndani ya muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, nipende pia kujielekeza katika mafanikio ambayo tumeyaona kupitia uongozi imara wa Taifa letu na Wizara, na pia kupitia kinara wetu maalum Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa kinara namba moja katika suala la kuhamasisha na kutunza utalii, kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunaendelea kuwa nyuma yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika miaka miwili tangu amekuwa madarakani kwa upande wa kuvutia watalii kutoka nje ya nchi zaidi ya asilimia 96 wameongezeka; na ukiangalia mpaka Desemba, 2023 tuliweza kupata watalii wa nje takribani milioni 1.8. Kwa upande wa watalii wa ndani kiwango kiliongezeka hadi kufikia asilimia 152 na tuliweza kupata watalii milioni 1.9 hadi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeweza kutambulika kimataifa. Kupitia Takwimu za Shirika la Utalii Duniani kwa mwaka 2023

tuliweza kushika nafasi ya 12 duniani kwa ongezeko la idadi ya watalii wa kimataifa kabla ya janga la UVIKO. Ukiangalia kwa miezi hii mitatu ya Januari mpaka Machi mwaka huu wa 2024 tumeweza kuweka rekodi kubwa ya kimataifa na kidunia. Tumeweza kushika nafasi za tano za juu duniani kwa nchi ambayo imeweza kuvutia watalii zaidi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pongezi nyingi zimfikie Mheshimiwa Rais, lakini na Watanzania wote kwa namna ambavyo pia wameendelea kushiriki kukuza utalii kwa kuhakikisha kunakuwa na uwepo wa amani.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukiangalia kwa takwimu za Januari mpaka Machi, katika mapato yanayotokana na shughuli za utalii, duniani pia tumeweza kushika nafasi ya nne na nafasi ya kwanza Afrika. Lile suala zima la kuvutia watalii katika nafasi ya tano tumekuwa pia nafasi ya kwanza Afrika, pongezi sana kwa Watanzania wote, tuendelee kuwa wakarimu zaidi ili tuweze kuvutia watalii wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa takwimu za Benki ya Dunia za mwezi Mei ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** ... tumeweza kupata dola bilioni 5.75, niwapongeze tena kwa mara nyingine Watanzania na ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema aliyetuwezesha kufika katika hatua hii tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nichukue fursa hii kukupongeza sana wewe, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha Bunge letu hili na kuishauri Serikali kwa namna ambavyo tumepokea kama Serikali ushauri, maoni na mazingatio ambayo sisi Ofisi ya Rais tutakwenda kufanya kazi ambavyo Wabunge wametushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri, Bunge hili limesheheni Wabunge wanaofanya kazi kubwa sana, lazima sisi kama Serikali tuwapongeze kwa kazi kubwa sana ambayo Waheshimiwa Wabunge wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mmoja wetu hapa ni shahidi, kila Mbunge aliyesimama kwenye Bunge hili amezungumza yale ambayo yanawahusu wananchi wake katika maeneo yao na wananchi watakuwa ni mashahidi kwa namna ambavyo Wabunge wamegusa hoja zao na ni matamanio ya wananchi kusikia Wabunge wao wakizungumza mambo ambayo yanawahusu wao katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza sana na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na kwamba tunaunga mkono hoja ambazo zimetolewa na Wabunge walio wengi katika maeneo ambayo wamezungumza. Ninaomba nikiri kwamba huu sasa ni mwaka wa tatu na nusu wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunakiri kabisa kwamba kazi kubwa sana imefanyika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge hapa ni shahidi wa kazi kubwa ambayo imefanywa katika sekta ambayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasimamia; sekta ya afya, sekta ya elimu na sekta ya miundombinu na yapo maeneo kutokana na mafuriko yaliyotokea tunakiri kabisa kwamba miundombinu mingi imeharibika, lakini si kwamba Serikali haikufanya kazi. Hii ndiyo sababu hata watendaji wetu wa *TARURA* wanapoingia hapa Bungeni wanapongezwa kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kusimamia sekta ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge hapa, kila kiongozi katika Serikali za Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji katika maeneo yetu, kila mmoja ana sababu ya kusema yale ambayo Serikali imefanya katika kipindi hiki, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi ndani ya Ofis ya Rais, TAMISEMI tunatambua kazi kubwa iliyofanywa, ujenzi wa zahanati, ujenzi wa vituo vya afya, ujenzi wa hospitali, uboreshaji wa miundombinu kwenye sekta ya elimu na mambo mengi kadha wa kadha katika kila jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika hatuna sababu hata kidogo ndani ya Bunge hili, kwa uwakilishi mzuri ambao Waheshimiwa Wabunge wameufanya kwa wananchi, kila Mbunge ana kila sababu ya kurejea hapa mwaka 2025 kwa sababu kazi kubwa imefanyika na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutasisitiza sana kwa watendaji walio chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameridhia utoaji wa mikopo ya 10%, mikopo hii lazima wananchi watambue kwamba ni Wabunge hawa ambao wao wamekuwa wakiishauri Serikali kuhusu utolewaji wa mikopo hii. Mikopo hii inapokwenda kwa wananchi wetu kila jimbo, kila halmashauri, kila wilaya na kila mkoa, ni Wabunge hawa hawa ambao ndiyo wamewakumbuka wananchi na kusisitiza na kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya utolewaji wa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tumesimama, ninaomba tumpongeze na kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Rais wetu ameridhia utoaji wa mikopo, Rais wetu ameshauri namna bora ambayo yeye anatamani kuona kila Mtanzania katika kila jimbo akipatiwa mikopo ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, maandalizi ya kanuni za utolewaji wa mikopo yatakuwa yamekamilika, lakini pia ifikapo tarehe 10 Julai, wataalamu wa TAMISEMI watafika katika kila jimbo katika kutoa mafunzo na elimu ya utolewaji wa mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuwa mikopo hii iende na ikamfikie kila Mtanzania katika kila jimbo, halmashauri na Mkoa wa Taifa letu hili. Mheshimiwa Rais ametamani na anatarajia kwenda kunyanyua uchumi wa kila Mtanzania, uchumi wa wanawake katika kila eneo la nchi hii, uchumi wa vijana katika kila eneo la nchi yetu hii, lakini pia uchumi wa Watanzania wenye mahitaji maalumu, wenye ulemavu kwa asilimia mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge lako Tukufu, niwataarifu Watanzania kwamba fedha tunazo za kutosha za utolewaji wa mikopo katika eneo hili. Tuna bakaa zaidi ya shilingi bilioni 307 lakini katika makusanyo ya mwaka huu, matarajio yetu ni kwenda kutoa mikopo zaidi ya shilingi bilioni 101.5 na fedha hizi tunazo. Matarajio yetu baada ya mafunzo, michakato ya utolewaji wa mikopo kwa halmashauri kumi ambazo zimetengwa kwa utaratibu wa kupitia benki, halmashauri hizi ni Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Dodoma, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Kigoma Ujiji, Halmshauri ya Mbulu, Newala, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima, Nkasi pamoja na kule Bumbuli na Siha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri 174 na zenyewe zitakwenda kupata mikopo kwa utaratibu ulioboreshwa zaidi. Dhamira ya Mheshimiwa Rais fedha hizi ziende kuwafikiwa Watanzania katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie hili lingine la kuhusu vituo vya afya; Mheshimiwa Rais alituagiza kila jimbo la uchaguzi kupeleka vituo vya afya. Maana yake Mheshimiwa Rais alielekeza majimbo ya uchaguzi 214, kila Mheshimiwa Mbunge apelekewe kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge lako Tukufu, maelekezo haya ni amri ya Mheshimiwa Rais mwenyewe ambayo ametuelekeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba vituo hivi vinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaanza sasa wakati wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunaendelea na mijadala.

Tunategemea kuanza ujenzi wa vituo vya afya na tayari nilitaarifu Bunge lako Tukufu, tunazo zaidi ya shilingi bilioni 400 ambazo zitakwenda kujenga vituo vya afya ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, zitakwenda kujenga zahanati, zitakwenda hospitali za halmashauri zaidi ya 21 kujenga na kukarabati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwa nafuu ya muda ninaunga mkono hoja na ninawashukuru sana Watanzania, waendelee kuwa na imani na Serikali inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambapo tunaona kuna hitilafu ya makusanyo ya ushuru wa mazao, tumekwishatoa miongozo na mimi mwenyewe na wasaidizi wangu tutafika huko kwenye halmashauri ambazo zina changamoto ya makusanyo ya ushuru wa mazao. Maelekezo yangu, Watanzania wasinyanyaswe kwenye maeneo hayo na kiongozi yeyote ambaye hatasikiliza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI hatutasita kuchukua hatua kwa kiongozi yeyote ambaye anawanyanyasa Watanzania katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde. Mheshimiwa Ummy Mwalimu ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa hoja mbili ambazo zimewasilishwa na Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji pamoja na Mipango. Nianze kwa kuwapongeza sana watoa hoja kwa wasilisho zuri, pia niwapongeze Waheshimiwa Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu, hoja nyingi zimechangiwa kuelekea kwenye Wizara ya Ujenzi na kwa sababu ni dakika saba, ninaomba niahidi kwamba Waheshimiwa Wabunge hoja zenu zote tutawasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitatumia dakika saba hizi kuzungumzia baadhi ya changamoto ambazo mojawapo ni changamoto ya madeni kwa makandarasi na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atakapokuwa anahitimisha, ninaamini suala la madeni kwa makandarasi ataweza kuliezea vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto ya madeni, Serikali inaendelea kuweka jitihada kubwa ya kuweka fursa kwa wakandarasi wetu hususani wakandarasi wazawa. Ukiangalia takwimu kwa miaka 11, kuanzia mwaka 2012 hadi 2023, kilometa ambazo zimejengwa na wakandarasi wazawa ni jumla ya kilometa 102 kwa miaka 11, lakini bajeti ambayo tunaenda kutekeleza kuanzia mwezi ujao Julai, Wizara na kwa maelekezo ya mpendwa wetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kuangalia takwimu kwa kazi ambazo zinaenda kwenye sekta ya ujenzi, 96% wanapata wakandarasi wazawa, lakini wanachukua 40% ya keki ya fedha ambazo zinaenda kwenye sekta ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi hazikumpendeza Mheshimiwa Rais, akaelekeza Wizara ya Ujenzi tuje na mkakati. Mkakati tumeuandaa, *local content strategy* tumeikamilisha na kwa mwaka wa fedha 2024/2025 tumetenga kilometa 120 mahususi kwa ajili ya wakandarasi wazawa. Katika hizo, zipo kilometa 20 ni mahususi kwa ajili ya wakandarasi wazawa

wanawake na tutawatengea vipande vidogo vidogo ili waweze kukidhi matakwa ya kujenga kilometa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake, kwa sababu tunaona kwenye miaka 11 kilometa 102 tu ndiyo ziliweza kujengwa na wakandarasi wazawa, lakini kwenye mwaka huu wa fedha ambao tunaenda kutekeleza, kilometa 120 ndani ya mwaka mmoja zimetengwa mahususi kwa ajili ya wakandarasi wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hizi nilizozitaja kilometa 120, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na hapa kwenye Bunge mwaka jana Bajeti Kuu kama hii kulikuwa kuna hoja ya Waheshimiwa Wabunge kwamba thamani ya miradi kwa wakandarasi wazawa ni shilingi bilioni 10 peke yake. Ninamshukuru Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, amesharekebisha kanuni, sasa hivi thamani ya miradi kwa wakandarasi wazawa ni shilingi bilioni 50, imepanda kutoka shilingi bilioni 10 kwenda kwenye shilingi bilioni 50. Baada tu ya bajeti hii tutakaa mimi na kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na *PPRA* ili tuweze kujipanga kuhakikisha kanuni hii inaanza kutekelezwa ipasavyo kwenye mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunaendelea na mazungumzo na wafadhili wa maendeleo *African Development Bank*. *World Bank* tumeshakaa nao, tunataka miradi mikubwa ambayo tunatumia fedha zao, lakini ni fedha zetu kwa sababu ni mikopo na mikopo hii inalipwa na sisi wenyewe Watanzania. Tumewaomba *World Bank*, *African Development Bank* pamoja na wafadhili wengine wa maendeleo, barabara na madaraja ambayo tunayajenga kuwe na kipengele cha ku-*subcontract* kwa ajili ya wakandarasi wazawa ili kuendelea kutengeneza fursa na mkakati huu utasaidia hata kuokoa fedha za kigeni tunapokopa fedha kwa ajili ya kujenga barabara na madaraja, basi kwa kiasi kikubwa fedha hizo zibaki ili ziweze kusaidia kujenga uchumi wa nchi yetu, kwa hiyo, hili tunaenda kulisimamia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kusimamia suala la fedha za Mfuko wa Barabara 100% kuendelea kutekelezwa na wakandarasi wazawa. Sambamba na hilo, kwenye masharti ya *tender* tumefanya marekebisho, miradi yote ya *TANROADS* kuanzia mwezi Julai kwenye upande wa manunuzi tumefanya maboresho kwenye masharti ya zabuni yaliyokuwa yanawakwamisha wakandarasi wazawa bila sababu za msingi. Sasa hivi kuanzia Julai nimeelekeza Wizara ya Ujenzi na taasisi yetu ya *TANROADS*, tutapunguza kiwango cha mapato ghafi *(average turnover)* ili kuweza kuwapa unafuu wakandarasi wazawa. Tutaruhusu kutumiwa kwa *tender* au *bid-securing declaration* badala ya *tender* ama *bid-security*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaruhusu kutumia *performance bonds* au *performance securing declaration* badala ya *performance bank guarantee*. Vilevile kwenye upande wa wakandarasi wote wazawa, mimi na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tulikaa nao mwezi Novemba na tukakubaliana kwamba mkakati huu kwa bajeti hii ambayo tunakuja kuandaa ya kuanza mwezi Julai, tutaanza kutekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu kuna michango kwamba pamoja na fursa hizi za kuendelea kuchelewa kulipa wakandarasi wazawa, pia kunawakwamisha kwa sababu wanapata kazi, lakini malipo yanachelewa.

Mheshimiwa Spika, mimi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumekaa na benki zetu nchini na kuangalia namna ambavyo Serikali itashirikiana na benki hizi kupunguza *risk portfolio* ya mikopo ambayo inaenda kwa wakandarasi wazawa. Jambo hili tutalisimamia, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yuko hapa, tutakaa na benki ili tuweze kukubaliana namna ambavyo wakandarasi wanaweza wakaanza kazi, wakapata *advance payment,* lakini pale Serikali ambapo inachelewa kuwalipa, basi benki zetu ziweze kuwarahisishia malipo kwa kutumia *security* ya mikataba ambayo tunaingia nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Deo Ndejembi ajiandae.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi na mimi nichukue fursa hii kwanza kabisa kuwapongeza sana watoa hoja kwa hoja zao mbili ambazo kwa kiwango kikubwa zimegusa maisha ya Watanzania na hasa kwenye sekta ya madini. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali ambayo wameitoa ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo ambayo yamesemwa sana ni kuhusu madini mkakati na kila Mbunge ameonesha ya kwamba lazima Serikali ichukue hatua kuyalinda madini haya, lakini vilevile na nchi yetu iweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, tunayo maelezo mahususi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza mkakati wa namna ya kushughulika na madini mkakati. Katika eneo hili, katika mkakati wetu, moja ya eneo kubwa ambalo tumelipa kipaumbele ni uongezaji wa thamani wa madini mkakati hapa nchini ili kuongeza ajira kwa Watanzania na vilevile kuongeza mapato kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wetu huu, moja ya jambo ambalo pia nilisema hapa Bungeni wakati wa bajeti yangu ni kwamba tumedhamiria, hivi sasa hatutatoa tena leseni kubwa ya uchimbaji mpaka yule mwombaji atakapotudhihirishia kwa ushahidi kwamba atafanya *investment* kubwa katika kuongeza thamani madini mkakati ili nchi yetu iweze kunufaika na madini haya. Huo ndiyo mkakati wetu kuhakikisha kwamba nchi yetu inanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mahitaji ya madini mkakati duniani ni tani milioni kumi, inategemewa ifikapo mwaka 2050 mahitaji haya yatafika mpaka tani milioni 150, kama nchi tumejipanga kuhakikisha kwamba tunanufaika na rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ambao tunao hivi sasa katika eneo letu la Buzwagi ambalo lilikuwa ni Mgodi wa Buzwagi ambao unafungwa hivi sasa, pale tumelitenga kuwa ni *Special Economic Zone* ambapo tuna ekari 1331 na tumeanza kutoa leseni kwa viwanda vya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, tunayo Kampuni ya *Tembo Nickel Refining Company Limited* ambao wao wanafanya *investment* pale ya dola milioni 500 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kusafisha madini na leseni imekwisha kutoka, muda wowote wataanza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limesemwa sana hapa ni eneo la utafiti wa kina, ni kweli nchi yetu ya Tanzania eneo ambalo linafanyiwa utafiti wa kina katika utafutaji wa madini ni 16% tu na tumebaki na eneo kubwa ambalo halijafanyiwa kazi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, katika bajeti yetu ya Wizara ya Madini tumeongezewa fedha mpaka kufikia shilingi bilioni 231 na moja kati ya mkakati wetu katika eneo hili ni kuhakikisha kwamba tunaongeza eneo la utafiti wa kina zaidi ili nchi yetu iweze kunufaika na pia tuwaongoze vizuri wachimbaji wadogo ambao wanachimba kwa kubahatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika fedha hizi pia tutanunua helikopta ambayo tutaifunga vifaa maalumu kwa ajili ya kufanya utafiti nchi nzima ili tuweze kubaini eneo kubwa zaidi lenye madini na kuwaongoza vizuri Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi ambao ni wa Serikali ya Hispania ambao tunategemea katika mradi huu zaidi ya eneo la *square kilometre* 165,724 litafanyiwa utafiti wa kina na hivyo kuongeza eneo kubwa zaidi ambalo tutakuwa tumelifanyia utafiti wa kina na kufikia 18%. Hivyo, ukijumlisha 18% na 16% mpaka mwakani tutakuwa tumeshafikia eneo la zaidi ya 34% ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, haya yatakuwa ni maeneo mazuri ya kuongoza vizuri wachimbaji wadogo, ili mwisho wa siku wasiendelee kuchimba kwa kubahatisha na mradi huo

tunategemea kuuanza Mwezi wa Saba mapema kabisa katika mwaka wa fedha unaokuja. La mwisho ni, imezungumzwa hoja ya kuwawezesha Watanzania, kwa ajili ya kununua madini, hasa ya dhahabu kwa sababu, Watanzania wengi mitaji yao mingi inatoka nje ya nchi na hivyo, kusababisha madini mengi kuuzwa nje ya nchi kwa sababu wanao watu waliowapatia fedha awali.

Mheshimiwa Spika, katika kuisaidia Benki yetu Kuu kupata madini ya dhahabu tumekaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha tumekubaliana. Pale Wizara ya Fedha wana kitu wanakiita *Export Credit Guarantee Scheme* ambapo hivi sasa tutawawezesha wachimbaji wetu wadogo na wafanyabiashara wa madini waweze kupatiwa mikopo, ili waifanye biashara hii ndani ya nchi tuweze kutunza shilingi yetu na vilevile tupate fedha ambayo itatusaidia kuendesha shughuli mbalimbali na hasa wachimbaji wadogo ambao wanamchango mkubwa sana katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ambalo limezungumzwa hapa ni namna ya kuiboresha Tume yetu ya Madini kuendelea kukusanya maduhuli ya kutosha, ili yatoe mchango mkubwa katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ummy Mwalimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ndejembi. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini na mimi nakupongeza kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya katika kuliongoza vyema Bunge letu na unaliheshimisha sana. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa kuleta hoja nzuri. Kipekee, sisi Sekta ya Afya Bajeti ya 2024/2025 imebeba dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo tunajivunia katika bajeti hii ni Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika kila siku kuhusu Sera ya Matibabu Bila Malipo kwa Akinamama Wajawazito na Watoto Wenye Umri Chini ya Miaka Mitano. Bajeti hii kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, Serikali imekuja na chanzo mahususi cha kugharamia huduma za afya, kwa ajili ya akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Huyu ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatafsiri kwa vitendo Sera ya Afya ya Mwaka 2007, kwa mara ya kwanza kuna chanzo mahususi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakupongeza sana wewe na Bunge lako pia, kwa kupitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Bunge la 12 linakwenda kukumbukwa na Watanzania kwa kupitisha Mfuko wa Kuhudumia Bima ya Afya kwa Wasio na Uwezo na katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuna chanzo mahususi, hatutafika asilimia 100, lakini tunapo pakuanzia. Historia itakukumbuka Mheshimiwa Spika, Watanzania watakukumbuka, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia ataendelea kukumbukwa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zipo nyingi za Waheshimiwa Wabunge ikiwemo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Bajeti. Naomba nijikite katika mambo makubwa matatu; kwanza, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri wenu. Jambo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bajeti, suala la Serikali kuiwezesha *MSD,* kuipatia mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nalo tumeliona katika bajeti hii kwamba, Serikali imetoa mtaji kwa *MSD,* shilingi bilioni 100, ambapo utaiwezesha *MSD* kutekeleza majukumu yake. Nimepata heshima ya kuwa Waziri wa Afya, huu ni mwaka wangu wa nane, hakuna siku Serikali ilitoa mtaji mkubwa kwa *MSD*, tulichopata ilikuwa ni shilingi bilioni 16. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, ametoa kwa mkupuo shilingi bilioni 100 na kuzipeleka *MSD,* ili kuweza kuimarisha utendaji kazi wa *MSD*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge tunaona mabadiliko mazuri kwa upande wa *MSD*. Tukiangalia mapato ya *MSD* sasa hivi, 2021/2022

kwa mwaka ilikuwa ni shilingi bilioni 336, Mwaka 2023/2024 yamepanda mpaka shilingi bilioni 530, maana yake ni kazi nzuri inafanyika ndani ya *MSD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni, badala ya *MSD* kusambaza dawa mara nne kwa mwaka kwa sababu, ya kuwezeshwa na Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, dawa zinasambazwa mara sita kwa mwaka. Kwa hiyo, kama dawa hakuna ni changamoto yetu sisi watendaji katika ngazi ya hospitali na vituo vya kutoa huduma za afya. Natumia Bunge lako Tukufu kuwataka Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuandaa makisio sahihi ya mahitaji ya dawa, kwa ajili ya maeneo yao kwa sababu, dawa sasa zinakwenda kila baada ya miezi miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ni kwamba, tumeanza kama *MSD* kuongeza kununua dawa zinazozalishwa ndani ya nchi yetu. Mwaka 2021/2022 tulitumia shilingi bilioni 14 kununua dawa zinazotengenzwa ndani, tumeongeza mpaka shilingi bilioni 39.77 kwa hiyo, unaiona dhamira ya dhati ya Serikali kuwaunga mkono wawekezaji wa ndani wanaozalisha dawa na vifaa tiba, ili tuweze pia, kuongeza ajira na kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo Kamati ya Bajeti imelisema pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala la uhaba au changamoto ya watumishi wa afya katika vituo vya kutoa huduma ya afya vya Serikali. Tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kweli tunayo hii changamoto, nilikuwa naangalia mkeka wangu, tumefanya uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Ndejembi, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Mheshimiwa Hamad Chande ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika

siku hii ya leo tukiwa wazima na wenye afya. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii na ninasema tu kwamba, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu hapa. Vilevile naomba nitumie nafasi hii kupongeza Wizara hizi mbili, Wizara ya Fedha na Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na wasilisho zuri ambalo lipo mbele yetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo la kikokotoo, ambalo limejadiliwa humu ndani na Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini limekuwa pia, likijadiliwa na wabunge humu ndani katika vikao mbalimbali vya Bunge. Bajeti hii ambayo tunaenda kuipitisha ni bajeti ambayo inaonesha ni namna gani Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaguswa na maisha ya wafanyakazi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu aingie madarakani Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeona mwaka wake wa kwanza tu katika uongozi wake alipandisha madaraja yaliyokuwa yamekwama miaka mingi. Kuna Watumishi wa Umma waliokuwa hawajapandishwa madaraja kwa zaidi ya miaka tisa, aliwapandisha zaidi ya watumishi 222,000 katika mwaka wake wa kwanza wa utumishi. Mheshimiwa Rais, vilevile aliguswa sana na madeni ya *arrears* kwa Watumishi wa Umma na alitoa fedha kwa ajili ya kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili ambalo nataka nilizungumzie, la kikokotoo, nalo linaonesha ni namna gani Mheshimiwa Rais wetu anawajali wafanyakazi wa Taifa lake. Julai, 2022 kuna mabadiliko ya kikokotoo yalifanyika ambapo wale ambao ni Watumishi wa Umma walilipwa kwa mkupuo wa asilimia 50 na kushuka kwenda asilimia 33 na wale waliyokuwa asilimia 25 walipanda kwenda asilimia 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni kilio kwa watumishi wengi ambao mishahara yao ni ya chini na mara nyingine husubiria mkupuo wa fedha hizi, kwa ajili ya kuanza maisha yao pale

wanapokuwa wamestaafu. Mheshimiwa Rais wetu, kama alivyosikia kilio cha madaraja, kama ambavyo alisikia kilio cha madeni ya watumishi, Mheshimiwa Rais, alielekeza kikokotoo hiki kiweze kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru na kuipongeza Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Fedha. Baada ya kukaa nao waliangalia ni namna gani bora tunaweza kupunguza kilio hiki na kuweka katika bajeti hii tunayoenda kuipitisha shilingi bilioni 155, kwa ajili ya kulipa kikokotoo, kunyanyua kutoka asilimia 33 kwa wale waliokuwa asilimia 50 kabla ya Julai 22 kwenda asilimia 40 na wale ambao walikuwa asilimia 25 vile vile hawakuachwa, mpaka Julai 22 nao wamepandishiwa kwenda asilimia 35. Hii inaonesha ni namna gani Serikali hii ya Awamu ya Sita inajali watumishi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia Waheshimiwa Wabunge wengi mmezungumzia suala la kuangalia kiwango hiki kiendelee kunyanyuka kurejea pale kilipokuwa, asilimia 50. Tumesikia utatu huu wa vyama vya wafanyakazi na waajiri; vyama vya wafanyakazi vimezungumzia namna ambavyo wanashukuru asilimia hii 40, lakini nakuomba asilimia iweze kurudi asilimia 50 lakini huu ni mwanzo mzuri, kilio hiki kimesikika na ndiyo maana asilimia saba hii imewekwa. Kadiri tunavyokwenda na kutengemaa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii inavyokuwa inaendelea, ile *actual evaluation* itakavyofanyika. Serikali itazidi kuangalia ni namna gani inarudi katika asilimia 50, lakini mwanzo huu ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge, hawa wanaokwenda kulipwa siyo tu wale ambao wanastaafu kuanzia Julai mosi mwaka huu 2024, wanaenda kulipwa wote hata wale waliostaafu kuanzia Julai Mwaka 2022. Katika bajeti hii inayoenda kupitishwa watumishi waliostaafu kuanzia Julai 22 mpaka Juni. Hivi tunavyozungumza 2024 jumla ya 17,068 wanaenda kulipwa mapunjo yao, yale ya asilimia saba ambayo walistahili kupata na wale ambao walikuwa wanapata

asilimia 33 kwenda asilimia 35 watalipwa mapunjo yao ya asilimia mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatarajia kuona wengi wakija kudai mapunjo ya mafao yao. Tutaendelea kukiangalia kikokotoo hiKi kadiri *actual evaluation* itakavyofanyika kwenye mifuko yetu ya hifadhi ya jamii. Ninawahakikishia Serikali hii ni Sikivu na itaendelea kuliangalia na kuona ni namna gani bora tunazidi kusogea katika kiwango kinachozidi zaidi ya hapa asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja tena. Ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu, ni lugha ya mazungumzo hapa mwishoni umesema mtaona wengi wakija kudai, nafikiri wanafahamika kwa hiyo, walipeni tu badala ya wao kuja kudai. Nafikiri ni lugha tu ya mazungumzo walipeni kwa sababu, la sivyo maombi yatakuwa mengi sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Chande. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi kwa mara nyingine ninasimama tena kwa mara ya kwanza kuchangia katika hotuba hii ya bajeti pamoja na Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Basi naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kunipatia nafasi hii, ili niweze kushirikiana na wenzangu katika kuhakikisha kwamba, tunalipeleka gurudumu la Taifa letu mbele na tulipeleke kwa kasi ambayo inahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa tena nafasi kufanya kazi na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, ambaye kwa kweli, ni Profesa ambaye ni mtu mwema, muadilifu na kwa kweli, nilifurahi sana kusikia kwamba, nakwenda kufanya kazi chini yake kwa sababu namfahamu. Nimefanya naye kazi katika Kamati iliyokuwa ya

Huduma na Maendeleo ya Jamii, ni mtu mwema, ni mwalimu mzuri na hakika nitajifunza mambo mengi kupitia kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwashukuru wapiga kura wangu kwa sababu, wameniwezesha kuwa hapa. Naendelea kushukuru, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kweli, nimesikiliza michango mingi ambayo imechangiwa na Wabunge katika kuboresha mpango huu au katika kutoa maoni yao katika Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. Kwa kweli, tumeweza kuchuma maoni mengi na tumeweza kupata mambo mengi mbalimbali ambayo yanakwenda kuboresha katika kuhakikisha kwamba, tunaweka mipango mizuri katika kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge Wengi sana wamechangia na mambo mengi Mheshimiwa Waziri wangu atayaeleza, lakini kwa kifupi kuna Mbunge, kwa mfano Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Ameweza kutoa maoni yake na kwa kweli, tumeweza kuyachukua ikiwa ni pamoja na kuomba kwamba, Serikali kupitia Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji tuje na mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba, mipango hii ya maendeleo inakuwa sawa kwa Mikoa yote bila kubagua Mkoa wowote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ina mipango mizuri kwa Mikoa yote. Mikoa yote inajaliwa kwa namna sawa, lakini mipango hii inatekelezwa kwa uimara mkubwa zaidi, kwa maana ya kuangali fursa zilizopo katika Mikoa hiyo, pamoja na kuhakikisha miundombinu na mahitaji mengine yote ambayo yanapewa vipaumbele katika Mikoa hiyo, basi yanafikiwa. Hii yote inategemea sana vipaumbele vya Mikoa husika ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Mwambe, ametoa mchango wake mzuri sana ambao kwa kweli, tumeupokea. Moja ya hoja aliyoitoa Mheshimiwa Geoffrey Mwambe ni, ametaka kwamba, Serikali iangalie namna ya kupitisha mapendekezo ya bajeti na mipango katika jumuiya za

wachumi, ili kupata michango zaidi kabla hatujaingia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu ni mzuri sana na kwa kweli, tumekwishaanza kufanya hivyo. Tunawashirikisha sana wachumi waweze kutoa maoni yao kuelekea katika mpango wa mwaka au kuelekea katika mpango wa kuandaa bajeti na hili limeanza kutekelezwa kama ilivyo kwa mujibu wa kanuni. Mipango hii inaanza kutekelezwa kuanzia katika ngazi ya Kata kwa maana ya *WDC* kwenda ngazi za Wilaya, Mikoa na mpaka kufika katika ngazi za Wizara hadi katika mpango wa Wizara, kwa maana ya mpango mzima kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu mchakato ni shirikishi ambao unaanzia chini kabisa. Tunaendelea kuwasisitiza Wananchi, Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuhakikisha kwamba, katika uandaaji wa mipango hii wawe wanashiriki, ili waweze kutoa vipaumbele, basi mipango hiyo iweze kuingia katika bajeti na baada ya hapo iweze kutekelezwa kwa maana ya kupelekwa mipango hiyo, ili kwenda kufanya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rweikiza naye ameweza kutoa hoja mojawapo. Ametaka Serikali, kupitia *TIC,* kuandaa miradi na andiko kuweza kuwasaidia wawekezaji wa ndani, ili kutekeleza miradi mikubwa kwa pamoja, mfano uzalishaji wa mataili ya pikipiki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa miradi mikubwa sasa hivi inashirikisha wadau ambao ni Watanzania kuhakikisha kwamba, tunawekeza katika miradi mbalimbali, ili tuweze kupata fedha na kuweza kufanya biashara. Kwa mfano tu mzuri, ukiangalia Mwaka 2022 na 2023 miradi iliyosajiliwa, ya *TIC*, tuliona kabisa hesabu zinaonesha theluthi moja ya miradi yote iliyosajiliwa ni ya Watanzania na theluthi mbili ni miradi ambayo ipo chini ya ubia, kwa maana ya Watanzania wameshiriki katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ambayo imesajiliwa na *TIC* ni 526 tofauti na ilivyokuwa Mwaka 2022 ambapo,ilikuwa ni miradi 293 tu. Miradi ya Watanzania pekee Mwaka 2022 ilikuwa ni 99, lakini mpaka kufikia 2023 ilikuwa ni 159. Kwa miradi ya ubia ilikuwa ni 130 Mwaka 2003 ukilinganisha na miradi 82 tu Mwaka 2002 na miradi ya wageni pekeyake ilikuwa ni miradi 214 kwa Mwaka 2023 na miradi 112 ambayo ilikuwa imesajiliwa Mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kwa kumalizia kusema kwamba, maoni pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara ya Mipango, tumechukua. Sasahivi tunaandaa Mpango wa Mwaka 2050, tunaomba sana kupitia Tume ya Mipango, Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na Watanzania wote, ili tuweze kuandaa mpango mzuri wa Mwaka 2050, ili tuweze kuleta maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda basi nakushukuru na mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Chande, atafuatiwa na mtoa hoja Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na pia, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Awali ya yote na mimi naungana na wenzangu, namshukuru Mwenyezi Mungu, Rahim, ambaye ametuwezesha kukutana hapa katika kikao hiki na hatimaye kuhitimisha Bajeti hii Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni mbeba maono ya Watanzania. Mheshimiwa Rais kwa uwezo wake mkubwa sana, ubingwa na ukinara wa kutafsiri sera kutoka kwenye makaratasi na kuwa kwa vitendo. Mara kadhaa tumekuwa na ndoto, sisi Watanzania, ya kuwa na miradi mikubwa kama *SGR* na mengineyo, lakini tumekuwa na ndoto ya kupeleka wanafunzi kwa mkupuo mmoja tu, siyo kwa awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu, hilo limekamilika. Hii ni kwa sababu ya uwezo mkubwa sana wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania wa kutafsiri sera kwa vitendo, lakini nimezoea kusema kwamba, sifa moja ya Mama aliyokuwanayo ni uwezo mkubwa sana wa kutafsiri chozi la watoto wetu au watoto wenu kwa vitendo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni watu wachache sana, sisi wakina baba sawa lakini uwezo huu mkubwa sana mnao ninyi wakina mama, mnajua kwamba sasa hivi kilio hiki mtoto anahitaji nini? Mnajua mtoto kilio hiki nini kinamsumbua. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nikushukuru sana wewe kwa malezi yako. Wewe umekuwa mlezi mzuri kwetu na ninavyokuambia hivi sasa hivi Wana-Kojani wanaku-*miss* sana. Siku umewatembelea wanatamani mara nyingine itokee utembelee Kojani kule. Wewe ni mlezi mzuri na tunashukuru kwa malezi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli michango yenu ni mizuri sana na ushauri wenu ni mkubwa na tumeupokea kwa mikono miwili. Hii ni kwa sababu huko nyuma wapo walionena aah! Kwamba Bunge hili la siku hizi lakini hili Bunge la Kumi na Mbili ndiyo ambalo limetoa Rais wa Mabara yote ulimwenguni. Rais wa ulimwengu ametoka ndani ya Bunge la Kumi na Mbili. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kujivuna Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, yeye ni *mentor* kwangu na ni mwalimu mzuri kwangu. Kwa hiyo, nasema kwamba huyu ni bingwa na ni miongoni mwa Mawaziri bingwa ambao wanatufunza na kutuelekeza vizuri. Mheshimiwa Waziri nikuambie tu mengine ambayo yanatokea katika jamii, ndiyo ulimwengu na ndiyo maisha. Maana yake hata washairi wameandika na wanasema kwamba;

"Wamaani nakupa neno siwate,
Ya waneni sikiapo sitete,
Duniani mtu hapendwi na wote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee pia kwa kuwashukuru sana Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, pamoja na Wizara zote za Serikali kwa kweli wanatusaidia vizuri na wanaisaidia Serikali yao kwa juhudi kubwa sana na uzalendo mkubwa sana. Kutokana na muda lakini pia nisisahau kumshukuru *care taker* wangu hapa Mheshimiwa Profesa Mkumbo, yeye alikuwa anafundisha vyuoni lakini hata hapa sisi wengine tunajifunza kutoka kwake. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, pia kwa kutuongezea *company* hapa na wewe kuturuhusu kuwa na *company*. Mwaka jana na mwaka juzi tulikuwa wawili tu hapa lakini leo tuna *company* hapa unaona naongea kidogo. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hasa nijielekeze moja kwa moja kwa hoja chache ambazo nimechagua kuzielezea kwa sababu hoja ni nyingi lakini nyingi zilikuwa ni ushauri na nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba hoja ambazo wametoa, ushauri ambao wametoa tumeuzingatia na tumeubeba kwa meno ya magego kabisa na tunaenda kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo ushauri Kamati ya Bajeti wameshauri kwamba Serikali ihakikishe mikopo ambayo inakopwa na Serikali inaelekezwa katika sekta za uzalishaji pamoja na miundombinu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mikopo yote ambayo imekopwa na Serikali imekuwa ikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo hususani kwenye miundombinu ya barabara, maji, reli na umeme, kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya 2025. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba mikopo yote ambayo itaendelea kukopwa na Serikali itaelekezwa kwenye sekta za uzalishaji ama miundombinu mbalimbali ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishauriwa kulipa madeni ya wazabuni wa dawa, kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Mei, 2024 Serikali imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 256 kwa ajili ya kulipa madai ya wazabuni waliosambaza dawa na vifaa tiba. Aidha,

mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kulipa wazabuni ambao wamesambaza dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, nimeona hapo imeshaanza kuwaka lakini naomba nimalizie hili. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba ule ushauri ambao umetoka na Wabunge basi ushauri huo umechukuliwa na Serikali. Mwisho kabisa, yupo mchangiaji mmoja Mheshimiwa Mbunge alisema kwamba kikokotoo hiki ambacho mmeongeza asilimia saba hadi kufika 40% mmefanya jambo lakini isionekane kwamba mmefanya jambo kubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nikuambie nyongeza hii ya asilimia saba ni kitu kikubwa sana kutoka 33% hadi 40% ni kikubwa sana. Hata ingekuwa asilimia moja tu basi ingekuwa ni hatua kubwa sana, kwa sababu wahenga wanasema; "Jicho hutaraji haja kila namna na penye moja na moja si moja tena." Kwa hiyo, hata ingekuwa moja tu ingekuwa inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba wafanyakazi walio wengi wameshukuru sana na Waheshimiwa Wabunge wapo ambao wametoa shukurani kuhusu jambo hili na ndiyo ulimwengu. Nimalizie kwa kusema kwamba wahenga wanasema; "Asiyeshukuru kwa yai basi na jogoo hachinjiwi." Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, aje ahitimishe sehemu ya hoja yake. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Wasaidizi wako kwa maana ya Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Zungu na Wenyeviti wa Bunge hili kwa jinsi ambavyo mmeweza kuendesha mjadala huu kwa umakini, umahiri na uwazi wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya lakini kwa

mimi binafsi nimshukuru sana kwa sababu amenipa heshima kubwa ya kuongoza Ofisi yake inayoshughulikiwa Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika historia ya nchi yetu hii ni mara ya tano nchi yetu kuwa na Wizara ya Mpango kamili. Tulianza mwaka 1965 mpaka 1975 tukawa na Wizara ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tukaendelea katikati ikachanganywa. Tukarudi tena mwaka 1980, Wizara ya Mipango na Uchumi, Ofisi ya Rais Mpango na Ubinafsishaji, Mipango na Uchumi tena na imerudi tena mara hii Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kunipa fursa hiyo na amenipa fursa na heshima ya kuingia katika historia ya kusimamia zoezi muhimu la kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya nchi hii, nikiwa Waziri wa pili tu katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya uongozi makini sana wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa uchambuzi wao makini, maoni na ushauri waliotoa. Nawashukuru siyo tu kwa utaratibu na utamaduni wa Kibunge uliozoeleka wa kushukuriana na kupongezana kama njia ya kutiana moyo. Ukweli ni kwamba nimesoma kurasa zote 82 za Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2023; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024; Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024; pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2024/2025. Kamati imeitendea haki sana Taarifa hii, uchambuzi wao ni wa kiwango cha juu sana cha weledi na maoni na ushauri wao waliotoa ni wa kizalendo sana. Tunawashukuru sana Kamati ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia; jumla ya Wabunge 137 ambao wamechangia moja kwa moja kwa kuongea, tumepokea maoni na ushauri wao. Aidha, tumepokea changamoto ambazo wamezitoa na tunaendelea kuzifanyia kazi. Sisi kama binadamu, kama Viongozi na kama Taasisi siku zote nafasi ya kuboresha na kuwa bora zaidi leo kuliko jana ipo na

tunaamini kwamba michango ambayo wametoa itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nijielekeze sasa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo walizitoa. Kwa ujumla wake katika michango yao kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Wwaka 2024/2025, Waheshimiwa Wabunge, wametoa maoni na ushauri katika maeneo mengi. Naomba nijielekeze katika maeneo mahususi saba na baadaye nitatoa pia maelezo kidogo kwenye maeneo ya jumla matatu hivi.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, ni kuhusu vipaumbele vya kuzingatia katika mipango yetu ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ikiwemo Dira yetu ya Maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wamependekeza maeneo kadhaa ya kuzingatia na wamesisitiza tuweke mkazo katika maeneo ambayo yatasukuma ukuaji wa uchumi kuelekea asilimia nane ambayo ndiyo lengo ambalo lipo katika Mpango wetu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wameweka mkazo katika maeneo ya kipaumbele muhimu kama elimu na mafunzo, kilimo, nishati, madini, sayansi, teknolojia, utafiti na maendeleo na maeneo mengine. Nisisitize kama nilivyosema katika hotuba yangu kwamba kipaumbele kikubwa cha Serikali ni kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi ili uchumi huo uweze kupunguza umaskini na kuwezesha watu wetu kuzalisha mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tufike katika katika eneo hili lazima tujielekeze katika sekta ambazo zinabeba watu walio wengi. Sekta hizi ukiangalia grafu ambayo tuliitoa ni muhimu tujielekeze katika sekta nne muhimu sana. Sekta ya kwanza, sekta ya kilimo, kwa sababu inabeba 65% ya watu wetu na inachukua zaidi ya robo ya Pato letu la Taifa. Kwa sasa kilimo chetu kinakuwa kwa 4.2%, lengo la Serikali ni kuona kwamba ifikapo mwaka 2010 sekta hii ikuwe angalau kwa 10% hili ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni eneo la viwanda, viwanda ndio vinatarajiwa kuzalisha ajira kwa wingi. Kwa sasa viwanda vinakuwa na sekta hii inakuwa kwa 4.3%. Lengo la Serikali ni kuona kwamba ikue angalau ifike asilimia saba mpaka asilimia nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, muhimu ni biashara, biashara pia inabeba watu wengi na ni eneo ambalo ni muhimu sana katika kuzalisha ajira. Hili na lenyewe linakuwa kwa asilimia 4.2, lakini lengo la Serikali na lenyewe likue lielekee asilimia saba mpaka nane.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho, ni usafirishaji, ni eneo muhimu sana takwimu zinaonesha kwamba linakuwa kwa 4.1% na lenyewe lazima tulisukume liende kwenye asilimia sita mpaka nane.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo Serikali inayawekeza ili tuone kwamba yakue kwa kiwango angalau kisichopungua asilimia sita mpaka nane na kwa mtindo huo tunaweza tukasogeza uchumi wetu ukuwe mpaka asilimia nane ambayo ipo katika Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelitolea maoni ni haja ya kuimarisha mfumo wa usimamizi wa Mipango ya Maendeleo na hapa tumeeleza Waheshimiwa Wabunge wengi wameunga mkono. Tunakubaliana na maoni yao kwamba tupunguze muda ule wa kutoa taarifa ya Kitaifa badala ya mwaka mmoja iwe ni miezi sita walitoa maoni haya. Kwa hivyo, itasomeka kwamba Waziri atapokea taarifa kila wiki; kila mwezi Wizara itawasilisha kwenye Tume ya Mipango na Tume ya Mipango itaanda taarifa ya Kitaifa mara mbili kwa mwaka (miezi sita sita). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, ilikuwa ni haja ya kufanya tathmini ya rasilimali watu ili kutambua idadi na aina ya watu wanaohitajika katika dunia ya leo. Kama tunavyofahamu kwa mujibu wa Sheria Na. 1 ya Tume ya Mipango ya mwaka 2023

hususani Kifungu 6(2)(a), jukumu la kwanza la Tume ya Mipango ni kutathmini hali ya rasilimali za Taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya rasilimali hizo. Kwa kuzingatia jukumu hili katika mpango wake wa kazi wa mwaka ujao wa fedha Tume ya Mipango imejipangia kufanya tafiti kadhaa ikiwemo hii ya kutathmini hali ya rasilimali watu, tukizingatia idadi na aina ya rasilimali ambazo tunazo lakini kuelekeea mbele tunahitaji rasilimali za aina gani katika uchumi wa dunia ya leo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ameeleza hapa kwamba tayari Serikali imeshafanya mapito ya Sera na Mitaala yake ya Elimu. Kwa hivyo, tumeiweka katika kiwango ambacho tunaamini inaenda vizuri na dunia ya leo.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ambalo Waheshimiwa Wabunge walitolea maoni ni haja ya kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini sambamba na kuweka mazingira bora ya kurasmisha sekta isiyo rasmi. Hili ni eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelichangia na tunakubaliana na maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisitize mambo matatu; La kwanza, tayari pale katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* tumeshafungua Kituo cha Kuhudumia Wateja cha Pamoja *(One Stop Centre)*. Kwa hivyo, mwekezaji popote alipo anaingia katika tovuti ya *TIC,* mule ndani ana uwezo wa kuomba ambacho anahitaji na atapata huduma za taasisi ambazo hazipungi saba kwa kuanzia. Baada ya hapo tunatarajia katika mwaka ujao wa fedha zifike taasisi 14. Kwa hivyo, ukienda pale unapata huduma ya taasisi 14 ikiwemo kusajili kampuni yako. Juzi nimezindua huduma nyingine kwamba unaweza ukafungua mpaka akaunti yako ya fedha pale. Kwa hivyo, hii ni hatua kubwa ambayo wawekezaji wengi sana wameifurahia.

Mheshimiwa Spika, ya pili, tunapoelekea ni kwamba tunataka tozo za mamlaka mbalimbali za uthibiti zilipwe mara moja. Badala ya mwekezaji kuzunguka aende kulipa *EWURA,* aende kulipa *TBS* aende kulipa na nyingine. Tunataka mwekezaji

alipe tozo mara moja na sisi ndani ya Serikali ndiyo tutakao gawana hela ambayo wamelipa kulikoni mwekezaji kuzunguka leo *OSHA,* kesho *FIRE,* kesho *EWURA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, la pili, mwaka huu tunaenda kuweka mfumo wa kutoa cheti kimoja badala ya utitiri wa vyeti. Tunafahamu wote ukiingia kwenye kampuni yoyote ya biashara kwenye ukuta ukiangalia utakutana na vyeti visivyopungua vitano mpaka kumi. Tunataka utaratibu huo tuachane nao, katika ulimwengu wa teknolojia inawezekana ukapata cheti kimoja ambacho ndani yake kuna kila kitu. Hili tunaenda kulifanyia kazi katika mwaka ujao wa fedha katika kurahisisha mazingira ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tano, ni suala la kuweka mkazo katika maendeleo ya vijijini, Waheshimiwa Wabunge walio wengi wameunga mkono lengo la Serikali kuendelea kuweka mkazo katika maendeleo vijijini. Hakuna namna ya kutokomeza umaskini wa watu wetu nje ya kuweka mkazo wa kipekee katika kusimamia maendeleo ya vijijini kama njia sahihi ya kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi na tayari tuna misingi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kupitia *TARURA* mtandao wa barabara vijijini umeongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, kati ya mwaka 2020 na 2024 Serikali kupitia *TARURA* ilifanikiwa kuongeza kiwango cha barabara cha changarawe kutoka kilometa 24,493 hadi kufikia kilometa 41,107 mwaka 2024 ikiwa ni zaidi ya lengo. Lengo letu lilikuwa ni kupeleka kilometa 35,000 ifikapo mwaka kesho. Tayari tuna mtandao wa barabara kupiti *TARURA* kilometa 41,107.52. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unafahamu kwenye lengo la kuwezesha watu wetu kupata kipato, kufanya biashara suala barabara vijijini ni muhimu sana. Tukishakuwa na mtandao wa barabara vijijini hii maana yake itasaidia wananchi kuweza kufanya biashara kuweza kusafirisha mazao yao ya mifugo kilimo, uvuvi na kadhalika kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kujipatia kipato. Vilevile, kiwango cha barabara za lami kupitia *TARURA* kimeongezeka kutoka kilometa 2,205, mwaka 2020 mpaka

kilometa 3,224 mwaka 2024 na kwa miradi inayoendelea tunaamini kwamba hatua kubwa zaidi itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, muhimu sana kwa vijijini suala la maji, tumepiga hatua kubwa sana katika eneo hili. Wakati tunaanza utekelezaji wa Dira ya sasa *coverage* ya maji vijijini ilikuwa 32%. Sasa hivi tunazungumzia 78%, hii ni hatua kubwa sana na ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wetu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, ambalo tumelisema wote hapa ni suala la umeme, hili tumepiga hatua kubwa zaidi ya 96% ya vijiji vyetu vina umeme. Hii ni hatua kubwa ambayo Serikali imeifanya na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa uongozi wake makini.

Mheshimiwa Spika, bila shaka vilevile mtandao wa barabara kwa ujumla kwa kutumia, kwa mfano, *TANROADS* umeongezeka sana wakati mwingine tunajisahau. Mwaka 2000 *TANROADS* mtandao wao wote ilikuwa ni kilometa 4,179, leo tunazungumzia kilometa 11,966. Wakati mwingine takwimu siyo muhimu hali halisi. Wale wanaotoka Singida kama mimi na mikoa mingine ya magharibi wanafahamu walikuwa wakisafiri Mwanza, Shinyanga na Singida; kutoka Singida wakifika Nala ilikuwa gari linasimama ubadilishe nguo ukung'ute vumbi ili kuelekea Dar es Saalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka kufika pale Nala ilikuwa ni vumbi tupu, hali ilikuwa mbaya, lakini wengi wanafahamu wanakumbuka miaka michache iliyopita kwenda Mwanza ilibidi upitie Nairobi lakini leo mtandao wa barabara kutoka Mtwara mpaka Mwanza ni barabara za lami, kwa hivyo hatua kubwa imepigwa sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita ni haja ya kuimarisha mashirika ya umma. Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza na kushauri kuwa Serikali ifanye tathmini ya kina kubaini mashirika ya umma ambayo yanafanya biashara na yaweze kufanya biashara na yatoe mchango kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kama mnavyofahamu ipo katika hatua za kufanyia maboresho na marekebisho makubwa sana mashirika ya umma ili mashirika haya yaweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi na hususani mashirika yale ambayo wanapaswa kujiendesha kibiashara. Katika sheria ambayo tunaipendekeza ambayo itakuja kusomwa mara ya pili tunasisitiza mambo mengi lakini mambo mawili muhimu.

Mheshimiwa Spika, moja ni kuwa na mfuko wa uwekezaji ili taasisi zetu ambazo zinafanya biashara ziwe na uhakika wa vyanzo vya kuweza kuwekeza. Pili, tunataka mashirika haya yaweze kumilikiwa na wananchi kwa hivyo yajisajili kwenye soko letu la hisa la Dar es Salaam na kwa njia hiyo wananchi wanaweza wakanunua hisa katika mashirika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la saba ni maandalizi ya Dira mpya ya taifa ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza sana, ushirikishwaji lakini pia kuzingatia vipaumbele ambavyo nimevieleza awali. Niendelee kusisitiza kwamba zoezi hili lina ushirikishwaji wa kutosha na mpaka mwezi Mei zaidi ya watu laki nane walishatoa maoni kwa njia mbalimbali ikiwemo mahojiano katika ngazi ya kaya, wametoa maoni kupitia simu, kupitia tovuti lakini pia kupitia makundi mbalimbali ya kijamii na mahojiano ya viongozi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo linafurahisha ni kwamba asilimia 80 ya wananchi waliotoa maoni kwa njia ya simu na tovuti ni vijana kati ya miaka 15 na miaka 35. Kwa hiyo vijana wamechangamkia sana eneo hili. Eneo la pili ambalo walisisitiza kwenye upande dira Waheshimiwa Wabunge wameshauri kwamba ni muhimu sana tukajifunza kutoka nchi ambazo zimepiga hatua kimaendeleo*(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, nitoe taarifa tu kwamba timu yetu kuu ya wataalam imeshabaini angalau nchi kumi ambazo zina mazingira kama ya kwetu ya kihistoria na ambazo zimepiga hatua kubwa ambazo tunaende kujifunza nchini pamoja na India kwa mfano, Indonesia, China, Singapore, Korea Kusini, Vietnam, Botswana,

Maurtius, Norway na zingine, kwa hivyo ushauri huu utazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la saba la mwisho katika maoni mahsusi ni eneo la mpango na bajeti. Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba ni muhimu sana mpango uje mapema ili uweze ku-*inform* bajeti. Maoni haya ni mazuri na yatazingatiwa ni suala pia la kikanuni kwa Mheshimiwa Spika hili pia lipo mezani kwako lakini niseme kwamba kimsingi hivi ndivyo ambavyo imekuwa ikifanyika kwa kiasi kikubwa kwa sababu kama mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge mwaka jana tarehe sita mpaka tarehe kumi Novemba tulikaa hapa Wabunge kujadili mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Kitaifa. Kwa hiyo, hili linazingatiwa lakini pia Machi tarehe 11 mwaka huu 2024 nilisoma, nalileta hapa mpango wa maendeleo ya Taifa, kwa hivyo njia hizi zinashirikishwa lakini nadhani fursa na nafasi ya kuboresha ipo, sisi wenyewe Wabunge ndiyo tunatunga kanuni zetu kama tukiamua kubadilisha ni suala la sisi kufanya uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufafanua nimalizie kutoa ufafanuzi katika maeneo ya jumla matatu. Eneo la kwanza nataka kusisitiza kwamba pamoja na mambo mengine mpango wa maendeleo ambao niliuwasilisha hapa pamoja na hatua za kikodi ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizitangaza, zinalenga katika mambo makubwa matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kuchochea uzalishaji wa bidhaa zitakazoifanya nchi yetu ijitosheleze katika mahitaji ya bidhaa muhimu nchini na kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje. Wote tunafahamu kwamba kuna bidhaa ambazo tunazitumia sana ni muhimu katika maisha yetu lakini tunaziagiza kutoka nje na tumekuwa tukipiga kelele hapa. Bidhaa hizi ni pamoja na chakula mfano mafuta ya kula, sukari, ngano, mazao ya chakula, madawa, mavazi na kadhalika. Ni katika msingi huu tutaendelea kulinda uwekezaji unaolenga kuchochea viwanda vinavyozalisha bidhaa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza suala la sukari hapa, kwa upande wa sukari kwa mfano, mahitaji yetu kwa mwaka

tunakadiria kuwa takribani tani laki sita elfu Hamsini, mwaka jana kwa kweli kabla ya mvua za El-Nino tulishapiga hatua kubwa, tulienda mpaka tani 460,000 kwa mwaka lakini kutokana na mvua za El-Nino hizi uzalishaji viwandani ukayumba, ukashuka mpaka tani 392,724 lakini tunaamini kwa uwekezaji ambao unaendelea na kama hapatajitokeza tena changamoto za El-Nino tunatarajia ifikapo julai mwaka kesho tufike angalau tani 520,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2025/2026 tuzalishe tani 700,000. Kwa hivyo, nisisitize hapa kwamba lengo la Serikali kuendelea kulinda uwekezaji katika viwanda vya sukari lipo pale pale, na tuwaambie wenye viwanda ambao tunafanya nao kazi kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba sekta hii sukari inakua, tufike mahala tujitegemee lakini muhimu zaidi tuweze kuuza sukari nje ya nchi kwa sababu nchi nyingi jirani zetu hawana sukari.

Mheshimiwa Spika, nisisitize Serikali inafanya nini? Tunafanya uwekezaji mkubwa sana katika uendelezaji wa sekta ya uzalishaji wa ndani. Kwa mfano, Serikali imewekeza shilingi bilioni 7.2 kuzalisha mbegu bora za sukari. Serikali imewekeza bilioni 12.5 kwenye miundombinu ya umwagiliaji ya miwa *especially* kwenye bonde la Kilimanjaro. Sasa hivi tunayo kampuni ya saba kutoka Ethiopia ambayo inafanya *visibility study* kwenye bonde zima la Kilombero lengo tukuze umwagiliaji katika eneo hilo na hii itakuwa ni hatua kubwa sana kwenye kuongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumegawa kitalu kipya hekta 400 bure za mbegu kwa wakulima ili waweze kulima, kwa hivyo mtu anayesema kwamba hatua zote ambazo tumezichukua hivi karibuni lengo lake ni kukatisha tamaa wawekezaji katika sekta ya sukari hajui alisemalo, Serikali inawekeza sana.

Mheshimiwa Spika, ukiacha yote hayo Serikali imesamehe kodi takribani shilingi bilioni 244 kwenye viwanda hivi ili kuweka mazingira rahisi ya wao kuwekeza. Tungekuwa hatuna nia ya kulinda uwekezaji isingewezekana tusamehe kodi yote hiyo, tufanye uwekezaji wote huo. Kwa hiyo, hili ni jambo la muhimu ambalo nataka tulisisitize kwamba lengo la Serikali lipo pale pale,

tujitosheleze kwa malengo katika sekta ya sukari na tuachane na mambo ya *sugar gap* na sisi tunaamini kwamba kwa jitihada hii ifikapo mwaka kesho suala la *sugar gap* katika nchi hii litakuwa ni suala la historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo linahusiana na hilo, lazima Serikali ihakikishe pamoja na kwamba tunalinda viwanda na uzalishaji lakini lazima kuhakikisha kwamba bidhaa muhimu zinapatikana nchini muda wote na kwa bei nzuri kwa walaji. Ni katika mazingira haya ilikuwa ni muhimu kwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuchukuwa hatua za dharura katika kuhakikisha kuwa bidhaa muhimu ya sukari inaendelea kupatikana nchi na kwa bei nzuri. Kutokana na mafunzo tuliyoyapata, mafunzo ambayo tumejifunza, kila siku tunajifunza, huko nyuma tuliona kwamba ni muhimu wapewe watu fulani kuagiza sukari ili kuondoa uholela wa soko ndiyo tukawapa wenye viwanda, lakini tumejifunza mwaka jana kwamba hii nayo ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo bidhaa muhimu zinakosekana katika soko atakayelaumiwa kwa vyovyote vile ni Serikali. Kwa hivyo lazima Serikali yoyote makini ichukue hatua za kulinda walaji katika mazingira ya soko huria. Kwa hivyo, hii ni muhimu sana kuizingatia wakati wote. Kwa hiyo, hatua hizi nisisitize tena, hazilengi kudhoofisha uwekezaji katika sekta ya sukari bali Serikali inachukuwa jukumu lake la msingi la kulinda wananchi dhidi ya mabavu ya soko huria. Serikali ni mwekezaji muhimu kama nilivyosema katika sekta ya sukari nchini na isingewezekana ijihujumu yenyewe. Hili ni jambo la muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika viwanda vyote vya sukari nchini unakadiriwa kuwa takriban trilioni 4.2. huu ni uwekezaji mkubwa ambao kama Serikali lazima tuendelee kuulinda. Eneo la tatu ni kuchochea mauzo ya bidhaa ambazo zimeongezewa thamani nje ya nchi. Pili, nizungumzie pia haja ya kuwa na mipango ya muda mrefu na ulinzi dhidi ya maono ya kitaifa. Jambo hili limezungumzwa kwa upana na Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Askofu Gwajima amekuwa akilirejea mara kwa mara ni muhimu sana, ni hoja ya msingi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo dhana ambayo kwa kweli imekuwa ikijirudia kwamba nchi yetu na pengine nchi zingine za Kiafrika zinakwama kwa kuwa hatuna maono na mipango ya Taifa ya muda mrefu. Hii ni hoja ambayo imezungumzwa kwa upana. Pamoja na umuhimu wa hoja hii, kwa lengo la kuweka kumbukumbu sahihi, nchi yetu hii ya Tanzania imekuwa na mipango katika historia yake yote. Katika Bunge la kwanza kabisa la wakati huo la Tanganyika na Mkutano wa Tano na Kikao cha Kwanza kilichofanyika tarehe 10 Disemba mwaka 1962, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa ndiyo amechukua Urais wa Jamhuri alikaribishwa kuhutubia Bunge kwa mara ya kwanza kama Rais wa Jamhuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hiyo pamoja na mambo mengine alitangaza kuanzisha idara mpya akaiita Idara ya Mipango ya Maendeleo, aliiweka chini ya ofisi yake. Jambo hili limekuja kujirudia tena mwaka 2023 pale ambapo Mheshimiwa Rais aliunda Ofisi ya Rais Mpango akaiweka chini ya ofisi yake. Lakini limefanyika jambo la ziada, Tume ya Mipango imekuwepo huko nyuma lakini safari hii imetungiwa sheria. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya kulinda maono ya Taifa hili ni hatua ya kulinda taasisi ambayo inasimamia mipango. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumeanzisha taasisi ya Tume ya Mipango, tumeipa majukumu 20 na taasisi hii sasa mtu hawezi tu hapa akakurupuka akaifuta, lazima alete katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere wakati anaanzisha alisema na naomba kunukuu "nakusudia kuanzisha idara mpya, Idara ya mipango ya maendeleo, idara hiyo itakuwa chini yangu mwenyewe na itajitahidi kadri iwezekanavyo kutayarisha mipango hususan ya vijijini kwa nchi nzima". Kwa hiyo, tangu tupate uhuru hatua yetu ya kwanza kabisa chini ya Rais wetu wa kwanza ilikuwa ni kuanzisha Idara ya Mipango na kazi ya kwanza ya idara hii ilikuwa ni kuandaa mpango wa kwanza wa maendeleo wa muda mrefu na mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa kwanza wa muda mrefu wa nchi ulikuwa ni wa mwaka 1964 - 1980, miaka 16. Mpango huo ulilenga kuongeza pato la mtu kutoka dola za kimarekani 55 wakati huo pato la Mtanzania ilikuwa dola za kimarekani 55 na tulisema ifikapo mwaka 1980 ziwe zimefika dola za Kimarekani 165. Leo tupo dola 1,222 kwa hivyo hata kwa takwimu hii tu mtu anayesema hatupigi hatua anatuonea sana, na ililenga kuinua umri wa kuishi kutoka miaka 35 wakati ule uende mpaka miaka 50 leo tupo miaka 66. Kwa hivyo, tangu mwanzo mpango ulikuwepo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine maarufu sana ambao tunaufahamu ni wa mwaka 1975-1995 ambao ulilenga mahsusi kabisa kwenye viwanda, ulikuwa unaitwa *basic industry strategy*, mpango pia ulikuwepo. Kwa hivyo miaka yote hii tumekuwa na mipango hiyo, lakini kwa mara ya kwanza mwaka 1998 nchi yetu ilianzisha mchakato wa kuandika dira ya taifa ya maendeleo ambayo ilianza kutekelezwa rasmi mwaka 2000 awamu ya tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kujadiliana kuhusu utekelezaji wa mipango yetu na mikakati yake lakini kwamba nchi hii imekuwa haina mipango haiwezi kuwa kweli. Hata Azimio la Arusha la 1967 mpaka miaka ya 2000 ilikuwa ni mpango wa maendeleo wa muda mrefu na kwa kweli ilikuwa ni dira ya taifa. Tunaweza kujadiliana kuhusu ufanisi wa utekelezaji, kwamba tumekuwa hatuna mipango haiwezi kuwa kweli sana. Kwa hiyo, hilo nilitaka nilitolee maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho katika eneo hili imezungumzwa hapa kwamba uteuzi wa viongozi wa Serikali na taasisi zake uzingatie sifa za kitaaluma na weledi na maadili. Ni jambo la msingi na ni muhimu sana katika ulimwengu wa leo. Ulimwengu wa leo ni ulimwengu wanaita wa kiuwedi *(meritocracy)* kwa hiyo hatuwezi kupingana nalo.

Mheshimiwa Spika, *of course* baadhi ya Wajumbe katika michango yao ndani na nje hata ya Bunge kwa njia moja au nyingine wanatilia shaka hata sifa na weledi wa baadhi ya

wateuliwa. hili ni muhimu kama nilivyosema, tunasisitiza mambo matatu, weledi ni muhimu, maadili ni muhimu lakini *of course* kufanya kazi kwa bidii ni nyenzo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge na hata Watanzania kwamba teuzi zetu ambazo zinafanywa na viongozi wetu zinazingatia sana vigezo hivi kwa maana ya sifa za kitaaluma, sifa za kiuweledi, sifa za kufanya kazi kwa bidiii na hata sifa za kimaadili. Wengi hapa jana mmepongeza hata Baraza la Mawaziri hapa kwamba tunachapa kazi kwa bidii. Ukiangalia kwa mfano wateule wa kwanza kabisa wa Mheshimiwa Rais ni Baraza lako hili la Mawaziri pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na siamini kwamba kuna mtu anatilia shaka sifa za wajumbe hawa 25 wa Baraza la Mawaziri pamoja na Manaibu wao. Mawaziri wanatoka wapi? Mawaziri wanatoka miongoni mwa Wabunge na mimi ninaamini hakuna mtu anayetilia shaka juu ya sifa za Wabunge wa Bunge hili la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia muundo wa Bunge, nimefanya kauchambuzi kidogo, muundo wa Bunge hili la 12 unaonesha kuwa kitaaluma kwa mfano na kiuweledi asilimia 9 ya Wabunge wana Shahada za Uzamivu *(PhD)* Bunge lako akiwemo Spika mwenyewe. Ukiangalia asilimia 34 wana Shahada za Uzamili *(Master's Degree)*. Kwa hiyo, ukijumlisha tu *Masters* na *PhD* unazungumzia asilimia 41. Asilimia 21 wana Shahada ya Kwanza, asilimia 32 wana ama Diploma, Kidato cha Sita ama Kidato cha nne. Asilimi 4 peke yake ndiyo darasa la saba katika Bunge lako hili. Sasa utahoji vipi juu ya sifa za kitaaluma kitaalamu na kiweledi wa Bunge hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimfanya fanya uchambuzi, ni moja ya Mabunge ambayo sifa hizo hapa Afrika zipo juu sana wakiongozwa na Spika wake. Sasa utatilia shaka juu ya weledi wa Spika huyu kitaaluma, *integrity*, bidii! Tafadhali sana! Sasa ukisogea katika Wajumbe 25 wa Baraza la Mawaziri ambao wanatokana na Bunge hili, asilimia 28 wana Shahada za Uzamivu, asilimia 36 wana Shahada ya Pili *(master's)* yaani Baraza hili asilimia 61 takribani theluthi mbili wana *master's* na *PhD,* asilimia

nane wana Shahada ya Kwanza, wameishia hapo. Utatilia vipi shaka juu ya weledi na sifa za kitaaluma za Baraza hili la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Kwa hiyo, tunaweza kukosoana kwenye mambo mengine lakini siyo juu ya sifa za kitaaluma, za kitaalamu na za kiweledi, sifa hizi katika Bunge hili na katika Baraza hili zipo za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachopaswa kuimarisha ni mifumo yetu ya uwajibikaji na kuendelea kujenga uwezo wa watu wetu katika utumishi wa umma. Hatuwezi kukata mwembe wote kwa sababu tu ya kuoza kwa maembe wawili, hapana. Kama kuna maembe mawili ambayo yameoza ndani ya utumishi wetu wa umma tutashughulika nayo, lakini hatuwezi kukata mwembe mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie; *a bit personal* lakini nitoe hizi takwimu zifuatazo kwenye sekta ya kilimo. Moja, kwa maono yangu sasa hivi kuna *clarity* kubwa sana juu ya nini tunafanya katika sekta ya kilimo. Mambo manne; mbegu bora, matumizi ya mbolea, kilimo cha umwagiliaji na zana za kisasa *(mechanization)*. Ndiyo mambo ambayo tunayafanya ili yatusaidie kuongeza tija, na yote hayo ukiangalia yanakwenda juu. Mbegu bora zinaongezeka, matumizi ya mbolea yanaongezeka, eneo la kilimo cha umwagiliaji linaongezeka na matumizi ya zana za kisasa za kilimo yanaongezeka, na matokeo yake ni kwamba uzalishaji umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazao 84 yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo uzalishaji umeongezeka kutoka tani milioni 30.6 mwaka 2021 mpaka tani milioni 36.4. Kitu gani kimetokea pia? Utoshelevu wa chakula umeongezeka kutoka chini ya asilimia 100 mwaka 2010 na leo tunazungumzia asilimia 124. Lengo letu mwaka kesho tufike asilimia 130. Muhimu zaidi uzalishaji wa mazao ya viwandani umeongezeka toka laki tisa mpaka tani milioni 1.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya kilimo, tumetoka wapi? Mwaka 2021 ulikuwa asilimia 2.7, mwaka 2022, asilimia 3.3, mwaka 2023 asilimia 4.2. Lengo letu ni kwamba sekta hii ikue kwa

asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Kwa jitihada hizi ninaamini kwamba tutafika na tukapata mapema. Ninayasema haya kwa sababu kilimo ni sekta muhimu. Haya ni mafanikio makubwa sana katika sekta ya kilimo katika muda mfupi uliopita. Mafanikio haya hajileti yenyewe, wapo watu nyuma yake; yupo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii tuna tabia na utamaduni wa kutokuaminiana. Ulifanyika utafiti mwaka 2014 ukaonesha kwamba katika watu 10 Watanzania saba hawaaminiani, wanashukiana; na kwa sababu hiyo tumekuwa na tabia mtu anayefanya vizuri huamini kwamba amefanya vizuri kwa nia nje, unaamini kuna kitu tu siyo bure. Tumekuwa tukifanya hivyo na tunawakatisha tamaa watu ambao wanafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe. Mafanikio yote haya ambayo nimeyasoma hapa ni kwa sababu kuna usimamizi imara wa sekta husika. Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu kuwatia moyo watu wanaofanya vizuri, tusiwakatishe tamaa. Tusipokuwa makini tutakuwa tunakwenda mbele hatua 10 na tunarudi nyuma hatua 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima mtu anayefanya kazi kwa bidii atafanya makosa, muhimu ni kwamba ajue na arekebishe lakini siyo kumkatisha tamaa. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii, mimi kama Waziri wa Mipango siwezi kusoma mafanikio ya mipango yangu bila sekta ya kilimo. Mheshimiwa Bashe tunakushukuru sana kwa kusimamia sekta hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kunukuu maneno kuntu sana ya Mzee John Samuel Malecela, aliyoyatoa mwaka 2010 wakati anawasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika jimbo lake wakati huo la Mtera. Alisema maneno haya; "Tangu kale hakijatokea chama chochote cha siasa au mfumo wa utawala ambao umekuwa na utaratibu wa kuwatajirisha watu wachache. Badala yake Chama chochote cha siasa kunachotaka kuheshimika kimetetea utoaji wa fursa sawa katika

umiliki wa rasilimali za nchi; na ndiyo sababu vyama vyote vya siasa vinavyotaka kuheshimika vimekuwa vinajitahidi kusimama imara, kupambana na umasikini na kuwatetea wanyonge. Haya ndiyo yanyofanywa na viongozi wa Chama cha Mapinduzi na ndiyo maana kinaheshimika duniani." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie nukuu hapa ya mwisho anasema, siyo mimi ni Mzee Malecela anasema, "Haya ndiyo yanayofanywa na viongozi wa Chama cha Mapinduzi na ndiyo maana kinaheshimika dunia." Ninaamini maneno haya yanaishi hadi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninakushukuru tena kwa fursa uliyonipa. Niwashukuru sana wasaidizi ambao tunafanya nao kazi; Mheshimiwa Naibu Waziri, Stanslaus Nyongo na ninamshukuru sana kwa sababu kaingia katikati lakini tayari ameshai-*capture* sekta vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu wetu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, na ninawashukuru sana Ndugu Laurance Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango kwa jinsi ambavyo ameweza kuisimamisha tume hii ndani ya mwaka mmoja taasisi imekamilika na juzi amepata wasaidizi wake; Makatibu watendaji wasaidizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwatoe wasiwasi baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ikiwemo Kamati yetu ambayo ilisema tuanzishe mamlaka ya usimamizi wa ufuatiliaji. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama mlivyotunga hii sheria, kimsingi Tume ya Mipango ndiyo imepewa jukumu hilo na tunaye Naibu Katibu Mtendaji wa Tume anayeshughulikia tu suala la ufuatiliaji na tathimini ya maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Ndugu Nehemiah Mchechu ambaye ni Msajiri wa Hazina kwa usimamizi mzuri wa mashirika ya umma. Mdogo wangu Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji, anafanya kazi nzuri sana na anasifiwa, Ndugu yangu Charles Tembe ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *EPZA*

na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Tume ya Mipango pamoja na taasisi nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumshukuru sana ndugu yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ambaye Ofisi hiyo ambayo unaiongoza ilimegwa upande mmoja kutoka kwake na kipande kimoja kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. Alinikaribisha vizuri, tumeshirikiana na amenipa ushirikiano mzuri sana. Muhimu zaidi ni kwamba fedha zote ambazo zilihitajika kuanzisha taasisi chini ya ofisi hii amezitoa kwa haraka sana. Mungu akubariki sana; na tunaendelea kushirikiana vizuri katika majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili aje ahitimishe hoja yake, kuna wageni wengine ambao wameingia na wengine wanasubiri. Wakati wa tangazo la awali nimeletewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolijia ya Habari kwamba ilipotambulishwa kwamba ni familia wawili walikuwa ni familia wengine ni watumishi wake. Moja, yupo katibu wake Naibu Waziri, anaitwa Peter Ngaya. Pia, yupo Erick Mange ambaye ni dereva wa Naibu Waziri. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, wapo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha. Hawa ni viongozi kutoka ya Wizara ya Fedha; lakini kwa sababu tumeshawatangaza mara kadhaa hapa Bungeni kipindi hiki, naomba wasimame wote kwa pamoja wakiongozwa na Dkt. Natu El-maamry Mwamba ambaye ni Katibu Mkuu. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hawa ni viongozi kutoka Tume ya Taifa ya Mipango; na wenyewe kwa sababu tumeshapata nafasi ya kuwatambulisha huko nyuma, wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wenu wengine. Wageni saba wa Mheshimiwa George Nathany Malima ambao ni Wachungaji na Wafanyakazi kutoka Kanisa la *St.* Alban kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 136 wa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekulu; wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Amka Afrika wakiongozwa na Mkurugenzi wa Shule Ndugu Simon Msangi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 101 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari Buigiri ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 96 na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Martin Luther ya Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema tunapofikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 13 Juni mwaka 2024 niliwasilisha katika Bunge lako Tukufu Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe mwenyewe moja kwa moja, Naibu wako pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa

kuruhusu mijadala kufanyika kwa weledi na kwa demokrasia ya kiwango cha juu. Tunakushukuru sana. Pia tunakushukuru sana kwa jinsi ambavyo unatulea tukiwa hapa Dodoma. Kuna wakati hoja za Waheshimiwa Wabunge zinakuwa za moto sana lakini umekuwa na ratiba ambazo zinatufanya Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata juzi uliandaa tamasha ambapo kupitia kwenye tamasha hilo niliweza kulipa kisasi kwa Babu Taletale ambaye alikuwa akinishinda mazoezini. Nilimshinda kwenye mita 100 kwa kumpita kama amesimama na hiyo imesababisha nipokee ofa nyingi sana za usajili. Basi hoja zote hizo zipelekwenye kwa meneja wangu wa usajili ambaye ni Ahmed Ally, Msemaji wa Simba. Babu Tale ameomba shindano lirudiwe, mimi niko tayari. Tunakushukuru sana kwa malezi hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua kazi kubwa inayofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, wakishirikiana pakubwa na Makamu Mwenyekiti ndugu yangu Twaha Mpembenwe pamoja na Kamati nzima ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tumepokea hoja za Waheshimiwa Wabunge wote, tunawashukuru sana kwa hoja nzuri sana ambazo mmetuletea; na kwa ajili ya ubora wa hoja hizo zilizotolewa nitakuomba nitoe ufafanuzi kwa utulivu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru watendaji wa Wizara ya Fedha, tukianza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ambaye ananisaidia kwa ukaribu sana, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge, Naibu Waziri wa viwango vya Wizara ya Fedha na Viwango vya Kidunia. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa unaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi ziende pia kwa timu ya wataalam wa Wizara ya Fedha. Hawa wamekuwa wakikesha ili

kuhakikisha kwamba gurudumu hili la Wizara ya Fedha linakwenda chini ya uongozi wake, Mwalimu wangu Dkt. Natu El-maamry Mwamba pamoja na taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitoe pongezi na shukurani kwa viongozi wetu wakuu ambao wamekuwa wakitupatia miongozo hapa; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na *Chief Whip*. Kweli tumekuwa nao bega kwa bega, hata wizara za kisekta wanazisimamia kama sekta ambazo ziko moja kwa moja chini ya sekta za kiwizara. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kurejea pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nilisema wakati nikiwasilisha taarifa hii, narejea kusema, "Mheshimiwa Rais ameonesha uwezo wa waziwazi na mpaka nchi zingine wanaona mambo makubwa ambayo Tanzania inafanya.Tumezunguka katika baadhi ya nchi nyingi lakini kote kule tumeona jinsi wanavyoichukulia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaheshimika kule duniani. Kote tunakokwenda, nchi yetu inaheshimika kule duniani. Si tu kwa kuheshimika kwa kuitaja historia, unaona hata panapokuwepo na mkusanyiko wa wakuu wa nchi wengi wengi, unaona jinsi ambavyo kila tukio linapotokea wanahitaji kusikia Mkuu wa Nchi wa Tanzania anasema kitu gani. Hili ni moja ya jambo ambalo linaitambulisha nchi yetu na linatwambia tunaye kiongozi bora. Mambo haya ambayo wanayaona ni haya haya ambayo tunayaona ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa sana imefanyika; niliorodhesha kwa kilefu siku ile wakati natoa mjadala, na tutaendelea kuyarudia mambo haya ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo kubwa lingine alilonalo Mheshimiwa Rais wetu ni zile *4R* ambazo alizianzisha. Hizo *4R* si kila mtu amejaliwa kipaji cha aina hiyo cha kuwasikiliza wengine.

Mheshimiwa Spika, hata sisi ni viongozi tunaweza tukajipima kwenye hayo, huwa tunaweza kuwavumilia walio chini yetu kwa kiwango gani. Iwe jimboni au iwe kwenye familia, unaweza ukaona ni namna gani Mheshimiwa Rais ana kipaji kikubwa sana cha kuheshimu mawazo ya wengine na kushirikisha hoja zinazotoka kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukianza na hoja ambazo zimejitokeza, kuna baadhi ya hoja nitazifafanua leo na kuna baadhi ya hoja tumezipokea na mtaziona tutakapokuwa tunajadiliana sheria yenyewe, kwa sababu zingine ni za kisheria. Nadhani kesho, kwa mujibu wa ratiba, tunakwenda kutunga sheria na mtaziona baadhi ya hoja ambazo tumezipokea na zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili ni Bunge linalowakilisha wananchi wake vizuri sana, hongereni sana Waheshimiwa Wabunge; na mimi nawaombea kwa wajumbe wote wawatendee haki kwa sababu mmewatendea haki katika kusimamia hoja zinazowahusu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja moja ilitolewa inayohusina na suala la kutoza kodi kwenye masuala ya gesi. Tumepokea hoja hii na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge watuvumilie. Wataalam wetu wanaendelea kukamilisha wakati tunaelekea kwenye kukukamilisha sheria ya kodi na bado tunamalizia. Hoja hii mmeisemea kwa nguvu kubwa sana, ninaomba nisitaje mmoja mmoja kwa sababu ya muda, Waheshimiwa Wabunge wengi sana mmeongelea jambo hili. Nawashukuru sana na tumepokea hoja hiyo kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi kubwa ambayo imeongelewa sana ilikuwa ni kuhusu adhabu ya milioni 15. Hoja hii kwanza ilinukuriwa vibaya; ilinukuriwa tofauti na lililokuwa limelengwa.

Mheshimiwa Spika, kilichokuwa kinalengwa kwenye sheria, na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tusikilizane kwenye hili halafu tuamue vile tunavyoweza kusonga nalo mbele.

Kilichokuwa kinalegwa mwaka jana, kwenye sheria ya mwaka jana tulitengeneza adhabu ambayo ilikuwa iko kwa asilimia; tuliweka kwa asilimia na asilimia tuliyoweka tulisema kwenye kile kiwango kidogo zaidi ambacho asilimia 20 yake ni ndogo sana kiasi kwamba yule anayekosea anaweza asione kama ameadhibiwa na kama anastahili kuacha kosa hili, adhabu tuliweka asilimia 20 ya vocha ya *invoice* ile ambayo itakuwa ina makosa.

Tukasema popote pale ambapo 20% hii tunaiona ni ndogo sana tutaweka kiwango cha chini kisichopungua 1,500,000. Kwa maana hiyo kwenye zile *transaction* ndogo sana ambazo 20% yake ipo chini ya 1,500,000 tukasema tutachukua 1,500,000. Hivyo ndivyo sheria tulivyokuwa tumeiweka, na hapa katikati kwa ajili ya kuweka usawa tukasema tutakuwa tunatoza 20% ya kosa lililogundulika nalo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama ni kosa lipo kiasi kadhaa ambayo ipo juu ya 1,500,000 inachukuliwa 20% yake. Sasa tulilokosea ambalo hatukuliweka ndio tulilotaka kurekebisha sasa hivi, tukasema popote pale ikizidi 15,000,000 hiyo 20% tunai-*cap* igote hapo kwa sababu makosa yanakuwepo yaliyo makubwa zaidi yanasababisha adhabu hiyo inakuwa kubwa sana kwa kiwango cha kutokulipika, yaani kwa mfano chukulia mtu akikutwa na vocha ya bilioni mbili; 20% ya bilioni mbili ni milioni 400. Kwa hiyo, kule ambapo tuliiacha iende wazi tukasema tui-*cap* kwamba itaenda 20%, 20%, 20% lakini ikizidi *fixed number* ya 15,000,000 inayotokana na hii 20% basi isipande iishie hapo, hicho ndicho tulichokuwa tumeweka.

Mheshimiwa Spika, tuliweka hivyo kwa sababu ukiweka tu namba moja mathalani milioni kumi unakuwa umewaumiza sana wale walio wadogo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo ilikuwa *logic* ya kuweka hiyo asilimia ambayo inapanda. Lengo la kuiwekea ukomo ilikuwa ni kwamba isije ikaenda sana kwenye maeneo ambapo vocha hiyo itakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tumepokea hoja za Waheshimiwa Wabunge na Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt.

Samia Suluhu Hassan ni sikivu na juzi tumekaa na wafanyabiashara chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na *Chief Whip,* Waheshimiwa Mawaziri, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila ndiyo alikuwa Mwenyekiti, tukajadiliana wakaunga mkono hiki tunachopendekeza kwa maana ya kuwekea ukomo usiende juu kwa sababu kwa kweli kuna mizigo mingine inayokuwa mikubwa sana inaleta madhara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wakasema tunavyoweka *range* kubwa hii inasababisha *negotiation* wakati wa utekelezaji wake unakuwa na ushawishi wa masuala ambayo siyo ya kimaadili na hicho ndicho ambacho wao na Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi wamekilalamikia sana. Pendekezo ambalo tutalileta bado tunakamilisha *consultation,* tunapendekeza ile 1,500,000 ibaki kama ilivyo na ile ya juu iishie milioni nne, hilo ndilo ambalo tunapanga tulifanye kama pendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi vitu ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamevisemea vinavyokosa maadili kwenye upande wa makusanyo ni kweli ni vitu ambavyo si vitu vya kupuuza, tumepokea sisi ndani ya Wizara, lakini pia kama Wizara tumeendelea kuongea na vyombo vinavyohusika na kusimamia haya masuala ya maadili ili kuweza kuhakikisha tunakomesha masuala haya ya upotevu wa fedha wakati wa ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna malalamiko ya aina hii ambayo yanajitokeza, mengine yanaanzia ngazi za vijiji, watu wanachukua *POS,* anakusanya, anaondoka na makusanyo, wengine tunagawana nusu kwa nusu, hivi kingine kinaenda Serikalini kingine kinapita njia hizo zingine, tumeyapokea hayo yote na tunayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika hoja nyingine ambayo imejadiliwa kwa kiwango kikubwa ni suala la fedha kwenda kwenye mifuko hii ya maendeleo inayosimamia hizi shughuli za maendeleo *TARURA, REA*, Mfuko wa Maji, Mfuko wa Barabara na maeneo mengine kama hayo. Hoja hii tumeipokea na kama ambavyo tulikuwa

tukiisema lililokuwa linajitokea ilikuwa inaathiriwa pale ambapo fedha ipo kwenye mifuko, lakini ipo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, tumeshalipokea hili na tumelifanyia kazi, katika mwaka wa fedha huo unaoanza fedha za mifuko hazitakuwa sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali ili zisiathirike kutokana na hali ya kifedha ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaziweka pembeni na tunapanga pia tufanye utaratibu huo huo kwenye fedha ambazo ni za wahisani na fedha zile ambazo utekelezaji wake wa miradi ndiyo unakaribisha fedha zaidi yaani zile za kupata fedha kutokana na unavyotumia maarufu kama *P4R,* kwa hiyo, hili jambo tutalifayia kazi na tumeshakubaliana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyongeza ya fedha tutalisemea zaidi kwa sababu kwenye barabara tunaongeza fedha mfuko wa dharura ambao utaweza kutumika katika kutengeneza masuala haya ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa maji, tumekubaliana na wenzetu wa Wizara ya Kisekta, mwaka jana katika mwaka wa fedha uliopita Serikali ilinunua mitambo ya kuchimba visima pamoja na mabwawa na kupima maji. Mitambo hii sasa ipo kila mkoa, kila mkoa una mitambo yake, tulisema kuliko tuendelee kujaza fedha kwa kutekeleza miradi hii kwa kutangaza zabuni na kujengwa kwa utaratibu wa zabuni, tukasema pia mitambo hii ambayo Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imenunua mipya na yenyewe iweze kutumika kuweza kuchimba visima, mabwawa ili kuhakikisha kwamba fedha ile ambayo ilitumika inaleta mrejesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge sisi sote tupo kwenye majimbo kule na utaratibu wa nchi yetu tunaujua, tusipoweka mkazo kwenye haya magari wananchi watakosa maji, magari yatakuwepo na magari haya yataota kutu. Kwa hiyo, nawaomba kule tunapokwenda mikoani kwetu tuhakikishe haya magari yanatumika, magari haya yatumike, Mheshimiwa Rais ameyaleta kwa ajili ya kuchimba visima. Haiwezekani

halmashauri ikakosa mpaka 15,000,000 ya kuchimba kisima katika eneo ambalo wananchi wamekosa kabisa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii tumeweka zaidi ya shilingi bilioni 41 kwenye ngazi ya Wizara kwa ajili ya kuchimba hivyo visima, lakini lazima pia halmashauri zetu ziwahurumie wananchi, tuunganishe nguvu na hiki ndicho ambacho tulikuwa tunasema, magari yapo yatumike, yachimbe visima ili kuweza kupunguza matatizo ya maji kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa ni suala la upungufu wa dola na matumizi ya dola, kwenye hili la upungufu wa dola tumesema ndani ya Serikali tumepitisha mkakati wa Serikali wa kuongeza upatikanaji wa dola ambao ndani yake sekta zote ambazo zinaweza kutuletea mapato zimejumuishwa katika mwaka wa fedha huu tunaoendelea nao. Hili ni jambo ambalo linatakiwa kuwa endelevu kwa sababu dola si sarafu ya nchi yetu, tunaipata dola kutokana na vitu tunavyouza nje, tunaipata dola kutokana na msaada, tunaipata dola kufuatana na mkopo na hasa hasa kwa nchi yoyote inayojali uendelevu tunatakiwa kuipata dola kutokana na mauzo yetu ya nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ni mkakati tumeuweka, umepitishwa na Baraza la Mawaziri na unaanza kutekelezwa. Baadhi ya mambo ambayo yamefanyika ni pamoja na uwekezaji kwenye sekta za uzalishaji, huu ni makakati wa muda mrefu ambao utatusaidia tunapokwenda tuweze kupata dola. Hata hivyo tunapokwenda mahitaji makubwa ambayo yalikuwa yanafanyika kufuatana na utekelezaji wa miradi mikubwa yanakuwa yanaenda yakipungua. Mfano bwawa la umeme tumeshamaliza maana yake *importation* ya vile vifaa ambavyo vilikuwa vinajenga bwawa havitahitajika tena. Tunahamia katika baadhi ya miradi ya kimkakati ambayo inatumia *importation* ya bidhaa hiyo na yenyewe itaenda kutusaidia kutupa ahueni huko tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya dola hapa nchini, tumeweka pendekezo hilo la kurekebisha sheria, natambua jambo hili liliwahi kufanyika mwaka 2007 nadhani Mama Zakia

Meghji akiwa Waziri wa Fedha na limefanyika juzi mwaka 2017 wakati Mheshimiwa Makamu wa Rais akiwa Waziri wa Fedha na jambo hili limekuwa likitolewa maelekezo haya, lakini limekuwa likipata upungufu katika utekeleaji wake.

Mheshimiwa Spika, nimeelekeza tunapoanza kutekeleza hili mwaka wa fedha huu unapoanza tunatengeneza na kanuni zake tutaweka na adhabu zake kwa sababu sheria ipo inayosema shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo yoyote ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo pia linatakiwa lilete heshima kwa nchi yetu, tuache kuifatilia dola inavyoenenda. Tunaposema tutumie dola, tutumie *Tanzanian Shilling*, tutumie fedha yetu ya Kitanzania, tunataka pia hata kunukuu bei zetu tuzinukuu kwa fedha ya Kitanzania, hatujasema tutumie fedha ya Kitanzania, lakini kwa kunukuu bei kwa kutumia dola. Haya ni mambo ambayo wenzetu wameyaweza ni sisi tu tunayaendekeza. Ukienda nchi za wenzetu tunapotembea kule hata hukutani, hamna sehemu ambayo unaweza ukakutana hata bei tu imetajwa kwa fedha ya kigeni, siyo hata mbali nenda Afrika Kusini hapa uone kama kuna eneo utalipia fedha ya kigeni. Nenda na maeneo mengine haukuti wanatumia fedha ya kigeni hata kunukuu bei. Twendeni tutaje bei kwa fedha ya Kitanzania, acheni dola itembee kivyake, hii ya kusema sasa dola ipo kiasi hiki, dola siyo fedha yetu achene itembee kivyake. Mbona tunaponukuu bei hatuulizi *pura* ya Botswana ipo kiasi gani ili tuweze kujua bei ya bidhaa hiyo ni kiasi gani, mbona hatuulizi *rand* ni kiasi gani, mbona hatuulizi *euro* ni kiasi gani. Acheni dola itembee kivyake, bei tuziweke kwa fedha ya Kitanzania. Wewe kama una shule ama una nyumba unatamani sana kupokea bei zake kwa dola nenda kajenge Marekani, mbona lipo wazi hili utapokea kwa dola na hamna mtu atakulalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twendeni bei za Tanzania ni sheria siyo Waziri wa Fedha anavyotaka ni sheria, *the legal tender* ni fedha halali ya malipo ya ndani ni shilingi ya Kitanzania tutaweka kanuni na tutaweka na adhabu. Tumeiweka hiyo na tutaweka na kanuni na tutaweka na adhabu, tutumie fedha yetu tunatengeneza

*pressure* ya kuitaka dola kutafutwa na inasababisha tushindwe kupata vitu vya muhimu kwa sababu ya vitu ambavyo tungeweza kuvifanya kwa fedha yetu ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anayetafuta leseni ya usafirishaji wa ndani tunamwambia kalete dola ya nini, mwananchi wa kawaida akalete dola, akaitafute wapi dola hiyo, hivyo hivyo na maeneo mengine. Twendeni tuwape kazi wageni kuitafuta shilingi ya Kitanzania kuliko kuwapa Watanzania kazi ya kuitafuta dola ambayo siyo fedha yao. Hii hapa Serikali tumesema tutatoa miongozo ili kuweza kuhakikisha jambo hili linatekelezeka na hili ni jambo ambalo ni la kisheria na Sheria ya Benki Kuu ndiyo inavyotuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la *cashless economy*, Waheshimiwa Wabunge wameongea sana kuhusu masuala ya *cashless economy,* tunaendelea nalo, ni jambo la msingi sana na hili wenzetu wameshapiga hatua. Ukienda hata siyo mbali sana hata majirani zetu tu hapo, hata ukinunua muhindi anakwambia ulipe kwa utaratibu wa lipa namba, wanafanya hivyo. Ukipanda bajaji wanakwambia ulipe kwa utaratibu wa lipa namba wanafanya hivyo, jambo hili Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwaambia hata wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Serikali tutaongeza jitihada za kujenga mifumo, kazi hii inafanyika pakubwa kuhakikisha kwamba ulipaji hauna matatizo kwa kutumia mifumo, tukishamaliza ulipaji hauna tatizo *then* tutaenda kwenye utaratibu wa *enforcement,* lakini kwa sasa hivi tunatamani tutangulize kwanza elimu na kujenga mifumo ili tutakaposema nchi nzima tuhamie kwenye utaratibu huo tuwe tumemaliza jambo la mifumo na tuwe tumemaliza suala la kuelimishana. Hili ni jambo ambalo tunaungana na hoja za Wabunge na ni hoja za kisasa kabisa, hoja makini kabisa zinazostahili kuwafanya wapiga kura wenu wawachague tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeongelewa ni jambo la Deni la Taifa, moja, naomba niweke wazi mambo machache kwenye hili suala la Deni la Taifa. Tuliongea kuhusu

deni lenyewe na nilielezea wakati wa kuhitimisha hoja. Mimi niweke wazi tu mambo machache; hili jambo la Deni la Taifa na wananchi walisikilize vizuri, moja hatutofautiani tu kuhusu *figure*, kuhusu jumla ya deni, lakini tunatofautiana kuhusu jambo la kwanza, kukopa kwenyewe hatujaelewana vizuri, hili jambo la kukopa, wengine wanadhani tunakopa wa sababu nchi yetu ni maskini, wengine wanadhani tunakopa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, wengine wanadhani ni Tanzania tu inayokopa.

Mheshimiwa Spika, moja hatukopi kwa sababu sisi ni maskini, tunakopa kwa sababu sisi ni matajiri. Maskini huwa hakopi, maskini hakopi kwa sababu hana cha kulipa, maskini haaminiki, hawezi kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo la umaskini ni *subjective*, ni jambo ambalo siyo *objective,* ni jambo ambalo tunaenda ngazi kwa ngazi. Yule aliye tajiri zaidi ndiyo mwenye deni kubwa zaidi duniani ipo hivyo, kwa hiyo, sasa hivi ukipanga ukubwa wa madeni anayeongoza ni yule mwenye uchumi mkubwa zaidi duniani na ndiyo mwenye deni kubwa zaidi duniani, hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, zile nchi zote kumi zinazoongoza kwa uchumi duniani ndiyo yenye madeni makubwa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija hapa Afrika ukipanga uchumi kama tunavyopangana kuanzia nchi yenye uchumi mkubwa zaidi hapa Afrika ndiyo yenye deni kubwa zaidi hapa Afrika. Nchi ya mwisho kwa uchumi hapa Afrika ndiyo yenye deni dogo zaidi na zingine hazina hata deni ni kwa sababu gani ukopaji ni utekelezaji tu wa mradi kwamba unachukua fedha kubwa kwa mara moja utekeleze mradi halafu ulipe kutokana na kipato kile ambacho ungekitekeleza kwa mwezi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata asiye mtumishi wa Serikali hawezi kukopa *salary advance,* ukiajiriwa ndiyo unaweza ukachukua *salary advance,* halafu unaanza kurudhisha kutokana na mshahara unaolipwa hii ipo hivyo. Kwa maana hiyo hili ambalo tunafanya kuliko ujenge reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma kwa makusanyo ya mwezi mmoja mmoja Watanzania tuelewane, ukichukua malipo ya mwezi mmoja mmoja ndiyo ukaanza kulipa

mradi mkubwa kama wa reli maana yake utamuweka yule anayejenga mkandarasi kwa miaka 50 au 60. Unachukua fedha ya miaka 20 unaiweka unalipia ule mradi uanze kukurudishia malipo yake halafu wewe kwenye makusanyo yale uanze kulipia kile ulichokikopa.

Mheshimiwa Spika, hata mimi tu hapa deni langu ni dogo kuliko deni la bilionea Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Musukuma lazima atakuwa na deni kubwa kuliko mimi, hata hapa hivyo hivyo. Mheshimiwa Mbunge wa kawaida kawaida hivi ambaye hana biashara kubwa deni lake halilingani na Mheshimiwa Mbunge mwenye biashara kubwa, hivyo ndivyo ilivyo, yeye atakuwa amekopa *salary advance,* lakini atakuwa amekopa *IFC,* atakuwa amekopa mpaka mabenki ya nje ya nchi, hicho ndicho ambacho tunatofautiana kuanzia mwanzo, hatukopi kwa sababu tupo maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakopa kwa sababu tunaaminika na tunakopa kwa sababu tunatekeleza miradi ya msingi ya kimaendeleo, hicho ndicho ambacho kinafanyika. Sheria moja ngumu sana iliyowekwa kwenye mambo ya mkopo ni ya nchi ya Tanzania ndiyo maana kwa Ukanda wa *SADC* na Ukanda wa *EAC* nchi moja ambayo deni lake limetajwa kwamba ni himilivu na linafuata masharti ni Tanzania na haya si maneno ya Serikali wala si maneno ya Waziri wa Fedha, ni wataalamu wanaochambua madeni wamesema Tanzania ndiyo nchi ambayo ipo na *B1+* kwa nchi zote za *EAC* na za *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Moody's* wamefanya mwaka jana, wamefanya na mwaka huu wamekuja na matokeo yale yale *fitch ratings,* wamefanya mwaka jana wamefanya na mwaka huu wamekuja na matokeo yale yale. Imetambulishwa duniani kote, ingekuwa taarifa ya *NBS* mngesema hii ni ya Serikali. Hawa ni wale magwiji wa kwenye eneo hili. Kwa hiyo, niliona niseme hili na taarifa hizi zinatuambia bado tupo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna mchangiaji mmoja alisema mbona *concessional loans* zimeongezeka wakati *commercial* zimepungua?

Mheshimiwa Spika, *concessional loans,* hii ni mikopo yenye masharti nafuu. Hizi ndio unaona *framework agreement* ambazo tunazipata ni kwa sababu tu, nchi inaheshimika na hizi ni nafuu, riba yake ni chini ya asilimia mbili. Ni tofauti na kwenda kukopa mkopo wa kibiashara ambao riba yake ni asilimia kumi, kumi na mbili na kuendelea. Kwa maana hiyo, hii kuongezeka ni akili kubwa sana ambayo Rais wetu ameitumia kuhakikisha tunakopa mikopo yenye masharti yaliyopoa. Mtu yeyote anayekopa angetamani apate masharti yaliyopoa. Nchi nyingine hawawezi wakapata hata hiyo, lakini hizi ni *PR,* ni mahusiano makubwa ya nchi yetu na nchi nyingine ambayo Rais wetu ameyajenga na hili ni jambo ambalo linasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Niwaondolee hofu Watanzania, hakuna siku Mtanzania atagongewa nyumbani kwake na mkusanya madeni kwamba, unadaiwa hapa nchi yako ilikopa, hakuna siku hiyo. Haya ni matumizi ya Serikali yatakuwepo kwenye Bajeti za Serikali kwa sababu, hicho ndicho ambacho kinafanya nchi inakopa kwa kuangalia Bajeti za Serikali. Sasa wenzetu wanaenda huko wanaanza kumwambia mwanakijiji aliyeko kule, ninyi hapa mnadaiwa; labda wao ndio wanawadai ile michango, kwa ajili ya kuendesha vyama vyao vya siasa, lakini Deni la Taifa hakuna siku Mtanzania mmoja atakutwa nyumbani kwake kwamba, wewe unadaiwa, kwamba ataswagiwa mifugo yake au atachukuliwa mahindi yake. Utaratibu wa uendeshaji wa nchi hauko namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona niseme hilo na nimalizie kwamba, kwenye masuala ya deni hakuna siku tunakopa, kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hii fedha yote inayokopwa inakwenda kwenye miradi ya maendeleo, miradi inayofungua uchumi wa Watanzania. Mathalani, zamani mtu alikuwa akitoka Mbeya kwenda Arusha inabidi apite Njombe, Iringa, Morogoro, Tanga ndio aende Arusha, lakini tukafungua njia ya kutoka Iringa kuja Dodoma na tukafungua njia ya kutoka Dodoma kwenda Manyara na tukafungua kwenda Arusha. Hata kama ule ni mkopo, lakini chachu tuliyoifanya kwenye uzalishaji kwa

wananchi ni jambo kubwa kuliko kwenda kuchukua mkopo wa aina hiyo. Niliona niliseme na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwenye kipengele hiki ni madeni ya wakandarasi na madeni ya wazabuni. Waheshimiwa Wabunge mmeliongea sana jambo hili. Serikali sikivu imesikia na jambo hili Mheshimiwa Rais ametukalisha mara kadhaa mimi pamoja na Mawaziri wa Kisekta, Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Wizara nyingine za Kisekta, Maji pamoja na Umeme. Hili ni jambo ambalo tunaliandalia mpango mahususi, tutakwenda kuwalipa, hasa hao wakandarasi wa ndani na sio tu kwamba, sasa hivi ndio tunaanza, kiporo chake kilikuwa kikubwa sana. Kuna watu hata walishasahau kama kuna siku watalipwa fedha hii. Tumpongeze sana Mama yetu, akasema walipeni hawa wakandarasi, ili fedha hii iongezeke kwenye mzunguko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulianza na shilingi bilioni 200, mwaka ule uliopita tukaenda shilingi bilioni 400, mwaka huu tulikuwa na shilingi bilioni 600 na sasahivi tuna utaratibu ambao tunaupanga. Tutatoa taarifa yake kupitia kamati yako ya Kibunge ambayo inatusimamia na tutatoa taarifa tutakapokuja hapa. Tunaweka mpango mkakati mahususi, wakandarasi, wazabuni pamoja na watoa huduma wa ndani watapewa kipaumbele hicho, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akielekeza, watapata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa matumizi. Hoja zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zinahusu kurekebisha *finance bill,* ni dhahiri zitaathiri mapato ambayo tulikuwa tumeyakadiria na Bajeti ya Serikali ya Wizara zote za Kisekta tulishaipitisha. Tumekaa na wataalam wangu tukakubaliana baadhi ya mambo ambayo yamepata baraka za Serikali. Tutakwenda kubana matumizi, ili kuweza kufidia fedha ambayo tumeshaipangia kwenye Wizara za Kisekta, kwa ajili ya kuhakikisha shughuli za maendeleo hazikwami.

Mheshimiwa Spika, moja; tulitenga fedha, kwa ajili ya kununua magari. Jambo hili la magari tuliliongelea hapa Bungeni na Bunge lilibariki jambo hili, linafanyiwa kazi kuweza kuhakikisha

kwamba, halileti usumbufu kiutekelezaji, linaendelea kufanyiwa kazi kuhakikisha ndani ya Serikali ni wapi wafuate mfumo upi na ni wapi wafuate mfumo upi. Kwa mfano, ni dhahiri askari anayefanya doria huwezi kumwambia nenda kwa gari lako kwa hiyo, kwenye upande wa vyombo hii hoja ya watumishi kupata magari yao itakuwa iko kando, lakini tumeangalia hata wale ambao wako *field*. Kwa hiyo, jambo hili liko linafanyiwa kazi na wenzetu wa utumishi, Mkuu wa Utumishi na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi, ili kuweza kupata utaratibu mzuri ambao utakuwa hauathiri shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tutakwenda kubana matumizi kwenye bajeti hii inayokuja. Nimemwelekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali kwenye takribani shilingi bilioni 129 ambazo zilikuwa zimewekwa kwa ajili ya kununua magari akate zaidi ya *fifty percent* abakize shilingi bilioni 50 tu wapeleke kwenye maeneo ambayo yatakuwa na umuhimu sana, kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Hivyohivyo kulikuwepo na takribani shilingi bilioni 67 ambazo zilikuwa za matumizi ya matengenezo akate kwa asilimia hamsini na hivyohivyo kwenye upande wa mafuta akate kwa asilimia hamsini. Fedha hizi zitakwenda kwenye miradi ya maendeleo ambayo itaathirika na marekebisho ya Sheria ya Fedha ambayo tayari tulishaiweka kwenye makadirio, zitakwenda kwenye miradi ya barabara, zitakwenda kwenye miradi ya maji, zitakwenda kwenye miradi ya umeme pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mmeongea kwa kiwango kikubwa sana kuhusu matumizi ya gesi na jambo hili ni rasilimali ambayo tunayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeelekeza kwenye fedha iliyokuwa imewekwa ya mafuta. Serikali ndio tunaenda kutoa mfano, tunaenda kuongoza kwa mfano kuhusu kutumia magari yanayotumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Serikali tunatumia mafuta, ndio matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya gesi kwenye magari kama mbadala wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali tunaenda kuwa mfano. Bahati nzuri sana Serikali huwa tunatumia kituo chetu ambacho ni cha Serikali chini ya bohari, kule ambako huwa tunatumia Serikali. Kwenye fedha tulizotenga za mafuta tutakwenda tukate fedha za mafuta tujenge hivyo vituo, tujenge Kituo Dodoma. Kama makadirio gari likijaziwa Dodoma halifiki Dar es Salaam, basi kijengwe na hapo Dar es Salaam, kijengwe na Morogoro na tutaendelea hivyo kujenga na *center* nyingine kubwakubwa ambazo zitasaidia kuweza kuhakikisha kwamba, jambo hili linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakata fedha ambazo tulishaziweka kwenye mafuta, tutaweka huo mfano, lakini pia, kama wenzetu wa *private sector* wameweza kuweka hiyo *dual* kwamba una fursa ya mafuta na una fursa ya gesi katika kipindi cha *transition,* hiyo na yenyewe tutaifanya na bahati nzuri sana *GPSA* iko chini ya Wizara ya Fedha kwa hiyo, maelekezo haya nimeyatoa waanze hivyo. Watakata bajeti ya mafuta tuweke hicho kituo kuweza kuhakikisha kwamba, utaratibu huo unafanyika. Ni lazima tuanze, lazima tuwe na pakuanzia kwenye jambo hili na ninaamini tutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye eneo hili ni fidia. Tumepokea hoja za Waheshimiwa Wabunge wote zinazohusiana na fidia, maeneo mengine yanahusisha uwekezaji, maeneo mengine yanahusisha maeneo ambayo yamechukuliwa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, tumepokea na tumeweka bajeti yake. Tuna maeneo kama Nyatwali, limeongelewa sana kwa upande wa uwakilishi, Mbunge wetu wa kutoka Bunda pamoja na jirani yake, tumepokea eneo hili. Kuna eneo la Kipunguni, limeongelewa sana hili na tumeshafanya vikao sana mpaka

ambavyo ame-*chair* Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Segerea ameliongea sana, Mheshimiwa Bonnah. Tumepokea hili na haya maeneo ya fidia tutaanzanayo.

Mheshimiwa Spika, tulitamani tuwe tumeshalipa Bunge hilihili na tulishatoa ahadi ya aina hiyo, lakini yalijitokeza, haya mambo ya mafuriko, ambayo tulilazamika kuyapa kipaumbele, hasa hasa ukiona maeneo ambako unakuta Mikoa miwili au mitatu inakuwa iko kisiwani, tulilazamika tuanze na hayo halafu tuendelee na haya ambayo tumeyaweka. Pia, nimeelekeza *OC* zitapunguzwa kwa asilimia 20, ili kuweza kuhakikisha kwamba, fedha hizo zinakwenda kwenye miradi ile ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambazo zilikuwa zinaendelea za upande wa wenzetu wafanyabiashara. Na mimi nawaomba ndugu zangu, sekta binafsi kwa ujumla, wakiwemo na wafanyabiashara ambao tumeongea mambo yao kwa kirefu sana na ninyi wawakilishi wao mmeliongea jambo hili kwa kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawaomba, Serikali inajali sana hoja hizo ambazo wenzetu wanazitoa. Serikali inajali sana, lakini la pili ni Serikali hii ni sikivu sana na inasikiliza sana hizo hoja za wenzetu hao walioko kwenye sekta binafsi. Moja ya jambo ambalo kwenye mtazamo wa kiuchumi wa Mheshimiwa Rais amelipa kipaumbele kikubwa ni kuhakikisha nchi hii uchumi wake unaongozwa na sekta binafsi, sisi Mawaziri ni nani hata tusitekeleze haya? Maono yake ni kuhakikisha uchumi huu unaongozwa na sekta binafsi, sisi Mawaziri ni nani hata tusitekeleze hilo? Kwa hiyo, kiongozi yeyote aliyeko Serikalini huu ndio mwelekeo wa Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba, tunailea sekta binafsi na sekta binafsi ina uwekezaji na ina biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge, jambo hili ninyi kule ndio wawakilishi wa wananchi, waambieni ndugu zetu hawa wala hatuna haja ya kuvutana kwa sababu, sisi Serikalini na wao tunaongea lugha moja. Mimi kila nikionananao huwa nawaambia hamhitaji hata kugoma kutekelezewa mambo yenu kwa sababu, kile mnachokisema ndicho Mheshimiwa Rais

anachoelekeza. Ingekuwa na maana sana kama mnachokisema Serikali iko kinyume na hicho, hapo ndipo ambapo nguvu huwa inatumika. Kwa hiyo, mimi nawaomba wenzetu wala tusijirudishe nyuma, sisi kama nchi, kwa mambo ambayo tunakubaliana mtazamo. Twende tuwe tunakaa tunaongea hoja moja-moja na tunapoongea hoja moja-moja tunaongelea nchi yetu na tunaongelea maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekaa na ndugu zetu hawa ambao tumewaambia wafanyabiashara kama Rais anawasikiliza anaweza kutenga siku nzima, huwa anakaa nanyi sekta binafsi anawasikiliza siku nzima. Waziri Mkuu alisimama pale, wao wenyewe wanajua, saa nane mpaka kumi anawasikiliza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amewasikiliza, sisi Mawaziri wa nne tumeenda tumewasikiliza, kama tunasikiliza na tunakubaliana hoja moja-moja na hatujakataa kuendelea kuzifanyia kazi, kwa nini tushinikizane kwa mgomo?

Mheshimiwa Spika, migomo hii inaturudisha nyuma kama Taifa na inarudisha nyuma familia moja-moja. Kwa hiyo, kwa sababu, tunasikilizana mimi rai yangu ni hatuna haja ya kutumia utaratibu wa nguvu, twendeni tuendelee na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana sekta binafsi walituambia tupandishe wigo ule wa kuandikisha *VAT,* tulifanya hivyo. Tulipotoka Kariakoo tulifanya hivyo na tukakubaliana tutandelea kwenda hatua kwa hatua. Hata hoja nyingine inawezekana zipo ambazo hatujatekeleza, sio kwa sababu ya kukataa, tumekuwa na hoja ambazo tumefanya *engagement;* kwa mfano, moja ya hoja ambayo ilikuwa inatolewa ilikuwa inahusisha kushusha *VAT* kutoka asilimia 18 kwenda asilimia 12. Hata mimi ningetamani iwe kumi na mbili, ningetamani iwe hata kumi, lakini hatujaacha tu kuishusha kwa sababu ya kiburi cha Wizara, wala hatujaacha kuishusha kwa sababu ya Serikali tu kukataa, tumeacha kushusha kwa sababu tuna mambo mengi tunatekeleza. Ukishusha asilimia mbili tu *VAT* unapoteza shilingi bilioni 600 kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, ukishusha hivyo na tuna miradi mikubwa, kama Taifa tunaitekeleza inaathiri bajeti, ukishusha kwa kiwango

hicho unakuwa na asilimia kumi, itaathiri. Wapo wengine wangedhani ukishusha hivyo, itaongeza *volume,* sasa kabla hujapata hiyo *volume* iliyoongezeka ukishusha na miradi ipo inatakiwa itekelezwe, inatekelezwaje? Kwa hiyo, tumesema twende nayo hatua kwa hatua na hii tunapunguza mzigo wa miradi, tunaenda kwenye huo utaratibu na Serikali ilishaweka hilo lengo la kuendelea kupunguza huo utaratibu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo hata ile *service levy; service levy* yetu hii, Waheshimiwa Wabunge ninyi mnatoka kule majimboni, inachangia zaidi ya asilimia 25 ya uendeshaji wa Halmashauri zetu sasa ukiitoa kwa mara moja kabla hujaleta mbadala kutakuwepo na *chaos* kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, hili na lenyewe tumeongea na wenzetu, tumelipokea, na tumesema tunatafuta utaratibu wa kuweza kupata mbadala wa uendeshaji wa Halmashauri zetu huku tukipunguza, ili ufanyaji kazi uwe mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walileta tuanzishe utaratibu wa bei elekezi; tumekubaliana na wenzetu wa sekta binafsi. Tutaanza na bidhaa nane kwa kuanzia kutekeleza utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na mambo ya *consolidation* na *deconsolidation;* tumekubaliana tunaanza kuanzia tarehe moja na wenzetu. Tutaanza kuanzia tarehe moja na wenzetu, tutaanza utekelezaji na mengine tunajenga mifumo.

Mheshimiwa Spika, haya mengine ambayo tunalalamikiana sasahivi ni *transitional,* tunakokwenda kule mbele tutaelewana. Kwa hiyo, mimi natoa rai kwa wenzetu hawa, wala tusiende kwenye utaratibu huu ambao unatusababishia matatizo kwa wote.

Mheshimiwa Spika, hivyohivyo na masuala ya kiukaguzi; hiyo na yenyewe tumesema tunakamilisha mifumo. Mfumo wa kodi za ndani pamoja na mfumo wa forodha ambayo itaenda kutuondolea haya matatizo ambayo yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo yamelalamikiwa ambayo ni ya kiutawala; tumeshapata ridhaa, Mawaziri wa Kisekta wala hatutawaita kituo kimoja, tutazunguka kule mikoani. *TRA* watakuwepo, Wizara ya Mipango itakuwepo, Wizara ya Biashara itakuwepo, Wizara ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI itakuwepo na Wizara ya Fedha itakuwepo. Tutatatua haya mengine ambayo ni ya kiutawala ambayo yanatukwamisha, wala hatuna haja ya kulumbana, nchi hii ni yetu sote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna mapendekezo mengine yalikuwa yametolewa ya kuwaondoa machinga Kariakoo, waondoeni machinga kwenye maeneo haya. Hilo na lenyewe, Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba, hatatumia nguvu ya dola wala migambo kuwaondoa machinga, atawatengenezea utaratibu mzuri wa kipato wa kufanya shughuli hizo, ili waweze kufanyia shughuli katika eneo mbadala bila kuathiri shughuli zao kwa hiyo, haya ndiyo ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneno ambayo tumeshafanya. Kwa mfano, Dodoma, mnaona pale ambapo wanafanya kazi ndugu zetu, wanafanya kazi nzuri kabisa. Hata Dar es Salaam tunajenga masoko, tukishamaliza mpangilio mzuri wa ufanyaji kazi utafanyika. Hii na yenyewe si kwamba, tumewakatalia wenzetu wafanyabiashara, lakini tulikuwa tunajali kwamba, wafanyabiashara ni watoto wa mama na ninawaheshimu sana na machinga ni watoto wa mama na nina waheshimu sana na sisi ndicho ambacho tunakitekeleza na hivyo ndivyo ambavyo Serikali inatekeleza. Yale mengine yote ambayo ni ya kiutawala, sisi kama Serikali tumeyapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine zote ambazo zilitolewa na Kamati ya Bajeti ambazo zinahusisha vifungu kwa vifungu, ninaweza nisipitie kifungu kwa kifungu kwa sababu, tumeenda kwenye vile vifungu na tumefanya *engagement* na kamati. *Almost* tumeelewana katika maeneo hayo ambayo walikuwa wameyaweka.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo na hoja nyingine ambazo zimetolewa na Mbunge mmoja mmoja; nyingine zimeshatolewa

majibu na Wizara za Kisekta, lakini zile ambazo zimetolewa na Wabunge kwenye hoja moja moja ambayo inahusiana na Sheria ya Fedha, tumezifanyia kazi, kesho tutakaposoma Hotuba ya Marekebisho ya Sheria ya Utungaji wa Sheria ya Mwaka huu tumeweka yale ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyasema. Tumeyarekebisha na tumeweka yale mengine ambayo tumeyafanyia marekebisho, ili kuweza kuhakikisha kwamba, hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema zinaweza kuonekana katika Sheria hii mpya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, narudia kwa kuwashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge. Bunge hili limekuwa Bunge makini sana, *Bunge objective* sana, ambalo linajali maslahi ya Taifa letu. Wabunge hawa tunashirikiana nao kuanzia kwenye kamati na mara zote wamekuwa wakitoa hoja zinazojenga nchi yetu na ndio maana Serikali imekuwa haipati ukakasi katika kukubaliana na hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila amesema, hoja hizi mwanzoni nilikuwa sijafanya utafiti huu, kumbe sio tu kwamba, zinatolewa na Waheshimiwa Wabunge wazalendo, lakini ni Wabunge ambao wanaelewa wanachokisema na ndio maana michango yao ambayo wanaitoa imekuwa michango makini sana. Kwa hiyo, sisi tumepokea hizo hoja zote, tutapata fursa ya hoja moja-moja na zile ambazo tutakuwa tumekubaliana na kamati tutakuwa tumekubaliana kwa niaba ya Bunge na tumefanya hivyo kwa *engagement* ya takribani muda wote ambao tumekuwa hapa, tumekuwa tukifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho. Namshukuru sana na kumpongeza Kaka yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, tunafanyanae kazi kwa ukaribu sana na mimi huyo ni kaka yangu na hii imerahisisha sana ufanyaji wa kazi kwa sababu, timu zetu wanakaa pamoja na wanafanya kazi vizuri sana. Ndio maana hata tunapokuwa na majukumu haya, tunapokwenda kwenye kamati tunaenda tukiwa na mambo ambayo sisi tumefanya kazi pamoja. Hivyo hivyo na Wizara za Kisekta tunafanya kazi kwa ukaribu sana na Wizara nyingine zote za kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwenye haya mambo ya kodi na mambo ya fedha tumefanya vizuri sana kazi pamoja na Wizara ya Mipango, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara zile za sekta za uzalishaji tumefanyanao kazi kwa pamoja kwa ukaribu sana kuweza kuhakikisha kwamba, masuala haya yanafanyiwa kazi ipasavyo. Tumefanya marekebisho mengi, mtayaona kesho.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilikuwa limeongelewa sana ni kuhusu hili lililokuwa linagusa sekta za uzalishaji. Tutakapokwenda kwenye kupitia vifungu vya Kisheria kuna mapendekezo ambayo tumesikiliza maoni ya Kamati ya Bunge pamoja na maoni ya Mbunge mmoja-mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Kitila ameongelea kuhusu uwekezaji tunaoufanya, ameongelea eneo la sekta ya sukari. Kuna jambo lingine lilikuwa linatolewa kuhusu, kama hivi tunavyoitwa maskini, hivi tutatoka lini?

Mheshimiwa Spika, kwanza hivi tunavyoongea Benki ya Dunia imeleta barua ambayo inasema wanatuma watu wa kufanya *evaluation,* kuangalia kama Tanzania inastahili kuendelea kuwa miongoni mwa nchi maskini zaidi Duniani. Kwa hiyo, zoezi hili linaendelea na wenzetu wanatuona. Mambo ambayo anayafanya Mheshimiwa Rais ni yale yanayoenda kutoa jawabu la kipato cha mtu mmoja-mmoja.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na hoja ambazo zilikuwa zinatolewa, za kitaalam tu kwamba, kipato cha mtu kimefika kiwango cha kipato cha mtu cha kati cha chini, lakini kulikuwepo na hoja za mtu mmoja-mmoja akijitokeza akisema, lakini tunaambiwa tuko kipato cha kati na kipato cha kati kiwango chake ni zaidi ya dola 1,040 ambayo ilishapatikana. Mtu mmoja-mmoja sasa anajiuliza, Je, hivi ni kweli mimi ninaipata hiyo?

Mheshimiwa Spika, zile zilikuwa *numbers.* Umechukuliwa wastani wa uzalishaji ndani ya nchi ukagawanywa kwa wastani wa idadi ya watu ndani ya nchi, lakini anachofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivi tunavyoona kwenye uwekezaji

kwenye sekta za uzalishaji, anaenda kutibu jambo la kipato cha mtu mmoja-mmoja kwa uhalisia wake. Ndio maana kwa sasa hivi tunaona zinakwenda shilingi bilioni 40 kwenye kijiji kutekeleza mradi wa umwagiliaji. Wale waliokuwa wanazalisha kwa uhafifu kwa mara moja wakizalisha mara tatu kwa ufanisi hawawezi kuendelea kuwa maskini kama walivyokuwa. Kwa hiyo, hii inaenda kutibu lile tatizo la kipato cha mtu mmoja-mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zimekwenda kwenye vijiji kwa kiwango ambacho hazijawahi kutokea, zinakwenda kwenye sekta ya uzalishaji. Tumeona kwenye umwagiliaji, lakini tumeona hata kwenye hii *BBT* ambayo inaendelea kwa sekta zote. Hii inawapeleka vijana wawe kazini, huwezi ukainua kipato cha mtu mmoja-mmoja ukiwa una-*unemployment* kubwa kwenye nchi husika. Kwa hiyo, hii inayowapeleka vijana wawe kazini inaenda kutibu kipato cha mtu mmoja-mmoja na *future* ya nchi hii iko kwa vijana. Lazima tuwapeleke vijana wawe kazini na tukishawapeleka utaona kwamba, kipato cha mtu mmoja-mmoja kitakwenda kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, suala la marejesho tumeliongea ni suala la kiutawala. Suala la kero bandarini kati ya mtu mmoja-mmoja anapobeba mzigo kutoka Bara kwenda Zanzibar na kutoka Zanzibar kuja Bara tumelichukua ni la kiutawala. Tutayafanyia kazi hayo kuweza kuhakikisha kwamba, hayaleti matatizo.

Mheshimiwa Spika, tumepokea masuala ya akaunti za wafanyabiashara, yaliongelewa masuala ya *M-koba Bank* pamoja na maeneo mengine yanayohusiana na hayo. Tumeyapokea na ninadhani ni masuala ya kiutawala, tutaenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, haya ya kuifanya *NFRA* iagize sukari; wale tunaowaita wafanyabiashara ni wafanyabiashara na wale wenye viwanda na wenyewe ni wafanyabiashara. Sisi tumeona, ili kuweza kutibu suala la bei ya sukari, hasa inayohusiana na masuala ya upungufu, tutumie taasisi hii ambayo imesaidia

kwenye bei ya bidhaa nyingine kuweza kuhakikisha kwamba, inamfikia mlaji katika bei inayohusika.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo linalokera pale Serikali inapotoa msamaha, ni wale walioko kwenye hiyo sekta, wanaofanya kazi za biashara, kudhania ule msamaha uliwalenga wao. Tumeona haya katika maeneo mengi; tulitoa kwenye *smarts phone,* simu janja na vitu vingine, badala ya kuwanufaisha Watanzania ikakwamia katikati. Tulitoa kwenye *dippers* badala ya kuwanufaisha Watanzania ikakwamia katikati, hata kuna wakati tulikuwa tunatoa shilingi bilioni 100, kwa ajili ya kushusha bei ya mafuta, hata hiyo haikwenda asilimia yote kwa maana kwamba, bei ile imnufaishe mia kwa mia yule ambaye Mheshimiwa Rais alikuwa amemlenga.

Mheshimiwa Spika, hivyohivyo na kwenye sukari. Bei imekuwa ikishuka, lakini bila kutumia huu utaratibu kumekuwepo na matatizo ndio maana Waziri wa Kisekta aliona kwa utaratibu huu ni lazima hili jambo tulisimamie, ili Mtanzania aweze kunufaika ipasavyo. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tumeona haya mambo ni lazima tuyafanyie utawala wa karibu, ili kuweza kuhakikisha kwamba, yanamnufaisha Mtanzania mmoja-mmoja ambaye alikuwa amekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda huu kwa mara nyingine. Hoja hizi, kama nilivyosema, zote tumezichukua na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huu, kwa mara nyingine nakushukuru wewe mwenyewe na wataalam wote ambao wamefanya kazi ikawa nyepesi, nawashukuru na Waheshimiwa Wabunge. Naomba sasa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini kwa utaratibu wetu nilipaswa kuwahoji, lakini wote tunafahamu hoja hii inakuja leo jioni na kila Mbunge ataitika kwa jina lake kusema kama anaiunga mkono hoja hii au hapana ama vinginevyo. Kwa hiyo, zoezi la kuwahoji litafanyika tutakaporejea kwenye sehemu ya pili ya kukutana kwetu leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo matatu hapa. Tangazo la kwanza ni la wageni ambao waliingia baada ya matangazo yaliyopita:-

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri wa Ujenzi, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Wageni watano wa Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mvumi, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma.

Wengine ni Wageni saba wa Mheshimiwa George Joseph Kakunda, ambao ni Walimu kutoka Sikonge, Uyuwi na Nzega, Mkoa wa Tabora. Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Pia, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ambao ni familia yake kutoka Karatu Mkoa wa Arusha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Tangazo la pili linatoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wabunge wote ambao ni wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* zilizopo eneo la Medeli Jijini Dodoma kuwa, kutakuwa na kikao baina yenu na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kikao hicho kitafanyika leo katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuhitimisha zoezi la kuzindua kitabu, kama ambavyo lilitangazwa hapo awali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao ni wapangaji huko Mheshimiwa Waziri anataka kuonana nanyi.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho:-

Nawakumbusha mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge hapa, wote tuelekee Ukubi wa Msekwa, kwa ajili ya uzinduzi wa Kitabu cha Taarifa zinazohusu mambo ya Bunge. Kwa hiyo, ni muhimu sana sisi wote kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni, leo.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. *(Makofi/Vigelegele)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo nilivyokuwa nimesema kipindi cha kwanza tulipokutana leo kabla hatujaahirisha, wakati mlipokuwa mkiunga mkono tulikubaliana kwamba mtahojiwa tutakaporejea. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 125 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwa siku zisizozidi saba Bunge limeelekezwa kujadili hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Kama mtakumbuka ili kukidhi takwa hili la kikanuni mjadala huo ulianza tarehe 18 Juni, 2024 na kuhitimishwa asubuhi ya leo

tarehe 26 Juni, 2024. Baada ya mjadala huo kuhitimishwa Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 126(1) ya Kanuni zetu inasema Bunge litaidhinisha Makadirio ya matumizi ya Serikali. Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya Serikali umewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 126(2) ambapo utafanywa kwa kupigwa kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja kuamua kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo sasa nitamwita Katibu hapa ili tuweze kuanza zoezi hilo la kumwita Mbunge mmoja baada ya mwingine na kila mmoja atakuwa anatoa uamuzi wake kuhusu bajeti hii.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kuitika kama unakubali kwa mujibu wa Kanuni zetu utasema ‘Ndiyo’, kama unakataa utasema ‘Hapana’, kama utakuwa haujaamua utasema ‘Sijaamua’. Hivyo ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Kama utakuwa umepiga kura ambayo haina uamuzi utasema hivyo na sasa nimwite Katibu ili tuweze kuanza zoezi letu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**KUPIGA KURA**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Mussa Azzan Zungu | – | Ndiyo |
| Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko | – | Ndiyo |
| Mhe. Job Yustino Ndugai | – | Ndiyo. |
| Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | – | Ndiyo. |
| Mhe. Salma Rashid Kikwete | – | Hayupo |
| Mhe. Najma Murtaza Giga | – | Ndiyo. |
| Mhe. Joseph Kizito Mhagama | – | Ndiyo |
| Mhe. Deodatus Philip Mwanyika | – | Hayupo |
| Mhe. Mansour Shanif Jamal | – | Ndiyo |
| Mhe. Taufiq Salim Turky | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi | – | Ndiyo |
| Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika | – | Ndiyo |

Mhe. Jenista Joakim Mhagama – Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene – Ndiyo
Mhe. Innocent Lugha Bashungwa – Ndiyo
Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo – Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu – Ndiyo
Mhe. Mohamed Omar Mchengerwa – Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji – Ndiyo
Mhe. Hussein Mohamed Bashe – Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa – Ndiyo
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba – Ndiyo
Mhe. January Yusuf Makamba – Ndiyo
Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax – Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela – Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni – Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro – Ndiyo
Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda – Ndiyo
Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima – Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana – Ndiyo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso – Ndiyo
Mhe. Nape Moses Nnauye – Ndiyo
Mhe. Angellah Jasmine Kairuki – Ndiyo
Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo – Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega – Ndiyo
Mhe. Antony Peter Mavunde – Ndiyo
Mhe. Jerry William Silaa – Ndiyo
Mhe. Deogratius John Ndejembi – Ndiyo
Mhe. Daniel Baran Sillo – Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete – Ndiyo
Mhe. Dkt. Festo John Dugange – Ndiyo
Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe – Ndiyo
Mhe. David Ernest Silinde – Ndiyo
Mhe. Khamis Hamza Khamis – Ndiyo
Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga – Ndiyo
Mhe. Paschal Patrobass Katambi – Ndiyo
Mhe. Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe – Ndiyo
Mhe. Hamad Hassan Chande – Ndiyo
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa – Ndiyo
Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk – Ndiyo
Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato – Ndiyo

| | |
|---|---|
| Mhe. Geophrey Mizengo Pinda | – Ndiyo |
| Mhe. Jumanne Abdallah Sagini | – Ndiyo |
| Mhe. Omari Juma Kipanga | – Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel | – Ndiyo |
| Mhe. Mwanaidi Ali Khamisi | – Ndiyo |
| Mhe. Eng. Maryprisca Winfred Mahundi | – Ndiyo |
| Mhe. David Mwakiposa Kihenzile | – Ndiyo |
| Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo | – Ndiyo |
| Mhe. Judith Salvio Kapinga | – Ndiyo |
| Mhe. Alexander Pastory Mnyeti | – Ndiyo |
| Mhe. Dunstan Luka Kitandula | – Ndiyo |
| Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma | – Ndiyo |
| Mhe. Zainab Athman Katimba | – Ndiyo |
| Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | – Ndiyo |
| Mhe. Fakharia Shomar Khamis | – Ndiyo |
| Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly | – Ndiyo |
| Mhe. Rashid Abdallah Shangazi | – Ndiyo |
| Mhe. Janejelly James Ntate | – Ndiyo |
| Mhe. Halima James Mdee | – *Abstain* |
| Mhe. Khalifa Mohammed Issa | – *abstain* |
| Mhe. Zahor Mohammed Haji | – Ndiyo |
| Mhe. Vita Rashid Kawawa | – Ndiyo |
| Mhe. Dennis Lazaro Londo | – Ndiyo |
| Mhe. Ally Juma Makoa | – Ndiyo |
| Mhe. Moshi Selemani Kakoso | – Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza | – Ndiyo |
| Mhe. Jackson Gedion Kiswaga | – Ndiyo |
| Mhe. Fatma Hassan Toufiq | – Ndiyo |
| Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | – *Abstain* |
| Mhe. Dkt. David Mathayo David | – Ndiyo |
| Mhe. Timotheo Paul Mnzava | – Ndiyo |
| Mhe. Deus Clement Sangu | – Ndiyo |
| Mhe. Husna Juma Sekiboko | – Ndiyo |
| Mhe. Oran Manase Njeza | – Ndiyo |
| Mhe. Florent Laurent Kyombo | – Ndiyo |
| Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri | – Ndiyo |
| Mhe. Vincent Paul Mbogo | – Ndiyo |
| Mhe. Justin Lazaro Nyamoga | – Ndiyo |
| Mhe. Riziki Said Lulida | – Ndiyo |

Mhe. Anna Richard Lupembe – Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile – Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhani Sima – Ndiyo
Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara – Ndiyo
Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan – Ndiyo
Mhe. Agustine Vuma Holle – Ndiyo
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga – Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula – Ndiyo
Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda – Ndiyo

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Twaha Ali Mpembenwe – Ndiyo
Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi – Ndiyo
Mhe. Abdallah Dadi Chikota – Ndiyo
Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo – Ndiyo

**SPIKA:** Katibu hebu subiri. Mheshimiwa Abdallah hebu itikia kwenye kisemeo kingine.

Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo – Ndiyo

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Abdi Hija Mkasha – Ndiyo
Mhe. Abdul Yussuf Maalim – Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood – Ndiyo
Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma – Ndiyo
Mhe. Abdullah Ali Mwinyi – Ndiyo
Mhe. Abeid Ramadhani Ighondo – Ndiyo
Mhe. Abubakari Damian Asenga – Ndiyo
Mhe. Agnes Elias Hokororo – Ndiyo
Mhe. Agnes Mathew Marwa – Ndiyo
Mhe. Agnesta Lambert Kaiza – *Abstain*
Mhe. Ahmed Ally Salum – Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali – Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby – Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani – Hayupo
Mhe. Aleksia Asia Kamguna – Ndiyo

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Dkt. Alfred James Kimea | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Hassan Omar King | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Juma Mohamed | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Khamis Yahya | – | Ndiyo |
| Mhe. Ali Vuai Khamis | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage | – | Ndiyo |
| Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila | – | Ndiyo |
| Mhe. Ally Mohamed Kassinge | – | Ndiyo |
| Mhe. Yahya Ally Mhata | – | Ndiyo |
| Mhe. Aloyce Andrew Kwezi | – | Ndiyo |
| Mhe. Aloyce John Kamamba | – | Ndiyo |
| Mhe. Amandus Julius Chinguile | – | Ndiyo |
| Mhe. Ameir Abdalla Ameir | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Ali Mzee | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Bakar Yussuf | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Daud Hassan | – | Ndiyo |
| Mhe. Amina Iddi Mabrouk | – | Ndiyo |
| Mhe. Amour Khamis Mbarouk | – | Ndiyo |
| Mhe. Anastazia James Wambura | – | Ndiyo |
| Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest | – | Hayupo |
| Mhe. Angelina Adam Malembeka | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula | – | Ndiyo |
| Mhe. Antipas Zeno Mgungusi | – | Ndiyo |
| Mhe. Anton Albert Mwantona | – | Ndiyo |
| Mhe. Asha Abdullah Juma | – | Ndiyo |
| Mhe. Asia Abdukarimu Halamga | – | Ndiyo |
| Mhe. Assa Nelson Makanika | – | Ndiyo |
| Mhe. Asya Mwadini Mohammed | – | *Abstain* |
| Mhe. Asya Sharif Omar | – | Ndiyo |
| Mhe. Athuman Almas Maige | – | Ndiyo |
| Mhe. Atupele Fredy Mwakibete | – | Ndiyo |
| Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe | – | Ndiyo |
| Mhe. Aziza Sleyum Ally | – | Ndiyo |
| Mhe. Bahati Keneth Ndingo | – | Ndiyo |
| Mhe. Bahati Khamis Kombo | – | Ndiyo |
| Mhe. Bakar Hamad Bakar | – | Ndiyo |
| Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa | – | Ndiyo |
| Mhe. Benaya Liuka Kapinga | – | Ndiyo |
| Mhe. Benardeta Kasabago Mushashu | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Boniphace Mwita Getere | – | Ndiyo |
| Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo | – | Ndiyo |
| Mhe. Boniventura Destery Kiswaga | – | Ndiyo |
| Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli | – | Hayupo |
| Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata | – | Ndiyo |
| Mhe. Catherine Valentine Magige | – | Ndiyo |
| Mhe. Cecil David Mwambe | – | Ndiyo |
| Mhe. Cecilia Daniel Paresso | – | *Abstain* |
| Mhe. Charles John Poul Mwijage | – | Ndiyo |
| Mhe. Charles Muguta Kajege | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | – | Ndiyo |
| Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka | – | Ndiyo |
| Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza | – | *Abstain* |
| Mhe. Condester Michael Sichalwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Constantine John Kanyasu | – | Ndiyo |
| Mhe. Cosato David Chumi | – | Ndiyo |
| Mhe. Daimu Iddi Mpakate | – | Ndiyo |
| Mhe. Daniel Awack Tlemai | – | Ndiyo |
| Mhe. Deo Kasenyenda Sanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Dorothy George Kilave | – | Ndiyo |
| Mhe. Edward Olelekaita Kisau | – | Ndiyo |
| Mhe. Edwin Enosy Swalle | – | Ndiyo |
| Mhe. Elibariki Immanuel Kingu | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai | – | Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Peter Cherehani | – | Ndiyo |
| Mhe. Eric James Shigongo | – | Ndiyo |
| Mhe. Ester Amos Bulaya | – | *Abstain* |
| Mhe. Esther Edwin Malleko | – | Ndiyo |
| Mhe. Esther Lukago Midimu | – | Ndiyo |
| Mhe. Esther Nicholas Matiko | – | *Abstain* |
| Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa | – | Ndiyo |
| Mhe. Felista Deogratius Njau | – | *Abstain* |
| Mhe. Festo Richard Sanga | – | Ndiyo |
| Mhe. Flatei Gregory Massay | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Florence George Samizi | – | Ndiyo |
| Mhe. Florent Laurent Kyombo | – | Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Francis Isack Mtinga | – Ndiyo |
| Mhe. Francis Kumba Ndulane | – Ndiyo |
| Mhe. Fredrick Edward Lowassa | – Ndiyo |
| Mhe. Furaha Ntengo Matondo | – Ndiyo |
| Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe | – Ndiyo |

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, hebu itika tena.

| | |
|---|---|
| Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe | – Ndiyo |
| Mhe. George Natany Malima | – Ndiyo |
| Mhe. George Ranwell Mwenisongole | – Ndiyo |
| Mhe. Ghati Zephania Chomete | – Ndiyo |
| Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi | – Ndiyo |
| Mhe. Grace Victor Tendega | – *Abstain* |
| Mhe. Haji Amour Haji | – Ndiyo |
| Mhe. Haji Makame Mlenge | – Ndiyo |
| Mhe. Hamida Mohamed Abdallah | – Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla | – Ndiyo |
| Mhe. Hamisi Shabani Taletale | – Ndiyo |
| Mhe. Hasan Seleman Mtenga | – Ndiyo |
| Mhe. Hassan Zidadu Kungu | – Ndiyo |
| Mhe. Hawa Mchafu Chakoma | – Ndiyo |
| Mhe. Hawa Subira Mwaifunga | – *Abstain* |
| Mhe. Hussein Nassor Amar | – Ndiyo |
| Mhe. Iddi Kassim Iddi | – Ndiyo |
| Mhe. Innocent Edward Kalogeris | – Ndiyo |
| Mhe. Innocent Sebba Bilakwate | – Ndiyo |
| Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe | – Ndiyo |
| Mhe. Issa Ally Mchungahela | – Ndiyo |
| Mhe. Issa Jumanne Mtemvu | - Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Kainja Andrea | - Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | - Ndiyo |
| Mhe. Jafari Wambura Chege | - Ndiyo |
| Mhe. Jaffar Sanya Jussa | – Ndiyo |
| Mhe. Janeth Elias Mahawanga | – Ndiyo |
| Mhe. Janeth Maurice Massaburi | – Ndiyo |
| Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi | – Ndiyo |
| Mhe. Jesca David Kishoa | – Ndiyo *(Makofi)* |

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Jesca Jonathani Msambatavangu – Ndiyo
Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo – Ndiyo
Mhe. John Marko Sallu – Ndiyo
Mhe. Jonas Van Zeeland – Ndiyo
Mhe. Jonas William Mbunda – Ndiyo
Mhe. Joseph Anania Tadayo – Ndiyo
Mhe. Joseph George Kakunda – Ndiyo
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma – Ndiyo
Mhe. Joseph Michael Mkundi – Ndiyo
Mhe. Joseph Zacharius Kamonga – Ndiyo
Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima – Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege – Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke – Ndiyo
Mhe. Josephine Tabitha Chagula – Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako – Ndiyo
Mhe. Juliana Daniel Shonza - Ndiyo
Mhe. Juliana Didas Masaburi - Ndiyo
Mhe. Juma Hamad Omar – Ndiyo

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma itika tena.

Mhe. Juma Hamad Omar – Ndiyo
Mhe. Juma Othman Hija – Ndiyo
Mhe. Juma Usonge Hamad – Ndiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba – Ndiyo
Mhe. Kabula Enock Shitobelo – Ndiyo
Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni – Ndiyo
Mhe. Kassim Hassan Haji – Ndiyo
Mhe. Katani Ahmadi Katani – Ndiyo
Mhe. Kavejuru Eliadory Felix – Ndiyo
Mhe. Kenneth Ernest Nollo – Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud – Ndiyo
Mhe. Khadija Shaaban Taya – Ndiyo
Mhe. Khalifa Salum Suleiman – Ndiyo
Mhe. Khamis Kassim Ali – Ndiyo
Mhe. Khamis Yussuf Mussa – Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala – Hakuwepo

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Latifa Khamis Juwakali | – | Ndiyo |
| Mhe. Leah Jeremiah Komanya | – | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho | – | Hakuwepo |
| Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula | – | Ndiyo |
| Mhe. Livingstone Joseph Lusinde | – | Ndiyo |
| Mhe. Lucy John Sabu | – | Ndiyo |
| Mhe. Lucy Thomas Mayenga | – | Ndiyo |
| Mhe. Luhaga Joelson Mpina | – | Hakuwepo |
| Mhe. Maida Hamad Abdallah | – | Ndiyo |
| Mhe. Maimuna Ahmad Pathan | – | Ndiyo |
| Mhe. Maimuna Salum Mtanda | – | Ndiyo |
| Mhe. Margaret Simwanza Sitta | – | Ndiyo |
| Mhe. Mariam Nassoro Kisangi | – | Ndiyo |
| Mhe. Mariam Madalu Nyoka | – | Ndiyo |
| Mhe. Martha Festo Mariki | – | Ndiyo |
| Mhe. Martha Nehemia Gwau | – | Ndiyo |
| Mhe. Mary Francis Masanja | - | Ndiyo |
| Mhe. Maryam Azan Mwinyi | – | Ndiyo |
| Mhe. Maryam Omar Said | – | Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Masache Njelu Kasaka | – | Ndiyo |
| Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki | – | Ndiyo |
| Mhe. Maulid Saleh Ali | – | Ndiyo |
| Mhe. Mbarouk Juma Khatib | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani | – | Ndiyo |
| Mhe. Michael Costantino Mwakamo | – | Ndiyo |
| Mhe. Michael Mwita Kembaki | – | Ndiyo |
| Mhe. Minza Simon Mjika | – | Ndiyo |
| Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu | – | Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi | – | Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Lujuo Monni | – | Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Suleiman Omar | – | Hakuwepo |
| Mhe. Mohammed Maulid Ali | – | Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Said Issa | – | *Abstain* |
| Mhe. Mrisho Mashaka Gambo | – | Ndiyo |
| Mhe. Muharami Shabani Mkenge | – | Ndiyo |
| Mhe. Munde Tambwe Abdallah | – | Ndiyo |
| Mhe. Munira Mustapha Khatib | – | Ndiyo |
| Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab | – | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Mwanakhamis Kassim Said | – | Ndiyo |
| Mhe. Mwantakaje Haji Juma | – | Ndiyo |
| Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | – | Ndiyo |
| Mhe. Mwantumu Mzamili Zodo | – | Ndiyo |
| Mhe. Mwantumu Dau Haji | – | Ndiyo |
| Mhe. Mwita Mwikabe Waitara | – | Ndiyo |
| Mhe. Nancy Hassan Nyalusi | – | Ndiyo |
| Mhe. Nashon William Bidyanguze | - | Ndiyo |
| Mhe. Ndaisaba George Ruhoro | - | Ndiyo |
| Mhe. Neema Gerald Mwandabila | – | Ndiyo |
| Mhe. Neema Kichiki Lugangira | – | Ndiyo |
| Mhe. Neema William Mgaya | – | Ndiyo |
| Mhe. Ng'wasi Damas Kamani | – | Hakuwepo |
| Mhe. Nicholaus George Ngassa | – | Ndiyo |
| Mhe. Nicodemas Henry Maganga | – | Ndiyo |
| Mhe. Njalu Daudi Silanga | - | Ndiyo |
| Mhe. Noah Lemburis Saputu Mollel | – | Ndiyo |
| Mhe. Norah Waziri Mzeru | – | Ndiyo |
| Mhe. Nusrat Shaaban Hanje | – | Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Oliver Daniel Semuguruka | – | Ndiyo |
| Mhe. Omar Ali Omar | – | *Abstain* |
| Mhe. Omar Issa Kombo | – | Ndiyo |
| Mhe. Omari Mohamed Kigua | - | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo | – | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi | – | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato | – | Ndiyo |
| Mhe. Pauline Philipo Gekul | - | Ndiyo |
| Mhe. Philipo Augustino Mulugo | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya | – | Ndiyo |
| Mhe. Priscus Jacob Tarimo | – | Ndiyo |
| Mhe. Rashid Abdallah Rashid | – | Ndiyo |

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Salma Rashid Kikwete | – | Ndiyo |
| Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika | - | Ndiyo |
| Mhe. Ravia Idarus Faina | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Regina Ndege Qwaray | – | Ndiyo |
| Mhe. Rehema Juma Migilla | – | Ndiyo |
| Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo | – | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati | – | Ndiyo |
| Mhe. Robert Chacha Maboto | – | Ndiyo |
| Mhe. Rose Cyprian Tweve | – | Ndiyo |
| Mhe. Rose Vicent Busiga | – | Ndiyo |
| Mhe. Saada Monsour Hussein | – | Ndiyo |
| Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe | – | Ndiyo |
| Mhe. Salim Alaudin Hasham | – | Ndiyo |
| Mhe. Salim Mussa Omar | - | Ndiyo |
| Mhe. Salome Wycliffe Makamba | – | Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Salum Mohammed Shaafi | - | *Abstain* |
| Mhe. Samweli Xaday Hhayuma | - | Ndiyo |
| Mhe. Santiel Eric Kirumba | – | Ndiyo |
| Mhe. Sebastian Simon Kapufi | – | Ndiyo |
| Mhe. Seif Khamis Said Gulamali | - | Ndiyo |
| Mhe. Seif Salim Seif | – | Hakuwepo |
| Mhe. Selemani Jumanne Zedi | – | Ndiyo |
| Mhe. Shabani Omari Shekilindi | – | Ndiyo |
| Mhe. Shally Josepha Raymond | – | Hakuwepo |
| Mhe. Shamsia Azizi Mtamba | – | Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya | – | Ndiyo |
| Mhe. Silyvetry Francis Koka | – | Ndiyo |
| Mhe. Simai Hassan Sadiki | – | Ndiyo |
| Mhe. Simon Songe Lusengekile | – | Ndiyo |
| Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda | – | *Abstain* |
| Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo | – | Ndiyo |
| Mhe. Soud Mohammed Jumah | – | Ndiyo |
| Mhe. Stella Ikupa Alex | – | Ndiyo |
| Mhe. *Eng.* Stella Martin Manyanya | – | Ndiyo |
| Mhe. Stella Simon Fiyao | – | *Abstain* |
| Mhe. Subira Khamis Mgalu | – | Ndiyo |
| Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | – | Ndiyo |
| Mhe. Suma Ikenda Fyandomo | – | Ndiyo |
| Mhe. Sylvia Francis Sigula | – | Ndiyo |
| Mhe. Tabasam Hamis Mwagao | – | Ndiyo |
| Mhe. Tamima Haji Abass | – | Ndiyo |
| Mhe. Tarimba Gulam Abbas | – | Ndiyo |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Taska Restituta Mbogo | – | Ndiyo |
| Mhe. Tauhida Gallos Cassian | – | Ndiyo |
| Mhe. Tecla Mohamedi Ungele | – | Ndiyo |
| Mhe. Tumaini Bryceson Magessa | – | Ndiyo |
| Mhe. Tunza Issa Malapo | – | *Abstain* |
| Mhe. Ussi Salum Pondeza | – | Ndiyo |
| Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo | – | Ndiyo |
| Mhe. Venant Daud Protas | – | Ndiyo |
| Mhe. Wanu Hafidh Ameir | – | Ndiyo |
| Mhe. William Vangimembe Lukuvi | – | Ndiyo |
| Mhe. Yahaya Omary Massare | – | Ndiyo |
| Mhe. Yustina Arcadius Rahhi | – | Ndiyo |
| Mhe. Zacharia Paulo Issaay | – | Hakuwepo |
| Mhe. Zaytun Seif Swai | – | Hakuwepo |
| Mhe. Zubeida Khamis Shaib | – | Ndiyo |
| Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka | – | Ndiyo |
| Mhe. Zuena Athumani Bushiri | – | Ndiyo |
| Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Ndiyo |

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tumemaliza *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, Katibu sasa ataenda kuhesabu kura namna zilivyopigwa kisha ataniletea hapa majibu nikishayapata nitawatangazia kama Bajeti ya Serikali imepita au vinginevyo. Kisha tutaendelea na jambo litakalofuata baada ya maamuzi haya.

*(Hapa Wabunge walisubiri matokeo ya upigaji wa Kura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025)*

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nilikuwa nauliza kwa ajili ya waliosema "Ndiyo", "Hapana" na

*"Abstain"* akashuhudie zile kura maana yake ameenda mmoja, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hesabu namna zinavyopigwa ndiyo maana hazina uwakala kule mbele ni kura ya wazi siyo kura ya siri. Kwa hiyo hapa zitatangazwa zote waliosema "*abstain"* watajisikia wenyewe kwamba kura yangu na mimi imo maana wanajulikana wako wangapi na waliosema "ndiyo" pia wanajulikana wako wangapi. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi hazihitaji mawakala kwa sababu ni kura za wazi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nimesikiliza wakati tunapiga kura, kuna waliosema *"Abstain"* na waliosema "Ndiyo" kuna mwingine amesema "Abusteini" sasa ile inahesabiwa wapi? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma hayo maneno yote mawili uliyoyasema mbona kama yote yanafanana au yana utofauti yoyote?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, moja ni "Abuu" moja ni "Apuu". *Abstain* na "Apuu" *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, katika kulisikiliza neno hilo, hiyo "u" iliyoongezeka hapo Katikati inasomeka "a, b" hamna "u" imesikika, lakini siyo "u" inasomeka hapo kwa hiyo ni "*a b s t a i n*" ni neno la kigeni jamani kwa hiyo inaruhusiwa.*(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikiliza haya maneno ya *abstain* kwa muda mrefu; hivi Kiswahili chake ni kipi?

**SPIKA:** Haya mtaalamu wa Kiswahili.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Ahaa kumbe mtaalamu wa Kiswahili anajijua, haya Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *Abstain* maana yake ni epukana/jinyima; ni epukana au kujinyima kitu, *abstain*. Nasoma kwenye *dictionary.*

**SPIKA:** Haya, sasa ngoja basi tumsaidie tafsiri. Kwa Kiswahili kwa sababu inaonekana maneno yanaweza kuwa mengi, lakini ukisema mtu ame-*abstain* maana yake hajaamua kuamu kwenye suala la kura. Yaani amechagua kutokuamua.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, neno kuu ni kuepukana.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Samahani kidogo. Mheshimiwa Almas Maige hapo mwisho umesemaje?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, neno kuu ni ameepukana/kuepukana.

**SPIKA:** Ndiyo, ameepuka kuamua.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ame-*abstain,* ku-*abstain* ni kuepukana.

**SPIKA:** Sawa, ndiyo ameepuka kuamua kwa sababu tunazungumzia kura.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Haya sawa, ngoja, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wenzangu hawakutaja kanuni zilizowasimamisha na kuomba mwongozo, na mimi ninasimama vivyo hivyo. Bunge lako linafuata Kanuni za *Commonwealth* na sehemu nyingine. Waheshimiwa Wabunge imekuwa kama wanatania, lakini kiukweli naomba mwongozo wako, uweze kueleza tunapokuwa tunapiga kura kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano tunapozungumzia kutokukubaliana au kukubaliana maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba mwongozo wako. Ikiwezekana na ikikufaa uweze kuweka semina kuweza kuwaeleza Wabunge wako ni namna gani kuna umuhimu wa kuomba kusema ndiyo au hapana. Ninaposema ndiyo ninamaanisha nini na ninaposema hapana namaanisha nini; na faida na madhaa yake ni nini. Tunaomba utuelezee kwa sababu Bunge lako ni Bunge linalokusanya chama tawala na vyama vya upinzani. Sasa naomba *seriously* kabisa uweze kutoa kanuni na maelezo ili watu wako waweze kupata wasitusumbue tunaposema lile neno ambalo Musukuma amelisema pale.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mohamed Said.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako, huyu Mheshimiwa Almas Maige asichukuliwe kwamba amekosea kwa sababu ni kawaida ya wanyamwezi na wasukuma kwamba wanatumia nguvu sana wanapozungumza. Hii lugha ilitakiwa iwe ya Taifa lakini kwa sababu wakiongea wanatumia nguvu ikaonekana kwamba mtu akiwa ni mgonjwa hataweza kusema. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Almas Maige asitafsiriwe vibaya.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu ni kwamba kura zinazotambulika kikanuni ziko tatu. Kura ya kwanza ni ya kukubali au kusema ndiyo, kura ya pili ni ya kukataa au kusema hapana na kura nyingine ni ya kutokuamua. Kwa hiyo, hii ya kutokuamua ndiyo hii ambayo wakati mwingine linatumika neno la Kingereza. Kwa hiyo, kuliko mtu aseme sijaamua anaona bora atumie neno hilo alilolitumia. Kwa hiyo, ambaye hajaamua asijisikie vibaya; kikanuni anaruhusiwa kabisa kupiga kura ya namna hiyo. Mheshimiwa Deo Sanga.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, tumekaa hapa kwa muda mrefu tukijadili bajeti za Wizara mbalimbali. Sasa nataka Mwongozo wako, wenzetu hawa walipitisha bajeti za Wizara mbalimbali, leo ambayo ndiyo sasa tunapitisha ziende kufanya kazi wanakataa kwamba hapana, nataka Mwongozo, hela hizi ambazo wamezikataa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kura zile nyingine kwa mujibu wa kanuni zetu huwa tunatazama wingi wa ndiyo au hapana lakini kura ya leo ni kura ya wazi. Kwa hiyo, ndiyo maana

tumesikia watu wakipiga kura kwa uhuru ambao Katiba yetu inatoa lakini pia kanuni zetu zinatoa. Kwa hiyo, hii leo ndiyo kura hasa ya bajeti.

## MATOKEO YA KURA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitangaze matokoe ya kura. Mbunge aliyesimama atafute kiti aketi; naam. Matokeo ya kura iliyopigwa kwa wazi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 126. Idadi ya Wabunge wote kikatiba ni 393. Idadi ya Wabunge waliopo mpaka sasa ni 393, lakini idadi ya Wabunge waliokuwepo Bungeni ni 381; idadi ya Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni 12. Kura za hapana ni 0; kura za ndiyo ni 362; na kura za hakuamua, zile zilizoitwa *abstain* ni 18, kwa idadi hiyo ya kura Bajeti ya Serikali imepitishwa kwa kura 362, sawa na asilimia 92.3, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunafuata hatua nyingine ya muhimu. Baada ya hiyo hatua nyingine ya muhimu inayofuata kisha nitazungumza machache.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2024
### *(The Appropriation Bill, 2024)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi 49,345,687,645,000 (shilingi trilioni arobaini na tisa, bilioni mia tatu arobaini na tano, milioni mia sita themanini na saba, mia sita arobaini na tano elfu) kwa matumizi ya Serikali kutoka katika mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2025, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo *(A bill for an act to applya sum of forty nine trillion three hundref forty*

*five billion, six hundred eighty seven million, six hundred forty five thousand shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending 30th day of June, 2025 to appropriate the supply granted for that year, to authorize reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2024**
***(The Appropriation Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi 49,345,687,645,000 (trilioni arobaini na tisa, bilioni mia tatu arobaini na tano, milioni mia sita themanini na saba, mia sita arobaini na tano elfu) kwa matumizi ya Serikali kutoka katika mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2025, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo *(A bill for an act to applya sum of forty nine trillion three hundref forty five billion, six hundred eighty seven million, six hundred forty five thousand shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending 30th day of June, 2025 to appropriate the supply granted for that year, to authorize reallocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2024 (The Appropriation Bill, 2024) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Muswada huo kusomwa kwa mara ya tatu kwa taratibu tulizojiwekea, sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoafikiana na Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024 *(The Appropriation Bill, 2024)* waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2024 *(The Appropriation Bill, 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. Baada ya kupitisha Muswada huu, sasa utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili na yeye aweze kufanya kazi yake ya kikatiba ya kusaini Muswada huu ili sasa uwe sheria na uweze kuanza kutumika.

Muswada huu kwa utaratibu wa kikatiba na kikanuni zetu huwa unapitishwa kwa sura hiyo kwa sababu tunakuwa tayari tumeshajadili bajeti na hapa tumeshapiga kura. Kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba sasa tunataka yale mafungu yote tuliyoyapitisha basi yawe kisheria, ndiyo maana huwa unapitishwa hakuna hoja na hakuna mjadala juu ya Muswada huu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ni kwa sababu tunakuwa tumeshajadili tayari hayo mambo na tunakuwa tumeshayakubali.

Nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa sababu kwa kura ambayo Waheshimiwa Wabunge mmepiga mmepitisha hoja ambazo Mawaziri hawa wawili walikuwa wamezileta mbele yetu.

Kwanza, leo tumepitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Pia tumepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/3025. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mawaziri hawa wawili, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote waliochini ya Wizara hizi na tunawatakia kila heri katika utekelezaji wa yale yote ambayo Bunge limewapitishia mafungu leo.

Nafahamu safari ilikuwa ni ndefu kidogo na bado inaendelea kidogo lakini nitumie fursa hii kwa ujumla wake; kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuweza kufikia hatua hii ni kwa sababu Wizara mbalimbali zilipata nafasi ya kuleta hapa makadirio na mapato na matumizi kwenye Wizara zao na Bunge likapata nafasi ya kuzijadili nanyi mkaenda kuyaweka pamoja yale yote ambayo yalikuwa yamejadiliwa na kupitishwa hapa ndani. Kwa hiyo, Mawaziri wote na Naibu Mawaziri tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya mpaka tumefikia hapa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu zoezi hili ni endelevu kwa maana ya kwamba bado tutaendelea kesho na keshokutwa; lakini naishukuru Serikali kwa ujumla wake kwa ushirikiano ambao wameuonesha kwa Bunge kipindi chote hiki na naamini wataendelea kutoa ushirikiano katika hizi siku chache zilizobaki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Esther Matiko alikuwa ameomba Mwongozo; naona anaashiria kwamba ameridhika na mambo yaliyoenda, kwa hiyo hakuna Mwongozo, Mheshimiwa Esther matiko ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shuguli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 11.53 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 27 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*